3ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kwanza- Tarehe 10 Mei 2017

(Kikao Kilianza saa 3.00 Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

(Hapa Wimbo wa Taifa wa Zanzibar uliimbwa kuashiria kuanza kwa Mkutano)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe Kwanza nichukue fursa hii kuwakaribisha sana katika mkutano wetu huu wa Sita wa Baraza letu la Tisa ambao unaanza leo tarehe 10 Mei, 2017.

Waheshimiwa Wajumbe hivi karibuni tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya vifo vya wanafunzi ishirini na tisa (29) pamoja na walimu wao watatu (3) vilivyotokea huko Mkoani Arusha, ambavyo vilisababishwa na ajali ya gari. Vifo hivyo vimeacha majonzi makubwa kwa wazazi wa wanafunzi hao, walimu wao, wananchi wa Mkoa wa Arusha na Watanzania wote kwa ujumla, vimetugusa sana sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azipumzishe salama roho za marehemu hao na awajaalie nyoyo za subra wazazi, walimu na marehemu hao na Watanzania kwa ujumla.

Aidha, salamu zetu za rambirambi zimfikie Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, kwa msiba huo mkubwa ambao Taifa umeupata. Tutaendelea kuwakumbuka marehemu hao.

Waheshimiwa Wajumbe pia tunafahamu kuwa mvua zinazoendelea kunyesha sehemu mbali mbali nchini zimeleta athari kubwa katika maeneo mbali mbali katika visiwa vyetu vya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla. Miongoni mwa athari hizo ni baadhi ya nyumba kuharibika na

miundombinu ya maeneo mbali mbali kuathirika. Tukiwa Wawakilishi wa wananchi tunatoa salamu zetu za pole kwa wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa maafa hayo yaliyotokana na mvua hizo.

Waheshimiwa Wajumbe nitawaomba tusimame kwa dakika moja ili tuwaombee dua marehemu ambao niliotangulia kuwasema.

Ahsanteni.

(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walisimama kwa dakika moja kwa kuombeleza msiba huo)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe baada ya taarifa hiyo ya huzuni, napenda kutoa kwenu na kwa wananchi kwa ujumla taarifa kuhusu Miswada ya Sheria iliyopitishwa katika Mkutano uliopita wa Baraza uliofanyika kuanzia tarehe 15 Februari, 2017 mpaka tarehe 3 Machi, 2017.

Katika Mkutano wa Tano wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Baraza hili lilipitisha Miswada mitatu (3) ya sheria ambayo ni:-

1) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya 1992 na Kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

2) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam.12 ya 2004 na Kutunga Sheria inayoweka Masharti Bora Yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya 2016 na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

3) Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya 2006.

Aidha, katika Mkutano wa Nne wa Baraza uliofanyika mwezi Novemba, 2016, miongoni mwa Miswada iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi ni pamoja na Mswada wa:-

Sheria wa Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na

Uuzaji Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 91(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016; naomba kutoa taarifa kwamba Miswada ifuatayo sasa imekuwa Sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:-

Sheria zenyewe ni:-

1) Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

2) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya 1992 na Kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

3) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam.12 ya 2004 na Kutunga Sheria inayoweka Masharti Bora Yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya 2016 na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

4) Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya 2006.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana.

Ahsanteni. *(Makofi)*

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba Mwenyezi Mungu atujaalie Baraza letu hili lifikie malengo yake na tumalize bajeti yetu hii kwa salama, amin.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha mezani nakala zote za Gazeti rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia Tarehe 4 March, 2017.

Mhe. Spika: Endelea kwa sababu bado upo wewe.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba tena kuwasilisha mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Omar Seif Abeid (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani kuhusu hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rai kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kutokana na dharura iliyojitokeza maswali tutakayojibu mwanzo ni ya Wizara ya Ujenzi Mawasiliano usafirishaji, kwa hivyo nitamuita Mhe. Simai Mohammed Said aulize swali lake Nam. 55.

Nam. 55

Faida ya Usafiri wa Anga Kwa Wazanzibari

Mhe. Abdalla Maulid Diwani (Kny: Mhe. Simai Mohamed Said) – Aliuliza:-

Kwa kuwa usafiri wa anga ni miongoni mwa mambo ya Muungano, ni faida gani Zanzibar inaipata kifedha pamoja na ajira kutokana na sekta hii ya usafiri wa anga.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 55 ambapo Mheshimiwa alitaka kujua faida gani tunazozipata kutokana na sekta hii ya usafiri wa anga.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa kwamba sekta ya anga ni miongoni mwa mambo ya Muungano. Sekta hii imeweza kutoa ajira nyingi kwa wananchi wetu si hapa Zanzibar tu bali hata Tanzania Bara. Kuna faida kubwa sana ambayo Serikali yetu imekuwa ikiipata kupitia sekta hii kutokana na safari za ndege za ndani na zile za nje ya nchi ambapo moja wapo ya mambo ambayo tunafaidika nayo ni katika kuitangaza nchi yetu katika sekta ya utalii.

Kuna kampuni mbali mbali za ndege na vijana wetu kutoka hapa Zanzibar na kutoka nje ya Zanzibar ambazo zimekuwa zikitoa huduma za usafiri hapa nchini, hivyo kuingiza mapato mengi kwenye serikalini yetu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Ni kweli tumeona usafiri wa anga umeshika hatamu sana katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na dunia nzima, lakini wakati tunapotumia ndege hizi kuna tatizo linajitokeza japo Sheria za *Aviation* haziruhusu.

Je, Zanzibar hatuoni sababu ya kutunga Kanuni kulazimishwa kwamba ndege zile ndogo ziwe na *co-pilot.*

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Spika: Si Mhe. Simai huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kauliza binafsi sasa hivi.

Mhe. Spika: Ndio ni lake yeye.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa hivyo napenda kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba imefika wakati wa kuangalia kuhusu hili suala la rubani mmoja katika ndege zetu, lakini kama nilivyosema mwanzo haya ni mambo ya Muungano. Hata karibuni tulikuwa na kikao na Kamati ya Ardhi na Mawasiliano tumeliona hili. Kwa hivyo tutapeleka taarifa kuanzia sasa ili

tuangalie kwamba hizi Kanuni zifanyiwe marekebisho hapa inapowezekana kutokana na usalama wa wananchi wetu.

Ahsate sana Mhe. Spika.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nishukuru kupata nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu amesema tumeweza kufaidika wananchi wa Zanzibar katika sekta hii, nilitaka kujua labda tumefaidika wananchi wangapi kiajira katika sekta hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo sekta hii ya usafiri wa anga ni sekta mtambuka. Kwa hivyo watu wengi wanafaidika kwa ajira tofauti, wapo wanaofaidika kwa kuuza tiketi, wapo wanaofaidika kwa kupeleka usafiri wao *Airport*, wako wanaofaidika vile vile kwa kuwepo katika mashirika haya tofauti ya ndege.

Kwa hivyo kusema la kweli ni wengi waliofaidika na huwezi kusema kwamba ni idadi fulani lakini kusema la kweli sekta ya utalii sasa hivi pia ni sekta ambayo vijana wetu wengi wameajiriwa, kwa hivyo pia nao wamefaidika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashkuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza.

a) Mimi namuuliza Naibu Waziri kwamba Shirika la Ndege la Tanzania lina uwiano gani au lina mapato gani moja kwa moja yanayohusiana na Zanzibar.

(b) Ndio sababu ambayo Shirika la Ndege la *Air Tanzania* ni sababu ya kushindwa kufunguliwa kwa Shirika la Ndege la Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mapato yote yanayoingia katika mfuko wa fedha za pamoja ambapo sisi Zanzibar tunapata asilimia 4.5 ya mapato yote hayo. Kwa hivyo *ATCL* pia nao mapato yake yakiingia kule na sisi tunapata gawio.

Kuhusu suala lake la pili hii sio sababu ya kutufanya sisi tusifungue shirika bali kutokana na vipaumbele vyetu hivi sasa tumeweka vipaumbele zaidi katika usafiri wa baharini na karibuni mtapata taarifa kwamba tunataka tununue meli mbili. Kwa hivyo tukishakumaliza vipaumbele hivyo suala lako tutaliangalia zaidi na linazungumzika.

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa maelezo ya ziada.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba niongeze majibu yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri ambayo ameshatoa kwenye swali la faida, ningependa niongezee kama ifuatavyo.

Kwanza usafiri wa anga ni suala la Muungano lakini pia Shirika hili ni miongoni mwa mashirika ya Muungano, lakini kama sote tunavyojua Shirika lilisita kufanya kazi zake kwa muda mrefu na hivi sasa ndio limeanza kurudi kufanya kazi zake, bado faida haijapatikana kwa sababu Shirika bado limo katika kujijenga. Lakini kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri faida ya mashirika ya Muungano yanatakiwa kwa sasa yanaingia katika mfuko au hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar inapata mgao wake wa 4.5. Lakini pale Shirika hili litakapopata faida ndio faida hiyo tutaweza na sisi kuipata.

Lakini pamoja na hayo kuna ripoti ya Tume ya Pamoja ya Fedha na ripoti hii bado inafanyiwa kazi na Serikali zetu mbili kwa maana ya kuangalia pia mgao wa Zanzibar. Kwa maana ya kwamba ama uongezwe kutoka hapo ulipo sasa hivi wa asilimia 4.5 lakini kwa sasa hivi hatujawa na faida ya moja kwa moja tunayoipata kutokana na Shirika la Ndege la Tanzania.

Nam. 122

Uhamisho wa Wafanyakazi wa Kiwanja cha Ndege Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye Taasisi za Ulinzi wafanyakazi huwa si vyema kuwepo katika kituo cha kazi kwa muda mrefu sana. Na kwa kuwa katika Uwanja wa Ndege wa *Karume Airport* Pemba kuna baadhi ya wafanyakazi waliohudumia hapo kwa zaidi ya miaka kumi na tano (15) jambo ambalo hupunguza utendaji bora wa majukumu ya kazi zao.

(a) Je, ni lini Serikali itawabadilishia vituo vya kazi wafanyakazi ambao wameshahudumia kwa muda mrefu kwenye Uwanja wa Ndege wa Pemba.

(b) Je, ni wafanyakazi wangapi ambao wameshahudumia uwanjani hapo kwa muda mrefu na ambao wanatarajiwa kufanyiwa mabadiliko ya vituo vya kazi ili kubadilisha uzoefu wa kazi.

Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Ni kweli kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi wa taasisi za ulinzi ambao wamekuwa wakihudumia katika Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba kwa muda mrefu sasa. Hata hivyo, Mamlaka imeliona hilo na hivi karibuni zoezi la kuwabadilisha vituo watendaji hao limeanza katika viwanja vyetu vya Unguja na Pemba.

b) Mhe Spika, kwa sasa Mamlaka haiwezi kutambua ni wafanyakazi wangapi kwa vile wafanyakazi hao wanatoka katika taasisi za Uhamiaji, Jeshi la Polisi ambazo ni taasisi za mamabo ya Muungano.

Aidha kwa wafanyakazi wa Zima Moto nao wanaendelea na hilo zoezi na karibuni tu nilikuwa Pemba wakatwambia kwamba kuna wafanyakazi ambao wanataka kuwabadilisha ili waondoke pale katika kituo kimoja walichozowea. Kwa hivyo ndio taarifa Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo yamenifurahisha lakini nilikuwa nataka kumuuliza kwa kuwa amekiri kwamba hawawajui wafanyakazi ambao wapo baadhi ya wafanyakazi kutoka taasisi nyengine za ulinzi ambazo zina mahusiano na Bara.

Je, haoni kwamba kukosekana hivyo kukosa serikali kuwatambua au Wizara kuwatambua wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye taasisi yake ni kosa, jambo ambalo linaweza kusababisha hata kukosekana inapotokea hitilafu yoyote pale kuwatambua pahali gani wawafuate, haoni kwamba hilo ni tatizo Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, wale wafanyakazi si kama hatuwatambui, tunawatambua lakini mambo ya ajira na kila kitu ni mambo ya Muungano. Nataka kumuhakikishia ni karibuni tu mimi nilikuwa na ziara na Mhe. Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. Hamad Yussuf Masauni na katika agizo alilolitoa kwa Mkuu wa Uhamiaji ni kuhakikisha kwamba na Polisi vile vile baadhi ya wafanyakazi *Airport* na Bandarini wanaondoshwa. Kwa hivyo ni kweli hivi sasa ukenda pale *Airport* wafanyakazi wa Polisi hasa Kitengo cha Madawa ya Kulevya na wale wa Uhamiaji wengi wamebadilishwa.

Kwa hiyo hizo ni kazi za Taasisi ya Muungano ambazo wao hatuwezi kuwaingilia katika mambo yao na jambo la pili kama ulivyosema sisi tuna mashirikiano mazuri kwa sababu moja wapo ya kazi zetu za Viwanja vya Ndege ni kuhakikisha tunalinda usalama wa viwanja vyetu vya ndege. Kwa hivyo mawasiliano yetu mazuri na tunajua kwamba wafanyakazi wangapi wanakuwa wanaingia *shift*, wangapi wanatoka ili na sisi tuendelee na kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu zetu. Lakini mambo ya kuwajua wangapi wamehamishwa, wangapi hawajahamishwa ni mambo ya Wizaraya Mambo ya Ndani. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Bismillah Rahman Rahim, Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuuliza swali la ziada lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Waziri majibu yake mazuri sana lakini anaposema suala la Muungano hawezi kuwaingilia sasa Zanzibar inahusika vipi kwenye suala la Muungano, kwa masuala kama hayo yenye matatizo yanapotokezea hasa yaliyoulizwa na suala lenyewe la kuwa na *pilot* vile vile. Kajibu kwamba swali hili liko Muungano tatizo keshaona kwamba kuna athari anaweza kuuwa mtu *pilot* mmoja, watu zaidi ya ishirini na nguvu gani kwenye suala la Muungano munaweza mkalitilia mkazo mkaamua wenyewe Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumwambia kwamba Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, kuhusu swali lake la nyongeza kwamba sisi tuna mahusiano mazuri na wanzetu wa sekta tofauti zilizokuwepo Uwanja wa Ndege za mambo ya Muungano.

Kama nilivyokwambia kwamba hili swali ambalo Kanuni zake ni za Kimuungano huko tunazungumza nao na Mwenyekiti wa hiyo Bodi ni kutoka Zanzibar na tumempelekea maombi yetu hayo na wamesema kwamba watayafanyia kazi. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Nadir astahamili kwa sababu hata sisi linatugusa na hatupendi katika ndege zetu hizi watu wapande wakiwa na hofu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri katika wafanyakazi wako wa ulinzi ambao wanamilikiwa na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, yapo malalamiko ambao wafanyakazi hao kwanza na wao wanakaa kwa muda mrefu kinyume hata yale masaa ya kazi wanaotakiwa kukaa.

Malalamiko yao yanagusa katika maeneo mawili. Moja ni kukaa kwa muda mrefu lakini la pili ni kutokubadilishwa katika mazingira ya kazi zao. Je, ni lini Taasisi yako itawapa haki zao stahiki zile za kufanya kazi kwa muda wa ziada lakini na kubadilishwa wakapangiwa wengine na ili na wao wawe na mazingira ya kupumzika, nazungumzia wafanyakazi wa Mamlaka yenyewe ya Anga ambao ni walinzi wanaokaa milangoni na kunako zile mashine zenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake lenye kifungu (a) na (b) la nyongeza kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba huwa karibu sana na wafanyakazi hasa katika ile sekta yangu zote sio pale tu katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, wanapokuwa na malalamiko yako wananambia na mimi huwa nayafanyia kazi. Sasa kama kuna malalamiko haya ambayo umenielezea leo mbele ya kikao chako hichi kitukufu basi mimi Mhe. Spika, nachukua ahadi kwamba nitayafanyia kazi na baadae nitampa majibu inshallah. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nadhani nyote mmepata taarifa ya msiba ambao nimeupata. Kwa hivyo naomba nichukue nafasi hii nimpishe Mhe. Naibu Spika ili shughuli hizi ziendelee. Mhe. Naibu Spika, karibu sana.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

Nam. 127

Utekelezaji wa Ahadi ya kutoa Kompyuta Skuli ya Ndagoni

Mhe. Suleiman Makame Ali – Aliuliza:

Mwezi Novemba, 2013 Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alifungua jengo la Skuli ya Ndagoni lenye vyumba vinne na aliahidi

kutoa kompyuta mbili na printer moja kwa niaba ya MBM Mhe. Shawana Bukheti Hassan. Hata hivyo, ahadi hiyo bado hadi leo haijatekelezwa.

Je, ni lini kompyuta na printer hizo zitapelekwa skuli ya Ndagoni ili kukamilisha ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake Nam. 127 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Suleiman Makame Ali kwa kuikumbushia ahadi yake ya kukabidhi kompyuta mbili na *printer* moja ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliyotolea wakati wa ufunguzi wa Jengo la Skuli ya Ndagoni Pemba.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri kuwa ahadi hii ni ya muda mrefu kwa dhati kabisa naahidi itatekelezwa wakati wowote pale ambapo hali itakaporuhusu. Ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kukubali kwamba ahadi hii imekuwa ya muda mrefu, huu ni mwaka wa nne tena kwa ufunguzi wa Skuli ile ya Ndagoni mnamo mwaka wa 2013 mpaka hadi hii.

Mhe. Naibu Spika, katika majibu ya Mhe. Waziri amenambia kwamba hali itakaporuhusu, sikatai na hilo hivi sasa tunakwenda katika bajeti hali itakaporuhusu lini 2018, 2019, 2020/2021 na je, huoni kwamba ni kuwakatisha tamaa wananchi wangu wa Shehia ya Ndagoni kutokana na kwamba kompyuta hizo zina gharama kiasi gani mpaka leo hii niambiwe hali itakaporuhusu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Sawa sawa Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu msingi. Jambo la kwanza nikiri lakini hatua ya pili kweli ahadi hii imekuwa ya muda mrefu lakini tukiamini kwamba kinachofanywa na Mhe. Waziri au kinachofanywa na Ofisi yetu kwamba ni kutekeleza ahadi hizi kwa kipindi chote ambacho kwa sababu ahadi hii inakwenda sambamba na Chama cha Mapinduzi, na tukiizungumzia Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sasa ahadi zake zote ni kuanzia mwaka 2015/2020 na tunaendelea kumuomba sasa Mhe. Mwakilishi kwa hilo atustahamilie hali itakaporuhusu tutampa vifaa vyake katika Skuli ya Ndagoni nakushukuru.

Nam. 118

Utaratibu wa Kupata Vyeti vya Kuzaliwa

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa kuna idadi kubwa ya watu wenye umri kuanzia miaka 40 na kuendelea ambao hawana vyeti vya kuzaliwa.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuwepo kwa idadi ya watu ambao hawana vyeti vya kuzaliwa kunasababisha Serikali kutokujua takwimu halisi ya watu wake na kutowezesha Serikali kujipangia mpango wake wa maendeleo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vyeti vya kuzaliwa Wazanzibari ambao hawana vyeti hivyo vya kuzaliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kombe Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 118 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2010 na Idara ya Uchumi na Takwimu za Kijamii ya Umoja wa Mataifa inayoelezea hali halisi ya usajili wa matukio ya kijamii ya nchi wanachama za Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afika (*SADC*), inaonesha kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri katika usajili wa vizazi ikiwa ina nafasi ya pili nyuma ya Mauritius kwa kuweza kusajili asilima 90 ya vizazi vyake. Takwimu hizi zinaonesha kutokuwepo uthibitisho wa kuwepo idadi kubwa ya wananchi

wasiokuwa na vyeti vya kuzaliwa, ingawa ni kweli kwamba kuna asilimia fulani ya wananchi wenye umri wa miaka 40 kwenda mbele ambao vizazi vyao havijasajiliwa.

Mhe. Naibu Spika, kuwepo kwa idadi hii ya watu wasiokuwa na vyeti vya kuzaliwa inaweza kuwa ni miongoni mwa sababu zinazopelekea Serikali kutokujua takwimu halisi ya watu wake. Hata hivyo Serikali katika kufahamu idadi ya watu haitegemei njia ya usajili wa vizazi pekee, bali ni njia kuu inayotumika ni kufanya zoezi maalum la Sensa ya Watu na Makaazi na zoezi hilo hufanyika kila baada ya miaka kumi (10).

(b) Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na mpango wa Serikali katika kuwapatia vyeti vya kuzaliwa wananchi wake ambao hawana vyeti hivyo, utaratibu uliopo kisheria ni wa *late registration*, yaani usajili uliochelewa. Kwa mujibu wa utaratibu huu muombaji hutakiwa kujaza fomu maalum inayoambatana na kiapo na mdhamini ambayo pia hutakiwa kupitia kwa Sheha wa Shehia aliyozaliwa muombaji pamoja na Mkuu wa Wilaya na hatimae kusajiliwa na kupatiwa cheti cha kuzaliwa baada ya kulipa ada iliyowekwa.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba wasaidie katika kuwaelimisha wananchi na kuwashajihisha kuweza kujitokeza kwa wale ambao wasiokuwa na vyeti vya kuzaliwa kufika katika Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo ili kuweza kusajiliwa na kupatiwa vyeti hivyo.

Mhe. Omar Said Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa ruhusa yako nimuulize swali la nyongeza lenye vifungu lenye (a) na (b)

(a) Mhe. Naibu Spika, mimi nashukuru kwamba Naibu Waziri amekiri katika swali lake jibu lake mama kwamba wapo baadhi ya Wazanzibari wenye umri wa miaka 40 ambao hawana vyeti vya kuzaliwa, lakini pia kwa kuwa vyeti vya kuzaliwa havitumiki kwa kazi hiyo tu ya kutambua idadi ya watu kama alivyosema kwenye jibu lake mama vinatumika kwa kazi mbali mbali kama kuombea paspoti au kupata vyeti vya Uzanzibari na mambo mengine kadha wa kadha.

Hata yeye mwenyewe atakapokwenda kuomba hiyo paspoti atatakiwa apeleke cheti cha kuzaliwa cha baba yake ambaye pengine ana umri zaidi ya miaka 60, na kwenye hiyo *late registration* anayosema kuna sharti lazma apeleke mtu anayemtangulia kwa miaka 10 jambo ambalo ni gumu kwetu sisi. Je, huoni

kwamba watu wenye umri huo wenye miaka 40 kukosa hivyo vyeti vya kuzaliwa ni tatizo ambalo pia linaweza kuathiri watoto wao.

(b) Kwa kuwa katika hati ya kiapo kama nilivyosema kina masharti hayo ya kupatikana mtu aliyezidi umri wa miaka 10 kwa yule anayepewa. Je, Serikali haioni kwamba kuweka sharti hilo lazima apatikane mtu wa miaka 10 ni moja kati ya sababu ya kuwakosesha vyeti hao watu wenye umri mkubwa. Ahsante sana Mhe.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ : Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza ambalo ni (a) na (b) lakini nimwambie Mhe. Mwakilishi katika majibu yangu ambayo nilivyokutangulia.

Swali la kuwepo na ugumu katika kufuata utaratibu, sheria au kanuni ambazo ziliopo sasa hivi kwamba kuwepo na mdhamini ambaye ana umri wa miaka 10. Nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba hilo si tatizo ugumu wa hata kama utakuwepo lakini haya ni matakwa ya Kisheria ambayo hatuwezi kuyafanya vyenginevyo kinyume na utaratibu na sheria ambao uliidhinishwa pia kupitia Baraza letu Tukufu.

Kwa hiyo naomba Mhe. Mwakilishi aendelee kuhamasisha wananchi wetu kwamba kujua kila jambo lina changamoto zake na hili Serikali imelifanya na sio kuwakomoa wananchi wetu na baada lake ni utaratibu wa kisheria ambao kwa sasa hivi ndio tunaoutumia. Kwa hivyo tuendelee tu kuhamasisha na kuweza kusaidia pale ambao panahitajika tuwasaidie ili waweze kufikia hatua waweze kupata hiyo huduma kwa mujibu wa utaratibu wa Kanuni na Sheria.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa hii kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kama tulivyomsikia kwenye majibu yake ya swali mama, alisema wazee hawa ni kuanzia miaka 40 na kuendelea wapo ambao hawana hizo targisi. Lakini kama kweli wazee hawa kuanzia miaka 40 mpaka 80 tunajua kwamba hawana hizo targisi lakini tukianagalia huu utaratibu unaotumika sasa hivi wa kwenda kufuata hizo targisi Wilayani, Mikoani mpaka kuipata ni *process* kubwa na refu ambayo inamuwezesha mama huyu au mtu mzima asipate ile fursa ya kupata kile cheti cha kuzaliwa.

Je, Serikali imeandaa mpango gani wa kuweza kuzifanya hizi *process* kuwa ni rahisi labda mwaka hadi mwaka kufika kwenye vituo vya karibu na hawa wazee ili waweze kupata huduma hii kwa urahisi na afadhali zaidi. Ahsante *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kupitia Mkoa wa Kaskazini Unguja Vijana, Mhe. Hidaya Ali Makame kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba jambo lolote lile limeanzishwa ambalo linafuata utaratibu wa kisheria linakuwa na changamoto zake. Lakini pamoja na changamoto hizo kama ambavyo nimeweza kumjibu Mhe. Mwakilishi ambaye alitangulia sasa hivi Mheshimiwa hili jambo ni jambo la kisheria na kwa upande wa Wizara kwa sasa hivi bado utaratibu wetu *process* ambazo tunazipita ni kuanzia kama nilivyoweza kutangulia kwa Shehia baada Wilayani. Lakini naomba kwa sasa hivi kutokana na hali halisi tuliyonayo tuendelee kutumia katika ngazi hizo ambazo tumezitaja na pale ambapo tutaona kwamba kunahitajika, basi Baraza lako tukufu litafanya mabadiliko mengine, basi nadhani tunaweza tukafanya hivyo ambavyo tunaona. Lakini nahisi kwa Wizara hili naona sio tatizo kubwa sana ambalo linaweza likatufanya tuweze kuendelea kutokuhamasisha wananchi wetu, kusaidia katika kupunguza ugumu ili wazee wetu waweze kupata vyeti.

Naomba nimuombe sana kwa hilo na panapomajaaliwa tutaangalia utaratibu ambao unaweza kuwa muafaka zaidi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naamimi kuniona ningependa nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa visiwa vyetu na wananchi wetu wamekuwa wanazunguka na kuishi katika pande zote mbili za Muungano ikiwa ni haki yao ya Kikatiba. Lakini pia kutokana na muingiliano huu watoto wetu wanazaliwa upande wa pili wa muungano ikiwa baba ni Mzanzibari na mama anatoka upande wa pili wa Tanzania Bara.

Je, serikali imejipangaje na ina utaratibu gani unaotumika kuhakikisha kwamba haki za mtoto anayezaliwa kwa upande wa pili wa muungano unaweza kulindwa wakati wa uthibitisho wa cheti cha kuzaliwa na upande wa Tanzania Bara.
Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa kuzilinda haki za vizazi au wananchi ambao wamekuwa wapo katika upande wa pili wa muungano naomba Mhe. Mwakilishi afahamu kwamba suala la usajili wa vizazi na vifo hili si jambo la muungano, na kwa vile kama sio jambo la muungano ni kwamba sisi tuna msajili yule ambaye amefika katika maeneo yetu au katika taasisi zetu na ambaye kwa kweli amekwenda kupata zile huduma.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu masuala mengine ya kuangalia ni jinsi gani ambavyo tunaweza kuangalia au kulinda hizo haki nyengine ambazo anastahiki. Hilo ni jambo ambalo linahitaji kuliangalia zaidi kwa umakini na pale ambapo itaonekana kwamba kuna haja ya kufanya hivyo naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi wizara haitosita kufanya hivyo.

Nam. 48

Sheria Kuandikwa kwa Lugha ya Kiingereza.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Aliuliza:

Mhe. Naibu Spika, wananchi wote wanawajibu wa kutii Sheria na si busara kwa wananchi kuvunja Sheria. Hata hivyo, uvunjifu wa sheria unatokana na wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya sheria za hapa nchini kutokana na sheria hizo kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Je, Mhe. Waziri huoni Sheria zetu kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza kunapelekea wananchi hao kushindwa kuzielewa na kupelekea wavunje Sheria hizo na kushindwa kudai pale wanapokoseshwa haki zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 48 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba wananchi wote wana wajibu wa kutii sheria za nchi na kuepuka uvunjifu wa sheria hizo.

Hata hivyo uvunjifu wa sheria hautokani na sababu ya sheria hizo kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza bali unatokana na tabia na hulka iliyojengeka miongoni mwa jamii yetu. Serikali kwa upande wake imeweka utaratibu wa kuzifanyia tafsiri kwa lugha ya Kiswahili sheria hizo ili kuongeza uelewa wa wananchi juu ya sheria hizo na kuongeza utii wa sheria bila ya shuruti. Pamoja na jitihada hizo, bado jamii yetu inakabiliwa na matendo ya uvunjifu wa sheria.

Naomba nichukue fursa hii, kutoa wito kwa jamii kuendelea kuzitii sheria zetu na kuepuka uvunjifu wa sheria hizo ili jamii yetu iendelee kuishi kwa amani na utulivu kwa faida yetu na vizazi vyetu.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na kuwa na umuhimu mkubwa wa uwelewa wa sheria kwa wananchi je, serikali ni lini sheria zetu zitatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha mama ili wananchi wawe na uwelewa mpana wa sheria**.**

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu mama kwamba serikali imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba zile sheria ambazo zipo katika lugha ya Kiingereza zinatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba hapo zamani palikuwa hakuna utaratibu wa kupelekwa sheria mbili, kwa maana ya Kiingereza na ya Kiswahili kwa Mhe. Rais, kwa maana kwamba Miswada ambayo ilikuwa ikitoka katika Baraza la Wawakilishi na kupelekwa kwa Mhe. Rais huwa inapelekwa ile ya Kiingereza na ile ndiyo ambayo anayoitia saini.

Lakini nikujulishe kwamba utaratibu ambao tunao siku hizi baada ya Miswada kutoka Baraza la Wawakilishi kufanyiwa marekebisho ya mapendekezo ambayo yamependekezwa na kufanyiwa marekebisho basi Miswada hiyo huwa inapelekwa kwa Mhe. Rais ikiwa ni miwili mmoja kwa lugha ya Kiingereza na mmoja kwa lugha ya Kiswahili.

Mhe. Suleiman Ali Suleiman: Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea na shughuli zetu kama zilivyopangwa na Mwenyezi Mungu atupe uwezo wa kuhakikisha tunamaliza salama.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo. Kwa bahati nzuri Tanzania ni miongoni katika nchi ambazo zinahakikisha kwamba inatumia lugha ya taifa ya Kiswahili na hata Rais wetu wa Muungano anapokwenda popote akikutana na mgeni yeyote yeye hutumia lugha yetu ya Taifa ya Kiswahili.

Je, kwa kuwa suala hili ambalo ni muhimu kwa wananchi wetu asilimia 80 ambao hawajui Kiingereza naweza kusema hivyo na naamini ndivyo ilivyo. Ni lini Wizara hii itahakikisha inaweka wakalimani wa Kiswahili katika Mahakama zetu ili inapotokea haja ya kufanya hivyo kuweza kuwanusuru wananchi wetu wasiingie katika majanga ya hukumu ambazo hawazielewi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba sheria zetu sio zote ambazo zimetafsiriwa. Kama nilivyoeleza kwamba serikali inafanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba zile sheria ambazo hazijatafsiriwa basi zinatafsiriwa. Sambamba na hilo utaratibu ambao uliokuwa ukifanyika mwanzo Miswada hupelekwa kwa Mhe. Rais kwa lugha ya Kiingereza basi hivi sasa inapelekwa kwa lugha zote mbili Kiswahili na Kiingereza ili kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili nayo tunaipa nafasi yake.

Mhe. Naibu Spika, nimwambie tu Mhe. Mwakilishi basi wazo lake tunalichukua na pale ambapo tunahisi ipo haja ya kufanya hivyo basi tutafanya hivyo ili kuwasaidia wananchi wetu kupata haki zao hapo Mahakamani.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Pia nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Mahakama ni pahali ambapo kila mmoja anakimbilia kupata haki yake naweza kusema kwa asilimia 90 mpaka 95, sehemu ambayo wananchi wake wote wanazungumza Kiswahili na kufahamu Kiswahili. Mahakama ile inawezekana hapo awali Majaji wa wakati huo walikuwa ni

Wazungu au Wahindi ndio maana sheria zao zilitungwa kwa Kiingereza lakini kwa sasa hivi Majaji wetu wote ni wananchi wa Zanzibar au ni Watanzania.

a) Mhe. Naibu Spika, kwa nini mpaka leo wakitoa hukumu au katika maelekezo yoyote wanatoa kwa lugha ya Kiingereza, hukumu ile kwa nini isitoke kwa lugha ya Kiswahili

b) Kama lugha yetu ya Kiswahili ni lugha ya taifa, wanafunzi wetu wengi wanaweza kuwa na akili nzuri ya kujibu maswali lakini kinachowahangaisha ni lugha. Kwa nini katika masomo mengine ambayo ukiachia somo la Kiingereza hawawezi kutungiwa mitihani kwa lugha ya Kiswahili.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa swali ulilioliuliza sio swali la msingi, kwa hivyo kama Mhe. Waziri atataka kujibu lile la kwanza, lakini la pili halikuwa ni swali la msingi la kuweza kujibiwa.

Mhe. Waziri unayo nafasi ya kuliwacha au kulijibu kama una uwezo nalo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ningelipenda Mhe. Suleiman Sarahan akalirejea swali lake nambari moja ambalo linalonihusu mimi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa rudia swali lako.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, namuuliza kwamba kwa utaratibu Mahakama ni pahala ambapo wananchi wote wa Zanzibar tunakimbilia kwa kwenda kupata haki yetu. Lakini kwa utaratibu wa kizamani mpaka ilivyofikia sasa hivi inaonekana kwamba Majaji wetu wa mwanzo walikuwa ni Wazungu au Wahindi, lakini sasa hivi takriban asilimia 100 Majaji wetu ni Watanzania wanajua kusema Kiswahili cha kutosha. Lakini mpaka leo hukumu zinazotoka pale wakati mtu anakwenda kutafuta haki yake zinatoka kwa lugha ya Kiingereza.

Je, ni kwa nini hivi sasa hazitoki kwa lugha ya Kiswahili ili mtu kujua kosa lake na tatizo lake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, panapotolewa hukumu Mahakamani ni kwamba hukumu zile sio kwamba zote zinatolewa kwa lugha ya Kiingereza, ukenda Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya unazikuta hukumu hizo zinatolewa kwa Kiswahili. Inawezekana hukumu hizo zikatolewa kwa lugha ya Kiingereza mara nyingi katika Mahakama zile za Rufaa.

Katika Mahakama zetu hizi za Mwanzo basi hukumu hizo unazikuta pia zinatolewa kwa lugha ya Kiswahili na sio lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo hukumu zile zinapotolewa wananchi wetu kwa sababu ni Waswahili wanaelewa kile ambacho kinachowafanya watoke katika hatia au waingie katika hatia.

Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Suleiman Sarahan, Mahakama zetu hususan hizi za chini wanatoa hukumu kwa lugha ya Kiswahili. Ahsante.

Nam. 2

Taratibu za Uwekezaji

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni miongoni mwa nchi yenye maeneo mengi ya uwekezaji lakini asilimia kubwa ya uwekezaji huo unaonekana kukiuka taratibu zilizopo kisheria.

(a) Je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kuwa taratibu zote za uwekezaji zinafuatwa.

(b) Migogoro katika maeneo ya uwekezaji inazidi kuongezeka siku hadi siku. Je, ni Wizara au Taasisi gani ina dhamana ya usimamizi wa utoaji wa vibali vya uwekezaji hapa Zanzibar na ni kwa nini migogoro hiyo inaongezeka.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi swalii lake namba 2 lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, sote tunakubaliana na Mheshimiwa kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizobarikiwa fursa nyingi za uwekezaji katika maeneo tofauti yakiwemo ya kilimo, utalii, viwanda, huduma za usafiri na usafirishaji, uvuvi na nyengine nyingi.

Kuhusu uwekezaji ni muhimu kuelewa kwamba masharti ya uwekezaji yanategemea aina ya uwekezaji wenyewe na kwa kiasi kikubwa mahali unapokusudiwa kuwekezwa. Kwa mfano, uwekezaji wa kiwanda karibu na makaazi ya watu au uwekezaji mkubwa ndani ya eneo la urithi wa Kimataifa wa Mji Mkongwe utahitaji kutimiza matakwa tofauti na uwekezaji wa kawaida wa hoteli nje ya Mji Mkongwe.

Kuhusiana na masuala yake (a) na (b), naomba kujibu kama ifuatavyo:

a) Wizara, kupitia Mamlaka ya Uwekezaji *ZIPA* imekuwa ikisisitiza juu ya kufuatwa kikamilifu utaratibu mzima wa kisheria kuhusu uwekezji nchini. Kwa kuzingatia haja ya kuweka bayana utaratibu huo, hivi karibuni *ZIPA* imefanya mapitio ya Muongozo wa Uwekezaji *(Investment Guideline)* na kuandaa na kutoa Muongozo mpya. Taarifa pia zinapatikana katika tovuti ya *ZIPA*. Wizara pia imekuwa ikiimarisha mashirikiano na Taasisi nyengine kama vile Mamlaka ya Mazingira, Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na Bodi ya Mapato (*ZRB*) ili kurahisisha na kufanikisha uwekezaji nchini.

b) Kama nilivyoeleza awali, Taasisi kuu inayohusika na uwekezaji ni Mamlaka ya Uwekezaji (*ZIPA*). Hata hivyo, taasisi nyengine kadhaa zinaweza kuhusika na mchakato wa uwekezaji kwa kutegemea aina ya uwekezji huo kama nilivyosema awali. Kuhusu migogoro katika maeneo ya uwekezaji, hatuna takwimu zinazoonesha kuwa migogoro hiyo inaongezeka. Hata hivyo, ni kweli ipo na aghalabu inatokana na kutofuatwa kwa utaratibu, udanganyifu kwa wenye maeneo ya ardhi, kujitokezi madalali wa kusaidia uwekezaji ambao wakati mwengine huwashauri vibaya wawekezaji hao.

Mhe. Naibu Spika, *ZIPA* itaendelea kutoa elimu kwa wawekezaji na wananchi ili kuepusha uwezekano wa kutokea migogoro.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, wewe ndio msimamizi mkuu wa Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar, unahakikisha vipi kuwa mamlaka yako inafanya kazi kwa mashirikiano mazuri na Kamisheni ya Ardhi.

b) Je, *ZIPA* ina nafasi gani kwa mujibu wa sheria juu ya suala zima na uidhinishaji na utoaji umiliki wa ardhi kwa uwekezaji.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu mama kwamba *ZIPA* katika kufanikisha majukumu yake ni lazima ishirikiane na taasisi mbali mbali ikiwemo Wizara ya Ardhi na hasa taasisi inayohusika na masuala ya Ardhi. Mwekezaji anapowekeza ni lazima kwanza anapeleka maombi yake *ZIPA* na baada ya kupatiwa hati ya uwekezaji *ZIPA* inakuwa inawasiliana na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kupatiwa ardhi mwekezaji huyo. Iwapo mwekezaji anakuwa tayari ameshaainisha ardhi yake *ZIPA* inashirikiana na Ardhi kuona kwamba mwekezaji huyo anapatiwa hati ya umiliki wa ardhi kwa ya kuitumia ardhi hiyo. Kwa hivyo mashirikiano hayo yapo kwa sababu bila ya mashirikiano hayo uwekezaji huo hautoweza kukamilika.

b) Mhe. Naibu Spika, pamoja na hilo *ZIPA* inashirikiana na wengine wote kwa mfano *immigration* inashirikiana pia na Mamlaka za Utoaji wa leseni lakini vile vile inashirikiana na Bodi ya Mapato katika masuala yote na katika kuhakikisha kwamba ushirikiano huo unafanikiwa zaidi. Hivi sasa Serikali imo katika hatua ya kuhakikisha tunakamilisha *process* ya kuwa na kituo kimoja cha uwekezaji kwa maana ya *One Stop Centre* na kwa maana taasisi hizi zote zitakuwa chini ya usimamizi wa *ZIPA* yenyewe baada ya mchakato huo kukamilika.

Mhe. Naibu Spika: Suala la pili la nyongeza Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, jembe letu nakushukuru sana kwa kunipa nafasi mimi nitaomba kumuuliza suala la ziada lenye (a) na (b) Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

a) Kwa kuwa maeneo ya *free zone* hasa ya Fumba yametolewa kwa ajili ya wawekezaji *serious* kama kina Bakhresa na wengine lakini matokeo yake maeneo yale wamepata baadhi ya watu au wamepewa watu ambao sio *Serious Investors* na wamepeana kienyeji enyeji watu wamekwenda kupewa tu lakini mpaka hadi hivi sasa hakujafanyika *any investment.* Sasa ni taratibu gani ambazo mtachukua kuhakikisha kwamba wale wote waliochukua yale maeneo waliohodhi ambayo sio *Serious Investors* mtayachukua mtayarudisha.

b) Ni maeneo mangapi hadi hivi sasa kwenye *free zone* mshayatoa kwa ma-*investors* na mangapi yamebakia matupu kwa muda huo. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango majibu

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Nadir swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba Serikali imeweka eneo la Fumba kama ni eneo maalumu la uwekezaji (*Free Economic Zone)* pamoja na maeneo mengine na uko utaratibu unaotumika kwa ajili ya wawekezaji katika eneo hilo na akifuatilia *Investment Guideline* ambayo nimeisema hapa ambayo imetolewa hivi karibuni mwaka 2017, ataona muongozi mzima unaotumika wa kufuata kwa ajili ya wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika maeneo haya ya *Free Economic Zone*.

b) Mhe. Naibu Spika, hadi sasa sina taarifa ya kwamba kuna mwekezaji ambaye sio *serious* ambaye kapewa eneo hilo au kapewa eneo katika eneo la *Free Economic Zone* la pale Fumba.

Namuomba Mhe. Nadir tuwasiliane anipe taarifa hizo kwamba hawa sio *Serious Investors* lakini hadi sasa tunajua wawekezaji waliopo pale ni *Serious* na wana muda wao ambao umekubalika kwa mujibu wa Hati ya Uwekezaji waliopewa na *ZIPA*, lakini hili la takwimu nitaomba nimpatie baada kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika: Suala la mwisho la nyongeza Mhe. Zulfa Mmaka Omar.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya suala la nyongeza.
Mhe. Waziri katika maeneo ya uwekezaji kuna eneo moja kuna mwekezaji wa Mpapindi ambaye kapewa Hati ya Uwekezaji lakini mpaka leo hakuna shughuli yoyote inayoendelea katika eneo lile, suala langu lina kitoto (a) na (b).

a) Je, ni kiasi gani cha fedha ambazo Serikali inaidai katika mwekezaji yule katika hati yake ile ambayo amepewa ya uwekezaji.

b) Nini hatma ya mwekezaji yule ya kufuta *lease* hiyo au hati yake ili aweze kupatiwa mwekezaji mwengine katika eneo lile na Serikali kupata mapato yake ya nchi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango majibu

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Zulfa Mmaka Omar swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba zipo changamoto zinazokabili uwekezaji wa mradi huu wa Mpapindi na sisi suala hili tunalielewa lakini Wizara ya Fedha na Mipango inashirikiana kwa karibu sana na Wizara inayoshughulikia masuala ya ardhi na tumeunda kamati yetu na hivi karibuni tulikuwa Pemba kufuatilia suala hilo. Kwa hivyo hili suala nimuombe Mhe. Zulfa atustahamilie wakati tunalifanyia kazi na tutampatia taarifa mara baada ya mchakato wetu huo kukamilika.

b) Mhe. Naibu Spika, lakini ni hasara gani iliyopatikana hadi sasa nalo pia tutampatia kwa maana ya ile hati kwa sababu mradi bado haujaanza. Sasa kama kodi ya ardhi kwa maana ya ile *lease,* sasa *lease fee* yake hiyo nitampatia pia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Suala la Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kunijibu swali langu namba 18 lakini naomba lifanyiwe marekebisho kidogo kifungu (b) kama dawa hiyo yenye ujazo wa lita 8,000 sio lita 8.

Mhe. Naibu Spika: Sawa marekebisho yamefanyika Mhe. Waziri

Nam. 18

Matokeo ya Uchunguzi wa Dawa za Kuulia Magugu

Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud - Aliuliza:-

Tarehe 16 Februari, 2017 wakati Mhe. Waziri akijibu swali namba 11 kuhusu wakulima kuuziwa dawa ya magugu ambayo imepitwa na muda aliliambia Baraza hili Tukufu kwamba dawa hizo za magugu zimepelekwa *TPRI*, Arusha *(Tropical Pesticide Research Institute)* kwa uchunguzi zaidi baada ya ule walioufanya Wizara ya Kilimo hapa Zanzibar.

a) Je, nini jawabu ya utafiti huo wa Arusha.

b) Kama dawa hiyo yenye ujazo wa lita 8 imebainika kuwa ni mbovu, huoni ipo haja ya alieshinda tenda arudishe hiyo dawa ilikotoka kwa gharama zake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi) – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud wa Jimbo la Bububu swali lake nambari 18 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Ni kweli Wizara ilichukua hatua za kupeleka sampuli tatu za dawa hiyo ya kuulia magugu *TPRI*- Arusha *(Tropical Pesticide Research Institute)* kwa uchunguzi zaidi baada ya ule uliofanywa na Wizara ya Kilimo hapa Zanzibar.

Matokeo ya uchunguzi wa kimaabara ya *TPRI* - Arusha yamebainisha kuwa sampuli zote tatu hazikidhi viwango kutokana na kutokuwa na viambato ambavyo ndivyo vyenye kuleta athari ya kuuwa magugu yenye majani mapana na majani membamba.

TPRI walishauri kutokuitumia dawa hiyo kwa madhumuni ya kuulia magugu.

b) Mhe. Naibu Spika, Wizara iko katika taratibu za kumjulisha aliyeshinda tenda hiyo ili aweze kuihamisha dawa hiyo kwa gharama zake na baadaye taratibu nyengine za kisheria zitafuata.

Mhe. Naibu Spika: Tunaendelea naona Mheshimiwa mwenyewe Masoud

Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa jawabu hii inathibitisha wazi kwamba dawa hizi ziliingizwa nchini na Wizara kupitia aliyeshinda tenda hiyo kuwa ni mbovu na kuwapa hasara kubwa wakulima.

a) Huoni kwamba aliyepewa tenda na wizara kuruhusu kuingiza nchini dawa mbovu ni uzembe wa wizara na ipo haja ya kuwajibishwa aliyefanya kosa hilo. *(Makofi)*

b) Nini thamani ya dawa ambazo wakulima tayari walishauziwa na hii thamani ya lita 8,000 ambazo sasa hivi ziko ghalani thamani yake ni kiasi gani.

c) Na ni lini wakulima watarejeshewa fedha zao ambazo walinunulia dawa hiyo mbovu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la nyongeza lenye (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kosa limetendeka na kwa kuwa sheria zipo za wanaofanya makosa taratibu zipo hivyo Serikali itachukua hatua za kisheria kila aliyefanya kosa awajibike kwa mujibu wa sheria. *(Makofi).*

b) Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la thamani kwa kuwa taarifa hizi nimezipata hivi asubuhi naomba sana Mhe. Mwakilishi atupe muda tuwasiliane na Wizara husika ili tuwasilishe thamani na gharama kwa maandishi kwake na kwenye Baraza lako tukufu. *(Makofi)*

c) Mhe. Naibu Spika, tutahakikisha kwamba fedha za wakulima ambazo zimetumika katika kununua dawa hizi itabidi tuchukue kila hatua wakulima hao waweze kurejeshewa fedha zao kwa mujibu.

Mhe. Naibu Spika: Suala la nyongeza Mhe. Miraji Khamis Mussa

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii hapa lakini nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri kuhusu dawa hii inayohusu wakulima.

a) Kwa kuwa Mhe. Waziri wakulima wetu bado wanaendelea na shughuli hizi za kilimo na wanahitaji dawa je, ni hatua gani ya wizara iliyoichukua mpaka sasa kutambua dawa muafaka kwa wakulima wetu ili wasije wakapata matatizo kama haya yaliyoweza kutokea.

b) Kama utaratibu umeshafanyika dawa hiyo yaani ni dawa gani imepatikana kwa sasa hivi wakulima watusikie waweze kwenda kuichukua kwa matumizi bora ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Miraji lenye (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, tayari Wizara ya Kilimo imechukua hatua ya kutoa lita 659 za dawa mpya ya *bansul* ambayo inafaa kutumika badala ya ile dawa ya *hansul.*

b) Kwa msingi huo wizara itaendelea kuchukua hatua kuhakikisha wananchi wanapata hii dawa ambayo inafaa ili taratibu nyengine ziendelee na wakulima waendelee na shughuli zao kama kawaida.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hassan Khamis Hafidh swali la mwisho la nyongeza.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kwa kuniona.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri Mohamed Aboud muungwana kwa kujibu swali na kukiri kwamba kweli Wizara ya Kilimo imefanya kosa la kununua dawa mbovu.

Mhe. Naibu Spika, ni matumaini yangu hii dawa kwamba ilikuwa ni tenda na hiyo kampuni ilishinda tenda ikalipwa ili ikaweza kuleta dawa. Suala langu liko hapa sasa je, kama kampuni ishalipwa na imetupa dawa mbovu, pesa zetu tutazipata lini tulizowalipa, kama walilipwa kiasi gani walilipwa na kama dawa mbovu washaturudishia pesa zetu na kama hawajaturejeshea lini wataturejeshea pesa zetu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hassan kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali kwamba kwa kuwa taarifa za suala hili nimezipata hivi asubuhi kuweza kupata thamani halisi ya fedha zilizonunuliwa dawa hizo, lakini kama nilivyoahidi Baraza lako Tukufu tutaleta thamani hiyo kwa maandishi katika Baraza hili.

Kuhusu fedha zitarudishwa lini napenda nimuhakimkishie Mhe. Mwakilishi kwamba taratibu za kisheria zitachukua mkondo wake na wahusika pamoja na waliopewa tenda hii watawajibika kurudisha fedha kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika: Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi kwa heshima kubwa naiomba Serikali inipatie jawabu la msingi kwa swali langu namba 8 kwa faida ya vijana wa Zanzibar. Ahsante

Nam. 8

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Aliuliza**:-**

Kuna vijana wengi ambao wana vipaji tofauti hasa katika michezo na kama wataendelezwa itakuwa vyema hata kuwasaidia kupata ajira.

Je, Serikali imejipanga vipi kuwaekea vijana mkakati wa kuweza kuendeleza vipaji vyao.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Mhe. Waziri nikikwita hapa maana yake uje ujibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu**:-**

Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, naomba kumjibu Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma Nafasi za Wanawake kupitia Vijana Mkoa wa Kusini Unguja swali lake namba 8 kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa kuna vijana wengi ambao wana vipaji tofauti hasa katika mchezo wa mipira wa miguu na kama wataendelezwa vyema wataweza kupatiwa ajira.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) tayari imeanza maandalizi ya kuhakikisha vipaji vya wachezaji vijana vinaibuliwa na kuendelezwa.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa mikakati hiyo ambayo inakwenda sambamba na maelekezo ya Shirika la Soka la Afrika (*CAF*) kuhakikisha kwamba timu zote za Daraja la *Premier* zinakuwa na timu ndogo za vijana. Pia Wizara itashajihisha taasisi mbali mbali kuanzisha *Academy* ambazo zitahusisha vijana katika kuendeleza michezo ukiwemo mchezo wa mpira wa miguu.

Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma swali la kwanza la nyongeza

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri ya kutia moyo lakini napenda kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Vipaji hakuna kimoja, vipaji viko vingi ikiwa vijana wa sarakasi, wakiwepo vijana wachezaji wa mipira lakini vipaji vingi vizuri ambavyo vinatuzunguka katika maeneo yetu lakini hatujui namna gani ya kuweza kuwasaidia vijana wenzetu. Je, Mhe. Waziri ni njia gani unazotumia ili kuweza kuwafikia na kuwasaidia vijana hawa hususan vijijini kuweza kufikia malengo yao.

Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo napenda kumjibu Mhe. Salha Mwinjuma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, nakiri kwamba kuna vipaji tofauti kama alivyovieleza Mhe. Salha na napenda kumjibu kwamba njia ambazo tutazitumia kwa kuwatafuta hawa vijana na kuibua vipaji hivi kuna njia mbali mbali ambayo njia hii tutatumia kwa njia ya ligi ambazo ligi hizi zitawakusanya vijana kupitia vijijini hadi kufikia hatua ya fainali. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Dk. Mwinyihaji swali la pili la nyongeza.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, kabla sijauliza swali langu naomba kwa kweli nishukuru sana wizara hii kwa masuala tunayouliza na majibu anayoyatoa na hatua wanazozichukua na mfano wa hai Mheshimiwa ni masuala ya Uwanja wa Amani. Leo *score board* linawaka, mageti yanafunguliwa, gari zinaingia na kutoka vizuri na hilo Mhe. Naibu Spika, tunaomba na Wizara nyengine hivyo hivyo wakijibu masuala na hatua zifuatwe. Swali langu Mheshimiwa la nyongeza kama ifuatavyo.

Pale Dole pana kiwanja chetu cha *Sport Academy* cha kuendeleza vipaji cha *Olympic.* Je, Wizara inakiendeleza vipi kiwanja kile ambacho sasa hivi kinaota magugu tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba tuna viwanja mbali mbali ndani ya Zanzibar. Napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba kwa jitihada ya wizara na serikali kwa jumla kuna jitihada nyingi ambazo tumezichukua kuviendeleza viwanja vile na sasa hivi tunajenga viwanja kila Wilaya kwa ajili ya michezo. Kwa hivyo tunamuhakikishia kwamba kiwanja hiki tutaendelea kukisimamia na kukishughulikia tuone kinafanya kazi kama zamani na vijana waweze kukitumia kwa ajili ya michezo.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza kwa Wizara hii ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Kwanza kabla sijauliza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya maswali mama na maswali ya nyongeza. Lakini nichukue fursa hii kuweza kuipongeza sana *ZBC* kwa kuweza kuandaa Kombe la Mashindano ya Vijana wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, mashindano yale yaliibua vipaji katika mchezo wa *football*, vipaji vingi sana Unguja na Pemba.

a) Kwa hivyo nimuulize Mhe. Waziri baada ya kuibuka au kuviona vipaji vile, vijana wale hivi sasa wanaendelezwa vipi.

b) Kuna michezo mbali mbali je, ni lini Wizara yako Michezo hiyo kama *basketball, volleyball* na riadha, ni lini Wizara yako itaweza kuandaa mashindano kama yale ya vijana kuweza kuibua vipaji katika fani nyengine. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi napenda nipokee pongezi ambazo tumezifanya na juhudi kubwa za Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ambazo tumeonesha juhudi nzuri kupitia vijana wetu. Mhe. Naibu Spika, napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba vijana hawa bado tunao na vipaji hivi tutaendelea kuviendeleza ili ukifika mwaka mwengine tutaendeleza kuwa na ligi hizi. Kwa mpango ambao nimejibu katika swali mama kwamba *CAF* wametutaka tuwe na *league* za *premier* kwa timu zetu ili kukuza vipaji wakiondoka hawa wazee kuwe na vijana kwa ajili ya kuendeleza timu zetu za taifa. Kwa hivyo nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba bado tuna imani na tuna jitihada tutaviendeleza vipaji hivi vya vijana wetu.

b) Mhe. Naibu Spika, napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba katika vipaji vyengine kwa watoto wetu ambapo kuna michezo tofauti, jitihada ambayo imechukua wizara na ametaka kujua lini vipaji hivi vitaendelezwa au tutavitafuta kuona vijana wanavifanyia kazi. Mimi nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi sasa hivi tuna mpango kama atakuwa anaangalia *ZBC* tunawaita watoto pale, kuna watu wa rika mbali mbali wanaonesha vipaji vyao na hatimae tunafanya mashindano na watapatikana vijana hawa na kuonesha vipaji vyao. Ahsante sana.

Nam. 5

Eneo la Kituo cha Umeme Mtoni

Mhe. Said Omar Said – Aliuliza:-

Itakumbukwa kwamba mnamo miaka ya 1990 serikali kwa nia njema ilivunja nyumba katika eneo la kituo cha umeme mtoni kwa nia ya kuweka usalama wa eneo hilo.

(a) Je, serikali bado inania kuliweka eneo hilo kuwa eneo la wazi.
(b) Kama nia hiyo bado ipo kwa nini eneo hilo linaendelea kutumiwa kwa shughuli nyengine.
c) Kama nia hiyo haipo kwa nini serikali isirejeshe viwanja kwa wananchi waliovunjiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye vipengele (a), (b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo**:**

Mhe. Naibu Spika, madhumuni yaliyolengwa wakati wa uvunjaji wa nyumba katika eneo hilo la Mtoni bado yapo pale pale, hasa ikizingatiwa kuwa usalama wa Kituo cha Umeme kilichopo katika eneo hilo ni suala muhimu na linahitaji kupewa uzito unaofaa.

Hivyo, haitokuwa busara kwa eneo hilo kugawiwa viwanja vya kujenga nyumba za kuishi au kuendesha shughuli zozote za kijamii. Ahsante sana.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa lengo la serikali bado lipo pale pale la kuweka eneo hili kuwa ni eneo la wazi. Je, wale wanaolitumia sasa hivi eneo hilo wamelivamia au wamepewa kisheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, angetujuilisha tu labda walitumia vipi kwa sababu tumeweka eneo lile pale kwa matumizi ya shughuli za umeme, kama

linatumiwa kwa shughuli hizo maana yake ndio shughuli mahususi. Lakini kama kuna shughuli nyengine basi angetueleza kwa sababu tunakagua kila wakati na kuona hakuna shughuli nyengine zaidi ya hizo na zile za usafi ambazo zinaendelea pale. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuniona maana nishasimama muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha siku ya leo tukakutana hapa. Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha tumeona athari mbali mbali ambazo zinajitokeza, moja wapo ikiwa inaikumba Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, ni muda mrefu sasa kwa upande wa Kaskazini Pemba tunapata shida juu ya hali halisi ya masuala ya umeme, ikitokezea kuanguka kwa nguzo, ikitokezea hitilafu yoyote ya kiufundi tunashindwa jambo ambalo mpaka tupige simu Chake-Chake watu watoke huko na kipindi hiki cha mvua njia zimekatika na zina maji hazipitiki, ilimradi tatizo hilo linabakia. Je, ni lini sasa kwa upande wa Kaskazini Wilaya ya Micheweni tutapatiwa kituo kidogo pamoja na fundi wake ili tuweze kuondoa matatizo ambayo yanajitokeza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Tumesikia maoni na haja ya kuwepo kituo hicho niseme kwamba tutafanya namna ya kulitengeneza hili suala likawa sawa ili liweze kupunguza changamoto za wananchi wetu. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, serikali inapofanya kitu huangalia maana ya kufanya lile jambo lenyewe, hasa usalama wa lile eneo. Usalama wa eneo la umeme Mtoni lilitokea athari kubwa huko nyuma Mwenyezi Mungu atunusuru lisitokee tena ambalo lilileta adha kubwa katika nchi yetu. Lakini kwa kuwa serikali iliamua eneo lile kuliweka safi kabisa ili liondokane na yale mashaka ya kuwepo karibu watu wanaoishi eneo hilo, mheshimiwa hadi leo eneo hilo liko kimya. Je, serikali kupitia Shirika la Umeme imeweka alama maalum za kusema kwamba

eneo hili ni la Shirika la Umeme na kama limefanya hivyo kuna *beacon* yoyote inayoonesha kwamba eneo hili liko katika mikono yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Ni kwamba serikali kupitia Shirika la Umeme linaweka na kama utaangalia upande wa Mashariki kuna ukuta ambao *phase I* umemalizika tutaendelea na *phase II* baadae, tukiangalia upande wa Kaskazini kuna uzio na upande wa Kusini kuna *ZAWA*. Kiufupi lile eneo lote ambalo zilibomolewa zile nyumba lipo salama, linalindwa na lina vitambulisho kama utapita upande wa Mashariki kumeandikwa hasa. Sasa nadhani nimejibu swali lake. Ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

UTARATIBU

Mhe. Naibu Spika: Sasa mmesimama watu wawili, wacha nimpe mmoja halafu nitampa na mwengine. Sawa, Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nimesimama kwa kifungu cha 42 na kinasema kama ifuatavyo. "Baada ya muda wa maswali kuisha, Mjumbe yeyote anaweza kutoa hoja kuwa Baraza liahirishe shughuli zake zilizooneshwa katika Orodha ya Shughuli za Baraza, na lijadili jambo la dharura na muhimu kwa umma na kwa ruhusa ya Spika".

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nakuomba ruhusa yako kwa mujibu wa kifungu ambacho nimekitaja cha Kanuni za Baraza letu, Toleo la 2016 tuakhirishe shughuli zetu za Baraza kwa muda usiozidi saa moja na tujadili jambo la dharura lilojitokeza hapa visiwani kwetu. Mhe. Naibu Spika, jambo ambalo la dharura ninalokusudia kuliwasilisha mbele ya Baraza lako lijadiliwe na chombo hiki cha wananchi ni kuhusu maafa ambayo yamejitokeza ya mvua.

Maafa waliyopata wananchi wetu katika majimbo yote Zanzibar ni makubwa sana…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa sijakuruhusu, sijakuruhusu na nafikiri hiyo Kanuni ambayo umeitumia inasema kwamba kwa ruhusa ya Spika ndio inaruhusiwa kuanza kujadiliwa. Kwa hivyo, sijakuruhusu subiri nataka

nimsikilize Mhe. Abdalla Maulid Diwani na yeye kama ana hoja yake halafu zote pamoja tutazitolea maamuzi. Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, utaratibu wangu nimesimama kwa hoja ya 96, naomba kuisoma. Hoja ya 96 inasema, "Kabla ya Kamati ya Matumizi haijashughulika na fungu lolote la makadirio ya Matumizi, fungu hilo kwanza litapelekwa kwenye kamati inayohusika likifiriwe na halitaletwa kwenye Kamati ya Matumizi ya Baraza Zima mpaka Mwenyekiti wa Kamati iliyopewa kazi kulifikiria fungu hilo atakapomwarifu Spika kwamba Kamati yake imemaliza kufikiria fungu hilo".

Sasa tunapomaliza hapa tutakwenda kusoma bajeti ya Wizara ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini mpaka dakika hii yale matabu makubwa ambayo tulipaswa sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuwe nayo, mpaka dakika hii hatujayaona. Sasa hatujui tutakuja kufanya vipi hapo baadae ilikuwa tupate kidogo wakati inasomwa na sisi tuweze kupitia vifungu ili kuweka umakini kwa ajili kupitisha bajeti hii.

Mheshimiwa naomba sana katika hilo, ile taarifa haijasema siku gani au lini, lakini je tunataka tupate haki yetu ya msingi, tupate yale matabu mapema ili tuweze kuyapitia kuifanya kazi yetu kuwa nyepesi. Hoja yangu ilikuwa ni hiyo.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nahisi kwamba kwanza tukubaliane na hii hoja ya Mhe. Abdalla Maulid Diwani ambaye ametumia kifungu cha 96, lakini kwa tafsiri inayoonyesha katika kifungu hiki vitabu hivi vifike kwenye kamati, vijadiliwe kwenye kamati ndio tafsiri kubwa ya kifungu hiki. Haijazungumzia suala la kuletwa ndani ya Baraza la Wawakilishi, ni kamati ijadili ikisha Mwenyekiti ndio alete taarifa yake hapa kwa Baraza.

Kwa maana hiyo humu hakuna Kanuni au kifungu ambacho kinalazimisha lazima, ingawa ni busara sana kwamba vitabu hivi vifike wakati hotuba inatolewa. Sijui umenifamu vizuri, hakuna kifungu, kifungu hiki tafsiri yake Mheshimiwa ni nyengine kabisa eeh! umekitumia lakini tafsiri yake ni kwamba vifike katika kamati. Sasa ninachokisema mimi labda nitamuachia Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais atoe maelezo kidogo kuhusiana na hili, kwa sababu ni suala la serikali atatuambia kwamba wamefikia wapi, kwa nini vitabu hivi havijafika hapa ili tujue tunachukua hatua gani.

Lakini kuna suala zima la Kanuni ya 42 ambayo ameitumia Mhe. Mohammed Said Mohammed, mimi kwa mamlaka niliyonayo naomba sana hata kama tutatengua muda basi usizidi zaidi ya nusu saa. Kwa sababu kuna shughuli

nyingi tutamuachia Mhe. Mohammed Said Mohammed atatoa hiyo taarifa na baadae vile vile Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais itatoa taarifa ya shughuli gani ambayo wanafanya katika suala hili. Suala ambalo kwa kweli ni dharura na inabidi tulijadili. Lakini ningeomba sana tunatoa nafasi kwa watu watano tu hawatazidi kwa sababu sote tunalijua hili na baada ya hapo tutakubaliana na tutakutana tutalizungumza kwa upana mkubwa nje ya hapa ili tuone namna gani tutaweza serikali pamoja na sisi Wawakilishi tutaweza kulifanyia kazi.

Kwa hivyo kwanza ningesema zaidi kwamba tuanze na Mhe. Mohammed Said Mohammed halafu tutaendelea na masuala mengine yanayohusu vitabu. Mhe. Mohammed Said Mohammed, karibu.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa aina ya pekee kwa kuelewa juhudi za wananchi na kuelewa dharura ambayo imetufika.

Mhe. Naibu Spika, jambo ambalo nimekusudia kuliwasilisha mbele ya Baraza lako hili lijadiliwe na chombo hiki cha wananchi inahusu maafa yaliyotokana na mvua zetu.

Maafa waliopata wananchi wetu katika majibmbo yote ya Zanzibar ni makubwa sana na athari nyingi zimejitokeza katika maeneo hayo. Nyumba kadhaa zimeharibika kabisa za maeneo ya wananchi hao kutokana na maafa hayo. Aidha, nyumba na familia hazina sehemu ya kukaa pamoja na miundombinu na vivutio kadhaa katika maeneo ya barabara vimeharibika. Zanzibar kwa ujumla imepata athari kubwa na ni dhahiri maafa haya yatakapothaminiwa na kwa umakini mkubwa itaonekana namna ilivyoathiri maendeleo ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, lakini zaidi kwa muda mrefu ujao hii inatokana na kipato cha wananchi wetu walio katika kipato cha chini na cha kati wameathirika sana.

Baada ya kutoa maelezo haya Mhe. Naibu Spika, nataka niliombe Baraza lako tukufu liweze kujadili maafa haya kwa sababu ni sehemu nyingi sana, si Pemba peke yake, si Unguja peke yake, si Kaskazini, si Kusini yametokea maafa makubwa sana katika sehemu mbali mbali. Sasa baada ya kutoa maelezo haya.

Nataka niliombe Baraza lako tukufu lijadili kwa umakini wake na liyapitishe maazimio hayo. Nimetoa maazimio matatu ili kwa pamoja tuweze kuyapitisha.

1. Serikali itoe kauli ya hatua zilizochukua hadi sasa katika kukabiliana na tatizo hili la maafa.
2. Baraza liazimie namna ya kuwasaidia wananchi wote walioathirika na maafa haya
3. Sisi Wawakilishi wa wananchi tueleze mikakati ya kudumu kukabiliana na maafa kama haya badala ya kuiachia Idara ambayo inafanya zimamoto tu kila siku, kunapotokea maafa ndio tunakutana tunaweka Idara ya Maafa. Sasa niseme. Sasa niseme maoni haya matatu ili tuweze kuazimia Baraza lako Tukufu na nikaona upo umuhimu wa kuleta hoja hii wananchi hawa waweze kujadili kwa upana wake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo yangu machache naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wajumbe kama nilivyosema mwanzo kwamba ningeomba sana tuijadili hoja hii kwa Wajumbe watano ndio nitakaowapa ruhusa ya kujadili hoja hii na tutatumia si zaidi ya dakika 10 kila mmoja.

Kwa hivyo naomba sana watu wajipange wasirudie rudie masuala ambayo tayari yameshazungumzwa na wengine, lakini nimeshapata wachangiaji wanne, kwa hivyo nina nafasi moja na nitaanza kumpa nafasi Mhe. Hassan Khamis Hafidh (*Diaspora*) baadae atakuja Mhe. Simai Mohammed Said atafuata Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy. Mhe. Hassan Khamis Hafidh karibu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii asubuhi ya leo kuwa ni mchangiaji wa mwanzo katika maafa haya makubwa yaliyotukuta Zanzibar, yaliyosababishwa na mvua zilizoletwa na Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Welezo kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao, kwani Jimbo la Welezo ni miongoni mwa majimbo yaliyokumbwa na maafa haya.

Mhe. Naibu Spika, kama sikosei najua kuna Idara inayoshughulika na Maafa. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hoja hii ni hoja ya dharura sina sera inayoweza kueleza nini jukumu halisi la Idara ile ya Maafa. Aidha, isubiri maafa yatokee wayafanyie kazi au kujipanga katika kufanya maafa yasitokee ili tuweze kuishi nchi hii kwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, wahenga wamesema, "Kinga ni bora kuliko tiba". Kama sikosei Idara ya Maafa nahisi ipo katika kusubiri maafa yatokee ili iweze kuyafanyia kazi, imekuwa kama mchimba makaburi. Niliweza kusema katika hotuba yangu imekuwa kama mchimba makaburi kila siku anaomba watu wafe ili apate kazi ya kuchimba kaburi apate pesa. Sasa Mheshimiwa tukiangalia ukweli maafa ni makubwa, ni mengi na tunajua nchi hii masika yakija aliyoona hayati bibi yangu yakiongoka lazima yalete athari kubwa. Nitaomba kusema baadhi ya athari ambazo zimejitokeza na maafa haya, miongoni mwa waathirika ni Jimbo langu la Welezo.

Mhe. Naibu Spika, jimbo langu la Welezo na Wazanzibari wote kwa jumla baadhi ya maeneo leo hii hawana pa kukaa majumba yao yameingiliwa na maji.

Mhe. Naibu Spika, athari nyengine iliyojitokeza leo hii wanafunzi wa skuli nyingi Zanzibar hawendi skuli kwa sababu njia zimefungwa. Ukienda Kibonde Mzungu, Mwanakwerekwe Sokoni na maeneo mengi mengine njia zimefungwa pa kupita hakuna. Watu hawafiki majumbani kwao baadhi ya madaraja tayari yamekatika.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar asilimia kubwa ya wananchi tunaoishi ni watu wanyonge tunategemea kipato cha kila siku ili tuweze kuishi. Mheshimiwa maafa haya ya mvua yamesababisha biashara nyingi zifungwe na wafanyabiashara wale wanaopata pesa zile za kila siku, Wazungu wanaita '*daily bread, hand to mouth'*, leo hii wamekuwa omba omba kutokana na maafa haya ya mvua.

Mhe. Naibu Spika, miundombinu mingi ya barabara imevunjika, kwa kweli maafa ni makubwa. Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali iwape msaada wa makusudi wale wote wahanga waliokumbwa na maafa hayo.

Mhe. Naibu Spika, nilisema mwanzo kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Maafa haya ukifanya utafiti kwa Zanzibar mengi yametokea Wilaya ya Magharibi ambako jimbo langu la Welezo limo. Kwanza Mheshimiwa kuna vitu vinaniuma, tunajua inapokuja mvua za masika Magharibi itakuwa haipitiki, maradhi yatakuwepo, mambo mengi tu. Lakini leo Zanzibar zinajengwa barabara za Kikwajuni, barabara za Miti Ulaya *instead* ya kuziangalia barabara za Magharibi ambako kuna asilimia kubwa ya watu wanaishi na wapo katika hatari ya kupata maradhi na mambo mengine, lakini hatimaye barabara zinazojengwa ni za mjini na zinaachwa kuangaliwa barabara za Magharibi ambako kunaishi watu wengi.

Mhe. Naibu Spika, sio siri jambo hili linaniuma, unapoiacha kuijenga barabara ya Welezo kitu ambacho bado wananchi dada zetu na mama zetu pamoja na watoto wetu wa kike wanajifungulia majumbani, kwa sababu hawawezi kufika hospitali kwa kuwa hakuna miundombinu ukaacha barabara ya Welezo, Hawai ukenda kujenga barabara ya Miti Ulaya, Mnazi Mmoja ile pale. Kwa kweli sijui utaratibu gani unaotumika katika kufanya vile vipaumbele. Mhe. Naibu Spika, jambo hili linaniuma na nafikiri sio jambo sahihi kwa serikali.

Mhe. Naibu Spika, maafa haya ni makubwa naiomba serikali itumie ile kauli ya wahenga kinga ili mwakani yasitukute kama yaliyotukuta, kila siku itakuwa maafa haya yanatukuta kwa sababu hatujipangi. Naiomba serikali tujipange na tulinde mambo yetu ili tusiwe kila siku tunakuwa wahanga wa maafa. Mhe. Naibu Spika, ni kweli nakubali hakuna aliyeiombea mvua ni Jaalla ya Mwenyezi Mungu hatuwezi kumfikia, lakini na sisi ametupa akili za kuweza kuangalia jinsi gani tunaweza tukalinda maafa haya.

Mhe. Naibu Spika, leo hii Zanzibar sote hatujui jioni kutakuwaje, tunaokaa Magharibi hatujui tutafikaje makwetu, watoto wameanza kuzama kwenye maji, maradhi ya kipindupindu yameanza kujitokeza katika kila hali kwa maafa hayo na mambo haya yanasababishwa kwamba hatuna mitaro madhubuti. Mhe. Naibu Spika, mwaka jana yalipokuja maafa haya tulipitisha Sheria au Kanuni ya kwamba watu wasiuze vyakula ovyo. Lakini kwa sababu leo hii maafa yamekwisha, kipindupindu kimekwisha tayari vyakula vinauzwa ovyo, mabucha hayakaguliwi. Kwa hivyo tunafanya kitu hiki pale tu yanapotokea maafa yakimaliza maafa tunasahau kama maafa mengine yanaweza kuja.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima kubwa naiomba serikali yangu jambo hili ilipe kipaumbele kwa sababu wananchi wetu wanaathirika. Kama ninavyosema kila siku kazi ya mwanasiasa ni kumhudumia mwananchi na kazi ya serikali ni kumfanyia kazi mwananchi. Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali iyaangalie maafa leo hii wananchi wengi katika jimbo langu la Welezo, Kijito Upele na majimbo mengi ya Magharibi ikiwemo na Pemba hawana pa kukaa, hawana cha kukila, hawaendi skuli kwa sababu ya maafa, haya makubwa ingawaje ni Jaalla na uwezo wa Mwenyezi Mungu, lakini na sisi binadamu tunao uwezo wa kujitahidi katika kufanya kazi, Mwenyezi Mungu ametupa akili ya kuyalinda yasituathiri kitu ambacho tunajua kila mwaka majanga haya yanatokea kwa sababu ya mvua za masika hasa zikiongoka.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ya serikali kusitisha baadhi ya mambo mengi katika kuyaangalia maeneo

yote ambayo yanaweza kufika maafa haya. Tumeona tulipotaka kununua meli tulikata mambo mengi katika serikali na *Alhamdulillah* leo meli tunayo.

Mheshimiwa naiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naipenda sana serikali yangu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi na hili ni janga la kawaida kila mwaka tunapata majanga makubwa kama haya, imefika wakati kama ipo haja ya kukata bajeti hii tunayoipitisha tuikate kama tulivyoikata ya kununua meli ili tuweze kutengeneza katika maeneo mengi ya Zanzibar ambayo yanatokewa na majanga kama Welezo kujenga barabara na miundombinu mingi ambayo tulinde wananchi wetu wasiingie katika majanga ya kila mwaka.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. *Comrade* Said Mohammed Said Dimwa kwa kuleta hoja hii. Naiunga mkono kwa asilimia mia moja na ninaamini Serikali yangu ya Mapiduzi ya Zanzibar jambo hili italipokea na kulifanyia kazi kikamilifu kwa manufaa na maendeleo ya wananchi wetu wa Zanzibar wana Mapinduzi, wakwezi na wakulima naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mchangiaji anayefuata ni Mhe. Simai Mohammed Said baadaye atakuja Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata). Naomba Waheshimiwa Wajumbe lengo la hoja hii linafahamika utakuwemo Mhe. Nadir Abdul-latif usiwe na pupa umo kwenye *list* yangu. Hoja inafahamika tusirudie maneno hayo kwa hayo, ukishasema *point* yako uliyokusudia kusema maliza muache mwengine aendelee.

Mheshimiwa karibu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia kumpongeza Mhe. Said Mohamed Said kwa mara nyengine pia kuonesha ushupavu wake na umahiri wa kuwa wa kwanza katika kutusaidia sisi wenzake huku ma-*backbenchers* katika kutetea na pia kuishauri serikali kwa mambo muhimu.

Baada hapo kwa niaba ya wananchi wangu wapendwa wa jimbo la Tunguu na mimi ningependa nitoe maelezo au maoni yangu machache.

Mhe. Naibu Spika, suala la maafa ni suala ambalo sasa inaelekea duniani kote tutakuwa tunapambana nalo kila siku zitakavyoenda, kila kukicha na kila miaka itakapokwenda miaka ya mbele.

Katika hili mimi ningeomba sana serikali katika masuala ya msingi ambayo inabidi tuyazingatie ni suala zima la elimu kuweza kuwaelimisha wananchi wetu, kuweza kutambua nini maana ya maafa, aina ya maafa ambayo katika visiwa vyetu kuna nafasi ambayo tutakutana nayo. Kuna maafa ambayo tulipambana nayo katika wakati wa *MV. Spice Islander* ilipozama, Hatukuyatarajia lakini yalikuwa makubwa na ya kihistoria na nisingependa hiki kidonda kujitokeza tena.

Mhe. Naibu Spika, lakini dhima dhidi katika hili suala la elimu ni kuhakikisha skuli zetu zote hasa katika kipindi hiki waweze kuelewa watoto, vijana wetu hasa katika kipindi hiki cha mvua. Lini na wapi yanaweza kujitokeza? Kwa sababu mambo mengine ya kwenda kucheza katika mitaro, maji machafu ambayo yanaweza kuleta athari kubwa yanazidi kujiendeleza ijapokuwa tahadhari inatolewa lakini yanaendelea katika maeneo ambayo kuna mafuriko.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka nizungumze suala zima la huu Mfuko wa Maafa. Huu Mfuko kwa kweli unahitaji msaada wa ndani lakini pia na wa nje. Mimi ningeshauri katika Idara hii ya Maafa kwa usimamizi mzima, serikali itafute utaratibu mzima wa kwenda kujifunza katika nchi au visiwa ambavyo viko karibu na sisi jinsi gani wamejipanga na wao katika kukabiliana na mambo kama haya na changamoto wanazozikuta katika kipindi kama hiki cha mvua.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia sasa hivi kwa mandhari tuliyokuwa nayo na mazingira yanayotukuta mvua hizi kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na maeneo ya pwani, upande wa Tanzania Bara athari ni kubwa lakini wenzetu Tanzania Bara mitaro wameanza kujenga ili kuyaondoa maji katika maeneo tofauti. Lakini bwawa kwa mfano la Mwanakwerekwe ukiliangalia miaka nenda, miaka rudi hatujui hadi hivi sasa ni mpango gani serikali imejipanga kuyaondoa yale maji pale ambayo yanatuama kwa muda mrefu, yanaathari pia kuleta uchafu na maradhi ya mripuko lakini na homa ambazo zisizoisha kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nizungumze suala zima pale inapotokezea upepo mkali kwa wavuvi wetu. Wenzetu *Tanzania Meteorological Agency (TMA).* Nafikiri ndivyo inavyoitwa wanatoa taarifa katika mitandao ya kijamii kututahadharisha katika siku ambazo kutakuwa na upepo mkali, lakini unakuta wakati mwengine bado wavuvi wetu taarifa hizi haziwafikii. Sasa mimi

nashauri sana kwa upande wa Jeshi letu la Zimamoto na Uokozi kutafuta utaratibu ijapokuwa namba ile ipo ya 114 ya kwenye simu, lakini pia kutafuta njia nyengine kutumia makampuni ya simu kuweza kutuma *messages* kwa Wazanzibari ili ziweze kuwafika taarifa na kuweza kujua kwamba katika siku ya kesho au kesho kutwa tunatarajia upepo, aina ya upepo na maeneo utapokuwepo ili angalau binadamu anaweza kujitahadharisha kabla kwenda baharini kuvua. Mhe. Naibu Spika, inawezekana tuna wavuvi wetu wengi sana wanakuwa wanakwenda baharini hatujui idadi yao lakini wanaathirika au wanapoteza maisha yao kutokana na kipindi kama hicho kwa upepo mkali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nisingependa nirudie lakini ningependa Wawakilishi wenzangu wapate muda pia wa kuweza kuchangia hili suala. Kwa hivyo naomba sana suala la Mfuko wa Kifedha serikali ije na mkakati mzuri wa kuweza kupata fedha ili katika mipango hii yanapotokezea mambo haya ya maafa hawa wananchi wetu tuweze kuwasaidia kifedha na kwa wale ambao wanahitaji tusisubiri kama ule msemo wanaosema Wazungu kwamba, *"Don't worry about tomorrow, when it comes tomorrow it will be today"*.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru sana Mhe. Simai Mohammed Said anayefuata ni Mhe. Ali Suleiman Ali na baada ya hapo atachangia Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa taarifa hii nzito juu ya maafa au majanga yaliyotokea katika nchi yetu. Lakini pia nimpongeze Mhe. Said Mohamed Said (Dimwa) kwa kuliona hili haraka ingawa tulikuwa tunalingojea kwenye taarifa ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na ambapo lazima tulichangie kwa hali na mali.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba maafa yametokea katika maeneo yetu mbali mbali na katika watu waliokumbwa na maafa hayo mmoja ni mimi katika jimbo langu la Kijito Upele. Naweza kuchukua fursa hii kusema kwamba zinafika kama nyumba 160 hawana pa kukaa mpaka muda huu. Jana tulifanya ziara mimi na viongozi wangu wa Chama na Serikali kupitia Shehia tumeona mazingira watu wanapata tabu na kweli pa kukaa hawana. Lakini ombi langu Mheshimiwa Kamati yetu hii ya Maafa isingojee wakati wa maafa ikahangaika mitaani. Kamati ya Maafa maana yake kuratibu zile shughuli zinazotokea au matatizo kila mwaka, ikinyesha mvua maeneo gani pana tatizo.

Mhe. Naibu Spika, mimi eneo la Mwanakwerekwe Sokoni linaniuma sana. Mheshimiwa niliomba katika bajeti iliyopita kwenye Wizara ya Ujenzi, Mawasilianbo na Usafirishaji pangejengwa daraja pale pahala ikaondoa adha ile kwa wananchi wetu. Leo ukienda kila vitongoji, kila eneo mporomoko watu na foleni kama tuko Dar es Salaam, kutoka Nyumba Mbili pale kama unataka kwenda Mwanakwerekwe 'C' unaweza kuchukua hata saa moja, hilo ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ninaloomba kuna mitaro naomba katika eneo langu. Hili naomba hata jana wananchi wangu tulivyoshauriana usiku walinambia ziko nyumba kama hazikuvunjwa maafa haya yatakuwa yanaendelea kila mwaka, serikali itaingia kwenye gharama. Sisemi mimi na hiyo nilikataa kuitoa kauli lakini niliwashauri kwamba kama kamati itakuja wakiorodheshwa watu hao wako tayari kubomolewa nyumba zao wengi wamesema wako tayari kwa sababu walijenga kwa makosa.

Mhe. Naibu Spika, daraja langu la Nyumba Moja kwa Shunda. Hili ni eneo la Meli Nne bondeni hawa wananchi wangu kweli wamepata shida na watu wamejenga nyumba zimebanana baadhi ya maeneo. Ningeomba kamati hii kama itafanya ziada tufanye pamoja na wananchi wenyewe ili watoe maelekezo tupate stara huko mbele tunakokwenda na usalama wa watu wangu hao.

Mhe. Naibu Spika, pia daraja la Meli Nne Uzi. Daraja hili tunashukuru kidogo limeleta faraja. Wananchi wetu wamekwenda vizuri kutokana na ujenzi mzuri uliofanywa lakini pia baada ya kusafishwa kwa sababu kila wiki palikuwa na zoezi la kusafisha, mbele huko tunakokwenda lakini halijajengwa. Mimi ningetoa ushauri tu pamoja na mambo mengi tuliyokuwa nayo lakini kero hizi za mwaka hadi mwaka ni hatari kwa wananchi wetu. Naomba yale maeneo yenye misingi mikubwa ya maji ambayo inaleta usumbufu kwa wananchi wetu yakafanyiwa utaratibu kwa kujengwa kuweka usalama kwa wananchi wetu.

Eneo jengine Mhe. Naibu Spika, ili kuwaelezea Kamati ya Maafa ipate kujua eneo la Tomondo Uzi. Hili ni eneo hatari na watu wengi wamehama pa kwenda hawana wamo kwa majirani. Lakini jengine Kijito Upele unakwenda Kwarara, huko Kijito Upele unakwenda zako mpaka Nyumba Moja watu wetu wengi tumeungana na Jimbo la mwenzangu la Mhe. Yussuf Hassan Iddi Jimbo la Fuoni wananchi hivi sasa wanaelea na hawana pa kwenda.

Vile vile kwa Mhe. Mwanaasha Khamis Juma tumebahatika tuko mpaka mmoja, ukitoka Tomondo Uzi unakwenda Tomondo na huko watu wengi wamehama pa kwenda hawana. Kwa hivyo, ningeomba serikali tusingojee mvua tukaangalia maafa, tuandae kuondoa maafa. Kuondoa maafa wakati wa

amani tutafute yale makero yote yaliyokuwemo kwenye maeneo yetu yaondoke ili tuwanusuru wananchi wetu. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, hatari inayotokea mvua zinanyesha usiku na tumeshuhudia wananchi wetu wamelala hatujui Yarabi Salama kitatokea nini.

Kwa hivyo mimi namshukuru Mwenyezi Mungu alau jana sijui huko nje kuko vipi sasa hivi. Lakini kutokana na hali ya hewa nilivyotembelea jana na kufika leo kidogo muangaza niliopata najua kidogo yamepungua maji. Lakini kupungua huko wananchi wetu tuwasaidie kidogo chochote tutachojaaliwa ili tuwafariji kwa hali na mali kwa sababu hawakutegemea na wengine wako Pemba wananipigia simu Mheshimiwa nyumbani kwetu kumezama mkatusaidie tumeyafanya hayo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache narudia tena maafa yametokea lakini tusingojee maafa tukatafute tufanye nini. Tuondoe maafa ili lisitukute janga.

Ahsante Mhe. Naibu Spika, nampongeza mtoa mada. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mimi nitakwenda kuchangia hoja ya dharura ya Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) kuhusu maafa yaliyotokea Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hili suala tunalifahamu sote Zanzibar kwa ujumla na niwape pole Wazanzibari wote waliathirika na matatizo haya Mwenyezi Mungu awajaalie kila la kheri ya uzima na vile vile Tanzania kwa ujumla waliopata maafa haya Mwenyezi Mungu awajaalie kila la kheri pamoja na Mombasa Kenya wameathirika zaidi nao pia Mwenyezi Mungu awajaalie kila la kheri.

Lakini tunalifahamu jambo hili kwamba ni jambo ambalo sio la kutaka ni jambo ambalio *natural* linatokezea sio la makusudi wala haijataka serikali wala hajataka Nadir au Mheshimiwa fulani. Ni jambo ambalo linatokezea kwa mazingira ambayo *natural*. Sasa mimi nampongeza sana Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kwa kuleta hoja hii kwa sababu hili jambo ni muhimu sana na yeye mara nyingi huleta hapa mambo ya muhimu tukapata kuyajadili sisi wengine nafikiri tunakuwa tukikaa tunakuwa hatuyaoni sana.

Lakini nitaanza na jambo moja kama ni ushauri kama ni kuelezea. Eneo mfano la Mwanakwerekwe lile linalojaa maji pale. Mimi wazo langu kwa wizara au kwa serikali kwa jumla basi afadhali ijengwe *flyover* kwenye eneo lile, ili basi hata ikiwa pana maji *flyover* watu waweze kupita. Lakini kwa daraja nahisi

mimi kwa uzoefu wangu niliokuwa sina mkubwa kwa daraja pale linaweza kufeli. Lakini *flyover* itaweza kufanya kazi vizuri hata kama itakuja mvua ya aina gani.

Lakini suala langu jengine maana tunakwenda kidogo kidogo na wenzetu wapate kuchangia serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ijitahidi sana basi yale maeneo ambayo wanayoona wao wa mwanzo wenye kuathirika ndani ya Zanzibar, basi waweze kuzungumza nao na wawahamishe wawapatie maeneo mazuri ambayo ya karibu sio wakawape shamba maeneo wale wahame halafu wawasaidie japo na kianzio kidogo na wenyewe watajisaidia ili waweze kukaa katika mazingira mazuri.

Lakini vile vile wizara ningeiomba sana kutokana na maafa haya ya mvua kubwa inge-*focus* zaidi sasa hivi kwenye kuwasaidia masuala ya magodoro na chakula kwa walioathirika kiafya. Halafu wakakaa kwenye tathmini ambazo za zile nyumba au majengo ambayo yameathirika ili waweze kuangalia vipi wataweza kuwasiadia.

Vile vile kwenye hoja ya upande wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ningewaomba sana kwenye makato yetu tuliokubali kuchangia basi tungechangia angalau posho jengine la kikao kimoja kwa ajili ya upande wa Zanzibar tu na Pemba yaani Unguja na Pemba ikasaidia zaidi kabla ile tuliyochangia mwanzo. Tungeomba pia kama tutakubaliana sote basi kikao kimoja chengine tukatwe ili na sisi tuweze kuchangia kwa ujumla. Kwa mfano mimi jimbo langu haliathiriki sana kwenye masuala ya mafuriko ya maji lakini kunaathirika sana kwenye masuala ya kipindupindu.

Sasa ningeomba zaidi kwa sababu kwamba nisijibagulie tu jimbo langu wananchi wa Zanzibar sote ni ndugu.Ttungeomba sana kama itawezekana tukubaliane Wawakilishi tutoe posho nyengine ya kikao chengine kiwe maalum hichi kwa sababu ya Unguja na Pemba, kile cha mwanzo kilikuwa Tanzania Bara upande wa Arusha pamoja na Unguja na Pemba. Lakini hichi chengine cha pili kiwe maalum kwa ajili ya Unguja na Pemba kwa upande wetu.

Lakini jambo jengine ambalo linasababisha miundombinu hii ijapokuwa hivi vitu ni *natural* kama nilivyozungumza mwanzo. Lakini vinasababishwa pia na miundombinu mibovu na hii inatokana na wizara husika mbili Wizara ya Idara Maalum ya SMZ pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, miundombinu yao mibovu mingi katika utekelezaji wao hawafanyi kwa kiwango kinachotakikana ni kudanganya tu hakuna chengine, wale wakandarasi wanapopewa zile kazi hawafanyi miundombinu iliyokuwa mizuri

na ndio maana hivi vitu tusisingizie kama hili balaa au labda bahati mbaya au *natural disaster* kwamba inatokezea tu.

Mhe. Naibu Spika, inatokezea kwa sababu saa nyengine inasababishwa na uzembe wa utekelezaji wa wale wakandarasi kusimamia vibaya na wizara husika ambazo za masuala ya miundombinu. Mfano mdogo hapo *Airport* kutajaa maji tangu. Mimi nazaliwa mpaka leo kunajaa maji pale kwenye nyumba zile za *Airport* kwenye vituo vya petroli vya Bakharesa. Maeneo hayo ukija maeneo mengine hivyo hivyo unakuta inatengenezwa misingi kabisa barabara zinatengenezwa mara kumi kumi lakini zile *project* zao zinakuwa *failure*.

Ningeomba sana haya mambo mengine yasingeweza kutokezea kama wizara hizi mbili zitafanya kazi vizuri na hasa kwa uchunguzi kabla ya kutekeleza lile suala inapotaka kufanya *project* kutoka kwao basi wawaite watu pia wa miundombinu wakae nao waangalie sehemu gani ambazo zinazoathirika kila siku waweze kukwepa watu wasipate matatizo. Lakini ukiangalia kila siku sehemu zile zinaendelea kuwa balaa tu. Sasa mimi naomba sana wizara hizi zifanye kazi zao zinavyotakikana zisifanye kazi zao kwa kubahatisha.

Suala langu jengine Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana wizara hii. Idara ya Maafa ingeandaa eneo maalum ikajenga jengo kubwa upande mmoja kwa wanaume na moja la wanawake. Imetokezea maafa yoyote siku za mbele hatuombi lakini inapotokezea basi likuweko eneo wanaweza kuweka kuna vitanda tayari wanasaidia, vyakula. Lakini leo ikitokezea maafa watu wanakwenda kuhifadhiwa maskuli wanaekewa maturubali kitu ambacho hakipendezi.

Serikali itenge maeneo maalum ikiwa shamba ikiwa mjini wajenge majengo makubwa mawili mazuri kwa upande wa wanawake na wa kiume, kutakapotokezea mafuriko, masuala ya kipindupindu masuala yoyote ya maafa ya nchi hii basi iweze kuwahifadhi bila ya kuanza kuhangaika kutafuta maskuli madarasa na kuweka watu wakati ni maeneo ya kusoma skuli. Hivi ni vitu viwili tofauti skuli na maafa ni kitu tofauti.

Lakini suala langu jengine ningeomba sana hawa Waheshimiwa Wawakilishi walioathirika zaidi katika maeneo yao basi wizara wakae nao karibu waangalie vipi wataweza kusaidia nchi kwa jumla pamoja na hawa waliathirika, zaidi waweze kuwasaidia kwa sababu vyenginevyo watakuja kulia wananchi watawafuata wao kama alivyosema Mhe. Ali Suleiman (Shihata) nyumba zaidi 160, watakuja kukerwa na uwezo wa kusema nyumba zote au vitu vyote

kumsaidia yeye hawezi. Ningeomba sana Wizara ikawaangalia Waheshimiwa zaidi walioathirika ili waweze kusaidia katika masuala hayo yaliyotokezea.

Vile vile ningeomba sana wizara itengeneze *project,* hii Idara ya Maafa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Maeneo yote ya Zanzibar ambayo wameshaona yana hatarishi kwa wananchi yenye matatizo makubwa basi watengeneze tayari ramani zao wafanye wenyewe bajeti yao watafute na kuomba huko nchi za nje ili utengenezwe mji mpya, nyumba za bei nafuu za kuwasaidia hawa watu wawaondoshe katika zile sehemu zenye majangwa yenye mashimo na mafuriko. Tungeomba sana watengeneze kabisa hizo *project* zenu kwenye maeneo yote ya Zanzibar mnayohisi haya ni hatarishi kwa wananchi basi muweze kuwasaidia.

Lakini tukisema tu hivi tuje tuwaondoshe tuwaambie wahame hawataweza kuhama, maisha ni magumu na hii Ramadhani Mhe. Naibu Spika, inakuja tungeomba sana serikali mnafahamu ina imani na wananchi wake kuanzia Mhe. Rais, Makamu wa Pili wa Rais na sisi Wawakilishi pamoja na Mawaziri. Lakini kwa suala hili tungeomba sana wachukue hatua haraka iwezekanavyo kutokana na Ramadhani inakuja na wenzetu ndio wameshaathirika na sisi kama peke yetu hatuwezi kusema tuweze kuwasaidia tunatakiwa tufanye kitu kwa umoja.

Mhe. Naibu Spika, mimi naikubali hoja hii asilimia mia kwa mia. Nampongeza sana Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kuileta na naiombea serikali iweze kufanya kazi zake vizuri kwenye suala hili.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru sana Mhe. Nadir sasa hivi tutampisha Mheshimiwa naona Mhe. Abdalla Maulid Diwani hayupo. Kwa hivyo, nitampisha Mhe. Suleiman Makame Ali baada ya hapo nitampa fursa Mhe. Mwanashaa Khamis Juma na yeye achangie.

Waheshimiwa tumekubaliana muda mdogo. Kwa hivyo naomba mtumie muda mdogo tusije tukawa nyuma na ratiba yetu na baada ya hapo nitampa Mhe. Bahati Khamis Kombo. Mwisho kabisa atamalizia Mhe. Dr Mwinyihaji Makame.
Mhe. Suleiman Makame Ali karibu.
Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii kwa kuweza kuchangia hoja hii binafsi iliyowasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa kaka yangu hapa Mhe.

Mohamed Said (Dimwa). Mhe. Naibu Spika, mimi niunge mkono kabla ya kusema chochote kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika, maafa ni kitu ambacho hakitabiriki. Lakini Mhe. Naibu Spika, wachangiaji wengi wamesema hapa kuna baadhi ya maeneo miundombinu sio. Kwa hivyo husababisha haya maafa yakatokea. Mhe. Naibu Spika, kama mfano Pemba mimi nina umri wa miaka 27 sijawahi kusikia hata siku moja Pemba yametokea maafa namna kama hii. Mhe. Naibu Spika, leo Pemba imefika watu majumba yao kuyahama kutokana na kadhia hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi niiombe Kamati ya Maafa kuwatizama kwa jicho la huruma. Mimi jimbo langu la Ziwani hawamo kati ya hao kwa sababu sijapata taarifa mpaka hivi sasa. Lakini kama Jimbo la Chonga, Ole na Wawi kuwaangalia zaidi katika mtizamo huu kwa jicho la huruma kutokana na maafa haya yaliyowakumbuka.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia vile vile niende kwa wananchi wenyewe nikiwemo na mimi. Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo wananchi wenyewe husababisha haya maafa, kwa sababu kuna ile mitaro ya kutolea maji wanaifukia kabisa na kuitupia taka kwamba maji yasipite. Sasa likitokea tatizo usikie serikali. Kwa hivyo serikali hapa iangalie kwa kina kuhakikisha kwamba ile mitaro yote ambayo kwamba wale wananchi waliosababisha kuifukia basi wawachukulie hatua, kwa sababu tukisema kwamba kila siku tusubiri serikali itoe pesa kwa ajili ya maafa na wakati maafa mengine yanasababishwa na wananchi wenyewe. Kwa hivyo naomba serikali hapa iwe makini sana kwenye suala hili.

Mhe. Spika, lakini pia vile vile niende kwenye suala la hapo hapo kwenye maafa na Mhe. Hassan Hafidh alizungumza hapa kuhusu maafa yatakapokuja hayawi maafa mamoja, hutokezea na maafa mengine ikiwemo na maradhi ya mripuko. Kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, na hili pia liangaliwe kwa sababu hivi sasa kusema la ukweli si nzuri kutokana na uchafu unavyozagaa, kwa sababu maji yanasambaa katika sehemu mbali mbali na ma-p*ampers* yanatembea ovyo yanayotupwa na watu bila ya mpango. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hapa husababisha pia maradhi ya mripuko.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki niseme mengi langu ni hilo lakini kamati iangalie zaidi wasisubiri kwamba mpaka maafa yatokee tena patafutwe mchango, nani achangie ili wale wananchi waweze kuokolewa na maafa yale. Mhe. Naibu Spika, serikali ihakikishe kwamba maafa haya yanadhibitiwa mwanzo kama alivyosema Mhe. Ali Suleiman.

Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii niweze kuchangia machache juu ya kadhia hii iliyotukumba katika Zanzibar yetu na hoja iliyoletwa na Mhe. Mohamed Said, pia nimpongeze kwa hoja yake hii na kabla ya kusema yote naomba nimuunge mkono hoja yake hii.

Mhe. Naibu Spika, suala hili kwa kweli limetugusa watu wote hususan Wazanzibari wote wakiwemo wa Unguja na Pemba. Lakini pia niwapo pole wale waathirika wote waliopata na kadhia hii. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, suala hili hasa niwape pole akina mama yaani wanawake na watoto. Suala hili limewagusa sana akina mama na watoto kwa sababu wao ni waathirika wakubwa ambao wanakaa ndani ya majumba na katika kuhama hama hizo za maafa haya wanawake ndio tunaowana sana wanahangaika katika masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali iangalie suala hili kwa muono mkubwa kwa sababu waathirika wakubwa ni akina mama na wao ndio wategemezi wa taifa hili. Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali leo hii hapa itwambie kwa sababu mitaro ambayo iliyokuwepo ndani ya mitaa au majimbo yetu waiangalie. Mitaro ile kwa kuifanyia kazi kwa mara moja ili tuondokane na kutwama kwa maji yanayoleta athari katika maeneo yetu.

Jengine nilikuwa naiomba serikali Mhe. Naibu Spika, Kamati hii ya Maafa ifanye ziara za mara kwa mara kupitia katika sehemu zile hatarishi na kutoa elimu ya kutosha kuliko tukisubiri mpaka yatokee maafa ndio kamati ile ifanye kazi. Kwa hivyo naiomba sana serikali.

Chengine Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali hebu iangalie uwezekano wa hili Ziwa maboga. Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa ziwa hili lilioko Tomondo, Ziwa maboga siku kama hizi linaathari limeshauwa sana watoto. Sasa kwa kipindi hiki kwa mvua hizi zinazoendelea ziwa lile bado linajaza maji na yanakwenda katika maeneo tofauti yaliyokuwa karibu na nyumba wanazoishi wananchi wetu. Kwa hiyo naiomba serikali kama kuna haja au wana mipango basi wafanye mipango zaidi ya lile ziwa kupunguza yale maji au kwa kuongeza mitaro ili yaende baharini yale maji ili pale yapungue yasiendelee kuleta athari kwa wananchi wetu.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali izingatie hoja hii iliyoletwa hapa leo na watupe maamuzi ambayo serikali wameifanya kutokana na kadhia hii.

Ahsante Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia mia. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanashaa Khamis Juma, sasa nampa nafasi Mhe. Bahati Khamis Kombo baadae ni Mhe. Maryam Thani Juma ameniomba dakika tano nitakupa na baada ya hapo tutampa Mhe. DKt. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia kutupa uhai na uzima na leo tukafika hapa katika Baraza letu hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Mohamed Said (Dimwa) kwa kuleta hoja hii hapa Barazani.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli maafa yametukuta lakini tuone kwamba wananchi wetu na sisi Wawakilihsi wao tunaungana nao katika maafa hayo. Mhe. Naibu Spika, katika Jimbo langu pia na mimi maafa yamenikuta. Lakini niseme katika kunikuta maafa haya katika Shehia ya Kwa Azani na katika Shehia ya Chumbageni ambapo Shehia hii imeandamana na daraja lililopo Zawadini. Niseme kwamba lile daraja ndio lililosababisha maafa yaliyowakuta wale wananchi wa kijiji kile kwa sababu lile daraja ni la zamani na lile daraja liko chini kabisa. Sasa maji yote yanapokuja yanaafika mpaka katika majumba.

Sasa niombe serikali kwamba "Kinga ni bora kuliko tiba". Haya ambayo yametufika kwa mwaka huu pale yalipofika basi tuombe kwamba yasije yakarejea tena. Ni kulifanyia ukarabati lile daraja na ukarabati wenyewe wa pale naomba serikali iweze kutafuta njia ya kukuzwa juu lile daraja, kwa sababu hata maji yakijaa pale basi gari ilioko huku ndio imekaa na iliko huku ndio imekaa kabisa. Nikisema hilo ni shahidi Naibu Waziri wa Mawasiliano juzi tu alikuweko katika jimbo langu amelishuhudia hilo. Kwa hivyo kwanza hilo Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali ilizingatie kwa kina.

Lakini vile vile katika Shehia yangu ya Kwa Azani Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Shehia ile ina kilio na tunaolia ni sisi akina mama. Kwa sababu kilichotokea kule wazee wamelala na watoto wamelala, lakini watoto wakajakushitukia tayari maji yamekuwepo ndani, wakaamsha wazazi wao

wakatoka, wakafanya ya kufanya mule ndani ili mradi watoke ndio wapate nusura. Lakini vile vile yanasababishwa na mazingira ambayo yako kule Kwa Azani. Kwa hivyo naiomba serikali ikaangalie yale mazingira ambayo yanaweza kusaidia basi yasaidiwe, kwa sababu kuna migomba mingi ambayo iko karibu na majumba na migomba ile tumeona ndio sababu tosha inayosababisha haya maji kukaa kwa sababu hayana njia. Ile njia iliyokuwepo zamani misingi imepandwa migomba imekuwa ni tatizo.

Lakini Mhe. Naibu Spika, tukija katika daraja lililopo Kimbuni. Lile daraja kwa wale Wawakilishi wa Pemba wanaona kwamba sehemu ile ni ya maji makubwa sana. Kwa hivyo tunaiomba serikali kwamba iende pale na itusaidie angalau kuta katika zile sehemu ambazo wanakaa wananchi ili yale maji yaweze kuzuilika na yaweze kupita katika lile daraja tu. Lakini bila ya hivyo Mhe. Naibu Spika, ikiendelea mvua kubwa kama hii basi tutazidi kupata maafa makubwa sana. Kwa hivyo naiomba serikali ituangalie juu ya masuala haya, hasa katika kisiwa cha Pemba kwa sababu mvua hizi za mara hii ndio kubwa zaidi ambazo ilianza kuleta majanga.

Pia Mhe. Naibu Spika, katika daraja liliopo Kibirinzi. Mhe. Suleiman Sarahan hapa siku zote analipigia kelele daraja lile na maji makubwa yaliopo pale ni hatari. Sasa hivi ikinyesha mvua basi wanafunzi walioko Kibirinzi wanabakia Kibirinzi na hawawezi kutoka kuja kama skuli ya Madungu au Shamiani. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, tunaiomba sana serikali itupie macho sana madaraja hususan yaliopo Pemba.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi).*

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ili kuweza kuchangia machache kwa mambo haya ya maafa ambayo yametufikia katika nchi yetu ya Zanzibar. Kwanza kabisa nampongeza Mhe. Mohamed Said Dimwa kwa kuleta hoja hii ambayo ni muhimu kwetu, ili wananchi wetu waone kwamba tunawajali kwa pale ambapo wanafikwa na matatizo kama haya yaliyotupata katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, na mimi napenda kusema kwamba nawapa pole sana wananchi wa Zanzibar ambao wamefikwa na maafa haya, kwa wale ambao wamevunjikiwa na majumba yao na vile vile kutokana na usafiri wa barabarani ambao na sisi wasafiri tumekuwa tukipata usumbufu mkubwa kutokana na mvua kubwa ambazo zinaendelea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, na mimi napenda kuishauri serikali kwamba pale ambapo litatokezea tatizo kama hili, ipo Kamati maalum ya Maafa. Hivyo Kamati hii ya Maafa kabla mvua kubwa hazijatokea na wanajua kwamba sehemu fulani ni hatarishi na sehemu fulani pia ni hatarishi na mvua zinazokuja huenda zikawa kubwa na zikaathiri sehemu zile husika ambazo wanaishi wananchi wetu. Sasa kamati ingefika mapema ikaona kwamba kama ni kuwahamisha wananchi kabla tatizo halijatokezea, wakaandaa utaratibu wa kuwaweka wananchi wale, ama kufanya utaratibu wowote ili sehemu zile kabla mvua kubwa hazijanyesha zikaepukana na zile athari kubwa ambazo zinatokezea.

Vile vile tumeona kwamba barabara nyingi hazipitiki na mimi niseme katika jimbo langu ziko barabara ambazo zimeathirika sana na Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji bado hawajazifanyia utengenezaji. Lakini serikali kwa kupitia Mwakilishi wao mpango huo tunao wa kuwasaidia wananchi wetu wa kijiji hiki cha Chozi ambacho wana usumbufu mkubwa wa barabara. Wananchi hawa kwa kweli mvua hizi kubwa zinazonyesha wanapata tabu sana ya usafiri na barabara zao zinakuwa mbaya hazipitiki kabisa kuja mjini kufanya shughuli zao za kibiashara. Kwa hivyo naiomba serikali ijitahidi sana kutusaidia sisi Wawakilishi ili kutatua matatizo haya yanapofika kwa wakati huu wa mvua kubwa ziponyesha.

Mhe. Naibu Spika, mimi sijapata taarifa nyingi za uharibikaji lakini kuna baadhi ya wananchi wangu ambao mashimo yao ya makaro yameharibika. Kwa hivyo nawaasa wananchi hawa kutokana na mvua hizi maradhi ya mripuko huwenda yakawaathiri. Hivyo wajitahidi sana kufanya usafi ili kuepukana na maradhi haya ya mripuko yasije yakawatokezea katika maeneo yao kutokana na mvua kubwa zinazotokezea.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, naishauri serikali kwamba kuwe na mfuko maalum ambao utawasaidia wale waathirika na sio kukaa tukajadili sasa. Mfuko utengenezwe kabla ya maafa hayajatokezea ili kuona wananchi wetu tunawasaidia vipi. Mhe. Naibu Spika, utakapowekwa mfuko huu maalum haitatokezea leo tuchangie nini, wahuku tuchangie nini na wa huku tuwafanye nini. Mfuko huu utumike pale ambapo maafa yanatokezea.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Mohammed Said Dimwa kwa kuleta hoja hii. Naiunga mkono kwa asilimia mia. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*
Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame karibu, baadae atachangia Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Said Soud Said, na baada ya hapo nitampa Mhe. Waziri wa Nchi

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na yeye aseme machache, akimaliza tunampa mwenyewe muwasilishaji wa hoja kwa ajili ya kufanya majumuisho. Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame karibu.

Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi niseme machache sana kuhusu hoja hii ya Mhe. Mohammed Said Mohammed, mwakilishi mahiri wa Jimbo hili la Mpendae kuhusu suala la maafa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mengi mazuri yametangulia kwa Waheshimiwa sitaki niyarejee. Lakini mimi nataka kusema kwa uchache kabisa kwamba kubwa hapa Mhe. Naibu Spika, tulilonalo wazungu wanasema ni *disaster preparedness*, utayari wa kujikinga na maafa, hili ndio suala la msingi sana. Mhe. Naibu Spika, tusingoje kukabiliana. Unajua hili neno tukiliweka la kukabiliana na maafa linatupotosha, zaidi twende na utayari wa kujikinga tunajitayarisha vipi. Hili ndio suala la msingi sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika moja ya hotuba zake katika kipindi kilichopita alizungumzia suala zima la kufanya maamuzi magumu. Lazima kwanza tuwashauri watu tuwaambie. Lakini mnajua mtu kila mmoja anataka pakukaa. Sasa mwaka humu mtu mwengine anajipeleka mwenyewe anakwenda bondeni kwa makusudi. Sasa analeta shida, analeta matatizo pale taifa haliwezi kukaa kimya yule ni mwananchi lazima tumtizame.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ndio nasema ile kauli ya Mhe. Makamu wa Pili aliyoishauri au aliyoelekeza ipo haja tuitumie, ni lazima fufanye maamuzi magumu kwa baadhi ya sehemu, haiwezekani. Pale Mwanakwerekwe hakuna asiyejua panavyojaa maji na ni njia ya maji, kwenda kujenga kituo cha mafuta pale. Baya zaidi kimeshajengwa kile lakini kuna misingi mitatu pale maji yamejaa hasa ile *level* ya misingi yanazuwia hata yale maji kupita, na yanasababisha kile kivuko cha maji kiwe kidogo. Sasa ndio hayo nazungumza maamuzi magumu mheshimiwa ni pale pamoja wapo.

Mhe. Naibu Spika, tumezungumza Kariakoo *Alhamdulillah drainage* maji yanakwenda. Lakini nitatoa mfano mwengine Mhe. Naibu Spika, Kisauni pale au Mitondooni yuko mfadhili mmoja kaamua ajenge nyumba ya ibada Msikiti, lakini kaambiwa pale maji yanatuama, yanatoka mabondeni mote yanakwenda kutuama pale. Ukitaka kujenga Msikiti basi ujenge kama Msikiti Mabluu. Sasa yule kwa bahati mbaya kumbe alikuwa na mipango yake, alitaka kujenga na milango ya maduka. Sasa sasa hivi sijui yamekwendaje mambo. Sasa hivi

kaanza ujenzi ule na kuanza kaanza na milango ya maduka. Kwa hivyo *Alhamdulillah* ndio nasema kumbe nia yake haikuwa nzuri.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa namuomba sana Mhe. Mohamed Aboud kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili tukitoka hapa twende zetu Kisauni nikamuoneshe pamejaa maji na pamefurika kabisa ule msingi wote. Sasa huo Msikiti wenyewe sijui watu watakwendaje. Kwa hivyo ndio hayo ninayosema tumkinge yule asiifanye ile kazi kabisa na suala zima la *environmental Impact Assessment.*

Mhe. Naibu Spika, hili ni suala muhimu sana. Mradi wowote hawa watu wawe *responsible*, sio kwa mradi huu tu lakini kwa mradi mwengine wowote tuhakikishe kwamba ule mradi uko *environmental friendly.* Lakini naongeza pia uwe *human friendly*, yaani uwe rafiki kwa jamii, usiweke mradi ukawatesa jamii. Haya ni mambo ya msingi sana Mhe. Naibu Spika, kuyazingatia. Kwa hivyo mimi nilitaka kusisitiza sana suala la kujikinga, kujiandaa na kukabiliana. Tusingoje kupambana tu.

Mhe. Naibu Spika, halafu nimalizie kwa kumuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Nashukuru jana nilisikia kwenye vyombo vya habari kwamba aliitisha Kamati ya Kitaifa ile, ni jambo zuri sana nampongeza sana kwa hatua ile. Lakini ile *multi disciplinary effort,* zile juhudi za pamoja ziwe za pamoja kweli, wengine hawatimizi. Tatizo letu ni *drainage*, maji yale hayana pakutokea yanakwenda kutuwama pahala yanafanya athari. Sasa tunampa kazi ile aifanye. Mabarabara yetu mengi sana, nenda Kiembesamaki kwa Marehemu Mzee Juma Ame pale, sasa hivi ukipita pale maji tele yametuama kwa nini. Sasa tunayempa kazi ile aifanye haifanyi, sasa hivyo sio vizuri. Ni lazima Mheshimiwa tunayempa kazi aifanye, sote tu-*act* kwa upande wetu, tutaliondosha hilo tatizo. Lakini kama tunampa kazi mwengine afanye na hafanyi tunangoja kuja kutibu tu, hatutafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kupongeza sana hoja hii na mimi nilikuwa..., kanipunguza kasi, nilikuwa nina maneno mengi katika hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili kwenye suala hili lakini inabidi tena tuchangie huku, huko tena tuta-*resolve, message* ndio hiyo kwamba tujitayarishe kwa pamoja sote Mheshimiwa tuutowe muhali. Mtu ambaye anatuathiri tusimuonee huruma. Nawashukuru baadhi ya ma-*DC* wamefanya kwenye mashamba na sisi tufanye kwenye mambo ya kawaida huku, yanakera. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala kwa kutujaalia kutupa neema hii ambayo tunaijadili hapa, naamini kwamba ameileta kwa nia ya kutusaidia sisi waja wake ili tuweze kupata mambo mengi tu ndani ya rehma hii.

Pamoja na hayo nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na Kamati yake kwa ajili ya kuona suala hili, na hasa pale walipotoa maamuzi ya kuwasimamisha wanafunzi wa skuli za Unguja na Pemba, ili waweze kukaa majumbani katika hali ya kunusuru maisha yao. Mhe. Makamu wa Pili pamoja na kamati yake naamini alifanya hili katika kutekeleza sera ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu Chama cha Mapinduzi nia yake ni kuwaona Wazanzibari wanaishi kwa vizuri bila ya kupata matatizo ya aina yoyote. Sasa kwa hilo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nakupongeza sana na tunaamini wewe ni jembe katika nchi hii.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kuwaomba wazazi wachukue juhudi za makusudi katika kuwalinda watoto na sehemu hatarishi kwa sababu ni kweli kabisa wamezuiwa, lakini wamezuiwa kwa maana ya kwamba wawe salama. Sasa ni wajibu wa kusema wazazi na walezi wachukue nafasi hii ya kuwazuwia watoto wao katika sehemu hizo na sisi pia tuchukue hatua za kuwasaidia wazee wetu wasiojiweza, tuwasaidie walemavu wa macho na pia tuwasaidie walemavu wa akili ili kuondoa janga hili la maafa ya vifo ambavyo hatuvitegemei.

Mhe. Naibu Spika, vile vile juhudi za makusudi zichukuliwe kwa Kamati hii ya Maafa kwa wale ambao huamua kujenga mabondeni, watu ambao wanajenga katika njia za maji. Watu kama hawa kuwajadili kwa kweli ni kazi kubwa sana lakini nadhani kuna haja ya kupewa barua za ushauri nasaha ili wajione kwamba serikali imechukua hatua za kuwaasa waondoke ili kuepusha maafa ambayo kila siku ni mzigo kwa serikali.

Mhe. Naibu Spika, maafa hayana itikadi ya kisiasa, yanapokuja yanakuja tu na wala hayachagui chama cha mtu. Kwa hivyo ninatoa wito kwa Wazanzibari kwamba hii ni nafasi yetu ya kusaidiana kwa wale waliopatwa na majanga, bila ya kujali rangi, kabila na Dini ili tuweze kupata nafasi ya kuyaepuka majanga haya kwa pamoja, huu ni msiba wa Wazanzibari na Watanzania wote. Kwa maana hiyo tuna haja ya kushikamana na hoja hii kuweza kunusuru maisha ya Wazanzibari na Watanzania wote.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Sawa. Sasa nimpishe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aje na yeye azungumzie kwa niaba ya serikali. Mhe. Waziri karibu sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi. Aidha, nimshukuru na nimpongeze Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa kwa hoja yake hii ya dharura. Vile vile nimshukuru Mhe. Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia katika hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme kwamba Kamati ya Maafa ni chombo kikuu kinachosimamia masuala ya maafa, na kamati hii ina wadau mbali mbali, *secretariat* yake ndio Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, kazi yake ni kuratibu mambo haya. Lakini kuna wadau wanaokwenda moja kwa moja katika kuyakabili maafa yenyewe hususan vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Kwa hivyo, ni kamati yenye wahusika wengi inayokaa kuzungumzia mustakabali wa kupambana na tatizo la maafa. Kama mlivyosema Waheshimiwa Wajumbe sio kwamba inafanya kazi pale yanapotokea. Kamati hii hutoa mtazamo wa mambo ya dharura muda wa kati na muda mrefu. Mambo mengi yanayofanywa na serikali ni pamoja na kuona namna gani tunakabiliana na maafa. Haya mengine yanayofanywa kwa kila siku basi yamo katika mtazamo mkubwa wa serikali namna ya kukabiliana. Kwa hivyo sio jambo linalodhaniwa kwamba linafanywa kwa dharura, linafanywa kwa kadri ya uwezo wa hali ya serikali. Tatizo la msingi ni uwezo wetu wa uchumi ndio tatizo letu. Bado tunahitaji kuimarisha uchumi wetu uwe mkubwa ili tuwe na uwezo mkubwa wa kifedha katika kuyafanya mambo ya msingi kama Waheshimiwa mlivyoyaeleza.

Mhe. Naibu Spika, matatizo ya msingi ambayo kwa kiasi kikubwa yangekuwa na mtazamo mkubwa. Kwanza ni suala zima la utaratibu wetu wa ujenzi. Nchi ilihitaji vyote vimepimwa vizuri, yametengwa maeneo ya ujenzi ya makaazi ya watu, yametengwa maeneo ya kilimo, yametengwa maeneo ya viwanda, zimetengenezwa njia za michirizi ya maji machafu, tumeweka utaratibu mzuri wa mtandao wa maji ili maji hayo yote yanakuwa *treated* vizuri kwa kutimizi vigezo vyote vya kiafya tumeweka msingi mzuri wa kujenga miundo mbinu, bora yakiwemo madaraja, barabara na kadhalika kuwa na zana vifaa mbali mbali zikiwemo meli, *risk boat*, ndege, *helicopter* n.k.

Kwa hivyo sio jambo jepesi mkafikiri ndugu Wajumbe kwamba linafanywa kwa dharura, linafanywa kwa mipango. Katika mipango ya kiserikali ya muda mrefu na muda wa kazi na wa dharura yanapotokea. Kwa hivyo tunazungumza lugha moja namna ya kulikabili jambo hili. Kwa hivyo cha msingi hapa sote kwa pamoja tushirikiane kuimarisha uchumi wetu tujenge nguvu kubwa zaidi ili haya mnayoyasema yote yawezekane maana yangewezekana tungewajengea wananchi wetu nyumba za kukaa mahala muafaka kabisa, pahala pazuri kabisa ambapo wasingepata athari hizi.

Lakini jambo la msingi ni uwezo wa ujumla wetu. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe ningependa jambo hili tulielewe na tulifahamu kwa pamoja sote kwamba hiyo kazi yetu ni pamoja lazima tuwe na miundo mbinu mizuri ya umeme, maji, mtandao mzuri wa afya wa elimu na kadhalika na yote haya yanahitaji fedha ndio maana kila mwaka tunakuja hapa tunapanga mambo yetu. Msingi wake pia ni kuepukana na haya majanga ambayo yanatokea. Majanga haya yana sehemu mbili, yako yanayosababishwa na binadamu mwenyewe na yapo yanayokuwa ni kudra ya Mwenyezi Mungu. Kama hilo suala la mvua limetokea hatuna namna kwa mara ya mwanzo kule Pemba milima imeanza kuporomoka inaangukia nyumba. Bahati nzuri tushukuru Mwenyezi Mungu kwa kiasi kikubwa nyumba zilizoangukiwa hazikuleta athari ya mauti na hasara nyengine, isipokuwa nipende tena kurudia kutoa pole kwa kijana wetu mmoja ambaye aliangukiwa na ukuta wa madrassa pale Chanjaani na akafariki dunia.

Kwa hivyo kwa kiasi fulani jitihada zinafanywa na shughuli zinaelekezwa vizuri na Kamati yetu inafanya kazi nzuri. Tatizo la msingi ni uwezo wa kukabiliana na changamoto nyingi ambazo zipo. Hatua zilizochukuliwa kwa dharura Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu viongozi kwanza wametembelea maeneo yote. Tathmini imefanywa tumejua walioathirika, nyumba ngapi zimeathirika, tatizo ni lipi na nini kifanyike katika kukabiliana navyo. Elimu kwa umma imetolewa taarifa ya Serikali inatolewa na zinaendelea kutolewa kila siku hatua nyengine ni ya jana hii ya kufunga maskuli kwa muda wa siku tatu ili kutizama hali ya hewa kutokana na taarifa ambazo wenzetu wa hali ya hewa wametupa. Kwa hivyo yote haya mambo yanafanyika ili kuepusha wananchi wetu wasipate madhara makubwa.

Suala la mvua ni kudra na sote tunataka mvua zinyeshe, tunaomba zinyeshe mvua za kheri ili zitusaidie kwa maendeleo ya kilimo kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula, misaada mbali mbali imeanza kutolewa na itaendelea kutolewa kuwasaidia wale ambao wamo katika hali ngumu zaidi. Kwa mfano kuna watu ambao tayari wamekosa nyumba zao za makaazi, majirani zao ndugu zao wapenzi wao wamewachukua kuwahifadhi katika nyumba zao. Kwa hivyo

watu hao waliowahifadhi wengine wana mzigo mkubwa wa kuhudumia zile jamii ambazo wamekwenda kukaa nazo pale. Kwa hivyo lazima kuwe na utaratibu kwa kiasi fulani Serikali isaidie. Napenda nichukue fursa hii kwa upande wa viongozi wetu wa Mikoa na Wilaya kwa urataribu uliowekwa katika kazi wameanza kuchukua hatua za awali kusaidia na Serikali Kuu inaendelea kuchukua kila hatua kusaidia ili kuepukana na janga hili.

Mhe. Naibu Spika, lakini kubwa zaidi hapa ni suala la maradhi ya mripuko inapofika wakati kama huu maji haya tunayoyatumia huchanganyika na maji ambayo sio salama na matokeo yake ikatupa athari kubwa. Serikali imejipanga katika kuhakikisha kwamba kila hatua zinachukuliwa ili kuepuka maradhi ya mirupuko na hatua zimeanza kuchukuliwa siku nyingi hata kabla ya mvua kutokea kama wengi wetu hapo wamefuatilia katika vipindi vya *ZBC* mtakuwa mkiona Halmashauri zetu, viongozi wa Wilaya na Mikoa na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa tukitoa taarifa mbali mbali ikionesha hata skuli ambazo vyoo vyao sio vizuri, ikifunga baadhi ya mikahawa na kadhalika. Mhe. Naibu Spika, yote hayo yamefanyika msingi wake tumejua kwamba yanaweza kuleta athari kubwa na yataleta maradhi ya mripuko. Sasa tunajipanga kwenye suala zima la kuelimisha wananchi kuitumia vizuri *chlorine* na kuchemsha maji vizuri na kuchukua hatua mbali mbali ambazo zitaleta salama za kuepuka maradhi.

Mhe. Naibu Spika, lakini kikubwa zaidi taasisi zetu zimekuwa na *coordination* nzuri na mashirikiano ya pamoja katika kukabiliana na hali pale inapotokea, mtaona hata madaraja yaliyovunjika haraka haraka hatua zinachukuliwa kurudisha katika hali yake ya kawaida, ijapokuwa kwa sasa hata ukirudisha bado mvua zinaendelea kunyesha, hujui athari gani itatokea lakini kila lile ambalo limeleta athari tumejaribu kuchukua, kila hatua ili tusipoteze maisha ya wananchi wetu. Mimi ningependa sana Waheshimiwa Wajumbe muone kazi iliyofanywa na Serikali, muone kazi iliyofanywa na wananchi mbali mbali na tuwapongeze katika hali hiyo kutokana na hali halisi ya umaskini wetu. Kwa hivyo suala la kuambizana na kuendelea kutoa taarifa ni suala siku zote lipo katika mipango yetu ya kibajeti, ipo katika mipango yetu ya muda mfupi, ipo katika mipango yetu ya muda wa kati na muda mrefu na hatua zote zitaendelea kuchukuliwa ili kunusuru jamii yetu.

Mhe. Naibu Spika, hatua mbali mbali zimechukuliwa hata mukiona huo mradi wa *ZUSP* ni pamoja na kusaidia majanga yasitokee na imesaidia sana katika yale maeneo ambayo mmeshauri maji yale yaliyokuwa na athari kubwa yameanza kupungua, bado hatua nyengine zitachukuliwa katika maeneo haya yakiwemo Mwanakwerekwe pale, Kiziwa Maboga na kwengine kuna utaratibu

pia wa kiserikali unaoandaliwa katika kupambana na hali hiyo. Lakini mambo yote hayo yanahitaji fedha nyingi, yanahitaji mipango mikubwa katika kutekeleza kwake.

Mhe. Naibu Spika, kwa ufupi huduma za afya tumejipanga katika kukabiliana na jambo hili. Mtandao wa maji tunajitahidi kuchukua hatua ili usilete athari zaidi na hatua nyengine zinachukuliwa pale mambo yanapotokea ili kuyakabili vizuri kuepukana na athari zinazoweza kutokea, tutaendelea kufanya hivyo kwa mashirikiano makubwa ya wote, Waheshimiwa Wajumbe naomba muelewe kazi yenyewe sio nyepesi inahitaji mashirikiano ya pamoja.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukueu ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru kwa maelezo yako mazuri sana. Waheshimiwa Wajumbe tumeona Serikali kwa kweli inafanya kazi. Kwa hivyo tuipe nafasi iweze kufanya zaidi pamoja na michango yenu mimi naamini kwamba Serikali imechukua na itaweza kuyafanyia kazi. Kama kuna suala lolote kila Mjumbe wetu ana nafasi nzuri ya kuonana na wahusika na akaweza kwenda kutoa ushauri wake katika maeneo yetu tuliyonayo.

Sasa baada ya kusema hayo sasa nimkaribishe mwenye hoja Mhe. Mohammed Said Mohammed *(*Dimwa*)* na yeye afanye majumuisho na kwa utaratibu wetu huwa tuna maazimio. Sasa kwenye hili naamini bada ya maazimio haya Serikali pia italeta ripoti yake namna gani imeyafanyia kazi ambayo hayo tuliyokubaliana humu ndani.

Karibu sana Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa kushukuru sana lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa majibu yake mazuri na ku-*react* vile ambavyo wananchi walikusudia wamsikie lile neno ambalo amelisema nikushukuru sana kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza tu niwataje wale ambao wamechangia hoja yangu kwa moja kwa moja lakini baadae nitawataja wale waliochangia kwa maandishi. Wale waliochangia moja kwa moja ni:-

1. Mhe. Hassan Ameir Hafidh
2. Mhe. Simai Mohammed Said
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf
5. Mhe. Suleiman Makame Ali

6. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
7. Mhe. Bahati Khamis Kombo
8. Mhe. Maryam Thani Juma
9. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
10. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) MBM,
11. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed Waziri katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Lakini wale ambao wamechangia kwa maandishi, naomba sasa Mhe. Naibu Spika, nao niwataje na muwatambue ni:-

1. Mhe. Nassor Salim Ali
2. Mhe. Asha Abdalla Mussa
3. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
4. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
5. Mhe. Ali Khamis Bakari

Mhe. Naibu Spika, hoja zote ziliendana sana na hoja yenyewe ambayo ilichangiwa lakini pamoja na hoja mahususi iliyochangiwa ni jinsi gani wananchi wasikie kauli za wananchi wao. Lakini na kuona Serikali je, jitihada gani imezifanya mpaka sasa kama maazimio yetu yalivyokusudia na tunaishukuru Serikali ime-*react* vizuri na inafanya vizuri. Kwa sababu tumeanza kuisikia kwenye vyombo vya habari lakini haitoshelezi tu kwenye vyombo vya habari wengine hawana vyombo vya habari, kuwa Kamati ya Maafa imekutana na imeamua nini wananchi wanafaidika, kwa sababu wengi wanyonge wenye kipato cha chini na cha kati ndio walioathirika na kadhia hii kubwa. Lakini leo wamemsikia Mhe. Waziri ndani ya Baraza la Wawakilishi chombo kikubwa cha wananchi akiyatamka yale ambayo wananchi wameyataraji. Hongera sana Serikali mmefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa wengi niliowataja kuchangia wamechangia mambo mbali mbali lakini si vyema nikayajumuisha yote kwa kila mmoja wao. Lakini nitayajumuisha kwa pamoja ili kuanza kukidhi na muda lakini kwa sababu tulipata majibu mazuri ya Serikali hatuna haja yote kuyasema moja, mbili, tatu mpaka kuendelea sasa nitasema tu baadhi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanaasha alichangia lakini sehemu kubwa ambazo tulikuwa tunazipigia kelele ni Kiziwamaboga, Sebleni, Mwanakwerekwe, Kwa bintihamrani lakini hata na Pemba ni sehemu nyingi safari hii. Wenzetu Pemba walikuwa hawajaanza kupata maafa ya mafuriko lakini safari hii wamepata

maafa ya mafuriko tena ni makubwa sana Mwenyezi Mungu atuepushie na mambo hayo tena.

Lakini jengine Kiziwamaboga Mhe. Mwanaasha alilia kusema linasababisha vifo vingi vya watoto vinavyotokea mara kwa mara. Ningeomba tu Serikali ichukue jitihada nyengine za makusudi kwenda kutembelea na kuona athari kubwa ambazo zinapatikana na kuziondosha mara moja. Lakini vile vile tumeona Mhe. Waziri amesema si jambo rahisi, maana yake kutekeleza lakini mimi nasema lipo jambo rahisi la kutekeleza. Tulikuwa na janga la meli lakini Mhe. Rais kwa makusudi alikata bajeti na kuanza kuweka vitu mbadala na meli ya MV Mapinduzi 11 tumeiona na sasa hivi tunasafiri kwa uzuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia na Serikali nataka kusema na jambo hili ni rahisi tunaweza kukata bajeti tukaangalie maeneo yale muhimu. Leo sehemu ya Mwanakwerekwe wanapita katika lile daraja ambalo Mhe. Shamsi amelijenga ambalo maarufu linaitwa daraja la Shamsi. Lile sio daraja, kile ni kivuko kwa sababu kuna gari kubwa sana zinapita pale halina uwezo wa kuchukua uwezo huo, tunaweza kufika pahala hata kile kivuko sasa kikaondoka tukaanza kupeana mikono na Mhe. Ali Suleiman Ali njoo huku nenda kule. Sasa hili tungeliomba tu Serikali ifanye jitihada.

Mhe. Nadir alisema tujenge *flyover* lakini kwa Serikali yetu sifikirii kama uwezo huo inao lakini hata hicho kidaraja tufikirie namna gani tunaweza kuondokana na mafuriko yake na kadhia kubwa ya wananchi kwenda kupita.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji amesema pale pana kituo cha mafuta ya petroli, pana mambo mengi ambayo yamejengwa pale si vyema kuacha wananchi wakiwa vile. Lazima tutekeleze maamuzi magumu lakini tuwapangie wananchi kwa sababu jambo hili ni la kila mara ambalo tunalisema hapa hawa wameingiliwa na maji, hawa wamepata kadhia hii, lakini lazima Serikali iwe na maamuzi magumu ya kuondosha pahala pamoja na kuwapa sehemu nyengine ili wananchi wale wasiadhirike nayo.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile niwapongeze kwa huu mradi wa *ZUSP* ingawa haujakamilika lakini umetupa angalau kidogo mwanga mzuri wa kuona. Niwaambie tena Serikali inayoongozwa na Chama changu kuwa ni vyema sasa Kamati hii ya Maafa kufanya kazi muda wote. Niliona bajeti ya mwaka jana kuna vituo mbali mbali vya maafa vinajengwa lakini sijui kama mara hii itajitokeza tutaangalia jinsi ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo mapana sana na kuona Serikali ime-*react* vizuri kwa sasa naomba nitoe hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe muwasilishaji wa hoja ametoa hoja wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiw)

Waheshimiwa Wajumbe kama mnakumbuka kulikuwa na miongozo miwili. Moja ilikuwa inahusiana na hoja hii ambayo tumemaliza, lakini jengine lilikuwa linalohusiana na vitabu vya Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2016/2017. Sasa kwa kuwa vitabu hivi tayari vipo, mimi ningeshauri kwamba tunaendelea na Hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu tayari jibu limeshatoka Serikalini vitabu vipo. Sasa naomba tuendelee na shughuli yetu ya vitabu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru baada ya kuliona hili pale pale uongozi wa mbele uka-*react* lakini cha kusikitisha kwa nini tupate muda mdogo kiasi hichi. Kwa maelezo naambiwa vilikuwepo katika jengo hili, sasa sijui kuna hofu ya nini kuvipata mapema kabla ya muda wake ili tulipoingia kama jana tumekabidhiwa kitabu cha hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais, tulikuwa tukae pamoja hivi ili tupate kujenga hoja vizuri zaidi lakini kama sasa hivi tabu ni kubwa imekuwa bure na sasa hivi muda wenyewe huu hautoshi. Kwanza muda mnatunyima mdogo sana. Sasa naona kama mnatuondosha njiani katika hili Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nimekusikia na ushauri wako nafikiri Serikali utalipokea kwamba mara nyengine vitabu vitafika mapema. Leo tunachoweza kufanya ni kwamba hotuba itatolewa muda utakaobakia mdogo tutaahirisha kikao, tutarudi tena mchana kwa ajili ya kuanza kutoa michango.

Sasa baada ya kusema hayo nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aje kwa ajili ya kusoma hotuba ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2016/2017
Wizara ya Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nategemea Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wamepata masahihisho kidogo ya hotuba yangu inayohusu tarakimu, kuanzia ukurasa wa 56, kwa hivyo naomba ipokelewe.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kwa niaba ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutoa pole zetu za dhati na rambi rambi kwa wafia wote wa wanafunzi 32, walimu wawili na dereva kutokana na ajali iliyotokea huko Arusha juzi naomba wafiwa wote hao wawe na subira na uvumilivu kutokana na kuondokewa na wapendwa wao hawa Mungu azilaze roho za marehemu pahala pema peponi. Amin.

Aidha, Mhe. Naibu Spika, napenda kuwapa pole zangu za dhati wananchi wote wa Unguja na Pemba walioathirika na kubomokewa na nyumba zao kutokana na mvua kubwa za masika zilizonyesha katika kipindi hichi, serikali inafanya tathmini ili kuona kiasi gani serikali inaweza kuwasaidia wananchi hao nawapa pole sana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo sasa, naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu lipokee lijadili na hatimae likae kama kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mtukufu mwingi wa Rehma kwa kutufikisha hapa katika Kikao hichi cha Baraza la Wawakilishi ikiwa katika hali ya amani, furaha na mshikamano wa hali ya juu katika Nchi yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu akipe kikao hichi Baraka ili tukiendeshe na tukimalize huku tumefika azma yetu tuliyokusudia. Matumaini yangu kuwa Baraza lako Tukufu litaipokea, kuijadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Makamu wa Pili wa Rais ili tuweze kupata nyenzo za kutumikia wananchi wetu kikamilifu.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa napenda kumpongeza na kumshukuru Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hekma na busara anazozitumia katika kuiongoza nchi yetu

kulipopelekea kupata maendeleo tuliyonayo sasa ambayo kila mmoja wetu anafaidika nayo, hakika juhudi na miongozo yake anayotoa imeonesha nia azma njema aliyonayo kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla juu ya kukuza uchumi wa nchi yetu na kuondokana kwa umasikini ni jukumu letu sisi viongozi tunaomsaidia na wananchi wote kwa jumla kuhakikisha kuwa tunamuunga mkono katika kufikia azma yake hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika kuwatumikia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akishirikiana na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa. Bila shaka viongozi wetu hawa wameonesha uwezo mkubwa katika kuongoza mabadiliko ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo na hekima katika kutekeleza majukumu yao hayo.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba uniruhusu kuchukua nafasi hii ili nikupongeze na kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika, kwa kuendelea kuliongoza vyema Baraza letu Tukufu kwa mashirikiano makubwa na wasaidizi wako na viongozi wote wa Baraza hili. Naomba niwapongeze Wenyeviti wote na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza hili kwa kazi nzuri wanazozifanya za kusimamia utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali. Uangalizi na usimamiaji wao wa karibu wa utendaji wa Wizara na taasisi hizo umeongeza kasi na umakini kwa watendaji wetu katika kutoa huduma bora kwa wananchi. Kwa namna ya pekee namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Konde, Makamu Mwenyekiti Mhe. Panya Ali Abdalla, Mwakilishi wa Viti Maalum na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya mwaka 2017/2018 na kukubali yawasilishwe katika kikao chako hiki kitukufu baada ya kuifanyia kazi miongozo waliyotupatia.

HALI YA SIASA

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ni takriban mwaka mmoja tangu nchi yetu kufanya Uchaguzi Mkuu wa marudio tarehe 20 Machi 2016 ambapo Chama Cha Mapinduzi kiliibuka na ushindi mkubwa. Ndani ya kipindi hicho Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliandaa Taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa Machi, 2016 kama taratibu za uchaguzi za nchi yetu zinavyoelekeza na

ilimkabidhi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo tarehe 9 Febuari, 2017. Aidha, nakala za taarifa hizo tayari zimesambazwa kwa wadau wote wa uchaguzi pamoja na maktaba za taasisi za elimu ya juu. Naomba sana viongozi na wananchi waisome taarifa hiyo ili kuelewa kwa kina shughuli zote za uchaguzi huo na changamoto zilizojitokeza ili kwa pamoja tushirikiane katika kukabiliana na changamoto hizo.

Mhe. Naibu Spika, tangu kumalizika kwa uchaguzi huo kumekuwa na taarifa za kupotosha zinazotolewa na baadhi ya viongozi wa chama cha siasa ambacho kilisusia uchaguzi huo kwamba ama uchaguzi huo utarejewa au mmoja wa viongozi wa chama hicho atakabidhiwa uongozi wa nchi.

Mhe. Naibu Spika,**,** nachukua nafasi hii kusisitiza kuwa uchaguzi huo umekwisha na Dk. Ali Mohamed Shein ndiye Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na panapo majaaliwa yake Mwenyezi Mungu uchaguzi mwengine utakuwa mwaka 2020. Hivyo, Serikali iliyopo madarakani inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015 – 2020. Aidha, natoa wito kwa wananchi kuendeleza hali ya umoja, amani na utulivu iliyopo hivi sasa na tuendelee kufanya shughuli zetu za uzalishaji mali na tuachane kabisa na “hadithi” hizo za alinacha zinazolenga kuturejesha nyuma katika kuwaletea wananchi maendeleo.

HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2016 umeendelea kuimarika ambapo ukuaji halisi ni asilimia 6.8 kutoka asilimia 6.5 ya mwaka 2015. Hali hii ni tofauti na taswira inayojionesha kwa mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo kasi ya ukuaji wa uchumi imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 1.6 kwa mwaka 2016 kutoka wastani wa asilimia 3.4 ya mwaka 2015. Aidha, uchumi wa Kanda ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2016 nao pia umekua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 2.7 kutoka asilimia 3.5 ya mwaka 2015.

Mhe. Naibu Spika, hali hiyo ya ukuaji wa uchumi kwa nchi yetu imepelekea pia kuongezeka kwa Pato la Taifa kwa mwaka 2016 ambalo limeongezeka kufikia thamani ya Shilingi 2,628.4 bilioni ikilinganishwa na thamani ya Shilingi 2,309.5 bilioni mwaka 2015. Vile vile, wastani wa pato la mtu binafsi limeongezeka kufikia Shilingi 1,806,000 kutoka Shilingi 1,633,000 mwaka 2015. Kasi ya mfumko wa bei nayo imefikia wastani wa asilimia 6.7 mwaka

2016 kutoka asilimia 5.7 mwaka 2015 kutokana na mwenendo wa bei za bidhaa za chakula.

MALENGO MAKUU YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, Serikali bado inaendelea na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 ikiwa katika kipindi cha miaka mitano ya mwisho. Aidha, hivi karibuni Serikali imeidhinisha awamu ya tatu ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA III). Hii inamaanisha kwamba malengo yetu bado yanadhamiria utekelezaji wa Mipango huo mikuu ambayo inalenga katika kukuza uchumi, kuimarisha huduma za jamii na kuimarisha demokrasia na utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, Serikali itaendelea kuweka mkazo katika kugharamia uendeshaji wake na kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kutumia rasilimali zilizopo kwa umakini mkubwa na kuhakikisha kuwa matumizi yote yanaleta tija kwa umma. Katika kuwezesha azma ya Serikali itaongeza jitihada kubwa katika ukusanyaji na udhibiti wa uvujaji wa mapato katika maeneo yote.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 maeneo muhimu yatakayopewa kipaumbele katika kutekeleza mpango wa maendeleo ni pamoja na kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, makaazi na upatikanaji wa maji safi na salama. Kuimarisha miundombinu ya uingiaji nchini inayojumuisha bandari na viwanja vya ndege pamoja na kuimarisha miundombinu ya msingi ikiwemo barabara na nishati. Kushajiisha zaidi uwekezaji katika viwanda vidogo vidogo kwa kuongeza thamani bidhaa na ubora wa vifungashio, kuimarisha kilimo, kukuza uwezo wa wataalamu katika fani zenye upungufu mkubwa, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kufanya tafiti zitakazosaidia kutoa maamuzi katika mipango ya maendeleo yetu.

Mhe. Naibu Spika, Serikali tayari imeandaa Sera ya Mafuta na Gesi Asilia na Baraza hili Tukufu limeshatunga Sheria ya kuimarisha masuala ya Mafuta na Gesi Asilia. Kutokana na kukamilika kwa hatua hizo, Serikali imeunda Taasisi ya kusimamia shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na Mkurugenzi Mwendeshaji (MD) wa Taasisi hiyo tayari ameshateuliwa. Hivi karibuni Serikali imekuwa katika utaratibu wa kufanya utafiti wa kubaini maeneo yenye muelekeo wa kuwepo rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia katika kitalu cha Pemba-Zanzibar kupitia kampuni za RAKGAS na BGP.

Mhe. Naibu Spika, katika kuendelea na maandalizi ya kuingia kikamilifu katika sekta hiyo, Serikali kwa msaada wa Shirika la OfD la Norway, imeanza kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani kwa kuwapatia mafunzo maalumu ambayo yatawawezesha kutekeleza kazi zao za kila siku katika sekta hii pamoja na kuwa na uwezo wa kutathmini rasilimali ya mafuta na gesi iliyopo. Ni matumaini yetu kuwa sekta hii itasaidia sana kukuza uchumi wetu na pia kuongeza ajira kwa vijana wetu.

MASUALA MTAMBUKA

Mazingira

Mhe. Naibu Spika, suala la utunzaji wa mazingira linaendelea kuwa na umuhimu katika ustawi wa maisha yetu hasa tukizingatia azma yetu ya kuwa na maendeleo endelevu. Mabadiliko ya Tabianchi bado yamekuwa yakileta athari kubwa katika jamii yetu ikiwemo mmong'onyoko wa fukwe za bahari na uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya makaazi na kilimo. Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kupunguza athari zinazotokana na hali hiyo ili maisha ya wananchi wetu yaendelee bila ya vikwazo. Bado tunaendelea kutoa wito kwa wananchi kuendelea kutunza mazingira yetu hasa misitu ya asili sambamba na kupanda miti kwa wingi maeneo ya wazi ikiwemo fukwe za bahari. Aidha, Serikali inasisitiza sana wananchi kuachana na tabia ya kuharibu mazingira kwa kukata miti ovyo na uchimbaji holela wa rasilimali zisizorejesheka ikiwemo mchanga, kifusi na mawe. Suala la kulinda mazingira siyo la Serikali peke yake bali ni la wananchi pia.

Athari za Mvua za Masika

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu imeshuhudia mvua kubwa za Masika ambazo zinaendelea hadi hivi sasa. Kutokana na hali hiyo, bado tunatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na madhara yanayoweza kujitokeza ikiwemo miripuko ya maradhi yanayosababishwa na uchafuzi wa maji tunayotumia ikiwemo matumbo ya kuharisha na kipindupindu.

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa kwamba mwaka jana (2015/2016) nchi yetu ilikumbwa na maradhi ya kipindupindu ambapo jumla ya wagonjwa 4,330 walilazwa katika vituo 22 vya matibabu vilivyofunguliwa Unguja na Pemba. Wagonjwa 2,652 kati yao walilazwa Unguja na 1,678 walilazwa Pemba. Ingawa mripuko huu uliathiri wilaya na mikoa yote ya Zanzibar, zaidi ya asilimia 75 ya wagonjwa wote walitoka Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na Mkoa wa Kaskazini Pemba. Tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukabiliana na hali hiyo na kufanikiwa kulimaliza gonjwa hilo kabisa.

Nawashukuru sana wataalamu wetu na wote walioshiriki katika operesheni na kukabiliana na maradhi haya.

Mhe. Naibu Spika, wito wangu kwa wananchi ni kuendelea kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wetu wa afya juu ya usafi wa mazingira ikiwemo kunawa mikono mara watokapo chooni na kabla ya kula, tuwache tabia ya kutupa taka ovyo zikiwemo za kinyesi, katika mazingira yetu tunayoishi pamoja na kuchemsha maji ya kunywa au kutia dawa.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa wafanyabiashara wa vyakula nao waendelee kufuata masharti yaliyowekwa juu ya biashara zao kwa kuzingatia suala la usafi na ulinzi wa afya zetu ili kujikinga na maradhi.

Mhe. Naibu Spika, usiku wa kuamkia tarehe 30 April, 2017 tumeshuhudia mvua hizi zikileta athari kubwa kwa wananchi wenzetu wa Mkoa wa Kusini Pemba, hasa katika maeneo ya Chonga, Kilindi na Vitongoji kwa upande wa Wilaya ya Chake Chake na Uweleni, Mbuyuni, Mwambe, Chumbageni, na Ng'ombeni kwa Wilaya ya Mkoani ambao walikumbwa na mafuriko na maporomoko ya ardhi *(land slide)* na kusababisha nyumba nyingi kubomoka na nyengine kufikiwa na udongo. Tukio hilo lilisababisha kifo cha mtoto Rahika Ramadhan Mohamed wa Chanjaani Chake Chake mwenye umri wa miaka 8 aliyofariki baada ya kuangukiwa na ukuta ulioboba maji wa madrassa ya Kur-an.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa mara nyengine tena kwa niaba ya serikali kutoa pole kwa wafiwa na wananchi wote waliopatwa na maafa haya na kuwataka kuwa na subra katika kipindi hichi kigumu. Serikali imefanya tathmini ya kina ili kubaini ukubwa wa taathari iliyojitokeza pamoja na waathirika wa tukio hilo ili kuwasaidia wananchi hao kuweza kurudi katika hali ya maisha yao ya kawaida.

Mhe. Naibu Spika, bado tunaendelea kuwataka wananchi kuepuka kujenga katika maeneo hatarishi ambayo mazingira yake yanaweza kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa hasa wakati mvua kubwa zinazoendelea kunyesha kama vile mabondeni kwenye njia za asili za maji na pembezoni mwa milima hasa Kisiwani Pemba.

Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Naibu Spika, masuala ya watu wenye ulemavu, serikali inaendelea kuchukua juhudi ya dhati katika kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapatiwa fursa na haki katika nchi yetu. Katika kutekeleza azma hiyo serikali itahakikisha kwamba vitendo vya udhalilishaji kwa watu wenye ulemavu katika jamii yetu vinatokomezwa ili wenzetu hawa waweze kuishi bila ya kubaguliwa, kudharauliwa na kudhalilishwa kwa namna yoyote ile. Serikali inaendelea na juhudi za kuwadhibiti na kuwachukuliwa hatua wale wote wanaohusika na vitendo vya ubakaji, upigaji, kuwatelekeza na wanaowaita majina mabaya watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, serikali pia inaendelea na jitihada ya kufuatilia kesi za udhalilishaji za watu wenye ulemavu ili kuhakikisha kuwa kesi hizo zinapatiwa ufumbuzi pamoja na kupatikana kwa ushahidi wa kutosha juu ya udhalilishaji huo. Hivyo naviagiza vyombo vya kusimamia haki na sheria kutimiza wajibu wao ikiwa ni pamoja na kuzishughulikia kesi kwa haraka na kuwapatia haki watu wenye ulemavu ili kulinda utu wao.

Hali ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI

Mhe. Naibu Spika, Tume ya UKIMWI imepewa jukumu na kuratibu muitikio wa taifa wa UKIMWI kuanzia 2016 hadi 2020 unaimarishwa kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za msingi kwa watu wote bila ya unyanyapaa ili kufikia malengo 90-90-90 ifikapo 2020 na kumaliza maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI (VVU) ifikapo mwaka 2030.

Mhe. Naibu Spika, tafsiri halisi ya malengo ya 90-90-90 kwamba asilimia 90 ya watu welioambukizwa VVU wawe wanajitambua kuwa wanaishi na VVU. Asilimia 90 wanaojitambua kuishi na VVU wawe wanatumia dawa za ARVs na asilimia 90 ya watu wanaotumia dawa hizo wawe na idadi ndogo ya VVU mwilini.

Mhe. Naibu Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inajumuika na nchi nyengine duniani kuhakikisha kuwa malengo hayo yanafikiwa ili jamii ya Wazanzibari iweze kuishi bila ya madhara kutokana na maradhi haya.

Mapambano Dhidi ya Madawa ya Kulevya

Mhe. Naibu Spika, suala la uletaji, usambazaji na matumizi ya madawa ya kulevya bado linaendelea kuwa ni tatizo sugu duniani kote ikiwemo Zanzibar na athari zake zimekuwa ni kubwa kwa vijana wetu na jamii kwa ujumla. Hali halisi ya athari ya dawa za kulevya inaonesha kwamba vijana ndio

wanaoathirika zaidi na matumizi ya madawa hayo ambayo ni nguvu kazi ya taifa. Katika kupambana na changamoto hii serikali kwa kushirikiana na wadau wote inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza usafirishaji na usambazaji na matumizi na athari zinazotokana na dawa hizo.

Aidha nachukua fursa hii kuvitaka vyombo vyote vinavyosimamia udhibiti wa dawa za kulevya kufanya kazi zao kwa uwadilifu mkubwa zaidi ili kurahisisha utekelezaji wa mipango ya udhibiti na kutokomeza dawa hizo hapa nchini. Pia nawaomba wananchi wote katika maeneo yao kuwa na Kamati za Kupambana na Dawa za kulevya na tusiwaonee aibu watu wanaofanya biashara hii katika maeneo yetu, tuwafichue na kuwaripoti katika vyombo husika.

Malengo na Utekelezaji wa Kazi za Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Miezi Tisa (Julai -Machi 2016/2017)

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha miezi 9 Julai hadi Machi ya mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na taasisi zake imechukua juhudi kubwa katika kutekeleza malengo iliyojipangia katika programu zake kama ifuatavyo:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamo wa Pili wa Rais (C011)

Mhe. Naibu Spika, Katika mwaka wa fedha 2016/17 Programu hii imetekelezwa na kazi zake kama ifuatavyo:

i. Ofisi imeratibu ziara mbili za kiserikali kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nje ya nchi katika nchi za India, China na Falme za Kiarabu. Ziara ya Nchini India ililenga kukuza na kuendeleza mashirikiano katika sekta ya kilimo, mazao ya biashara na viungo, viwanda vidogo vidogo vya kusindika viungo, uwekezaji na ushirikiano katika sekta ya Afya. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alitembelea jimbo la Kerala, Chennai na mjini New Delhi. Pia, alikagua maeneo ya kilimo, viwanda vya mazao ya kilimo na vifungashio *(packaging)* pamoja na masoko ya bidhaa za kilimo. Vile vile Mhe. Makamo wa Rais alitembelea Hospitali ya MIOT yenye mahusiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupokea wagonjwa kutoka Zanzibar kwa ajili ya uchunguzi wa afya na matibabu. Mheshimiwa pia alifanya ziara katika Kiwanda cha Matrekta cha Mahendra, kuangalia technolojia kuangalia umwagiliaji maji pamoja na kufanya mazungumzo na wafanyabiashara na wawekezaji wa India.

ii. Lengo la ziara la Mhe. Makamo wa Pili wa Rais katika Falme za Nchi za Kiarabu ilikuwa ni kukuza mashirikiano baina ya Zanzibar na nchi hizo katika na uendelezaji wa Sekta ya Mafuta na Gesi, uimarishaji wa usalama katika Viwanja vya Ndege na Bandari na kutathmini maendeleo ya uzanzishwaji wa Afisi mpya ya Mamlaka ya Usafirishaji Zanzibar.

iii. Katika ziara ya China, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ililenga kukuza na kuendeleza mashirikiano katika Sekta ya Miundombinu ikiwemo gati na uwanja wa ndege, uendelezaji wa mfumo wa *e-government, e-health na e-taxing*, Uvuvi wa Bahari Kuu na ukuzaji wa sekta ya utafiti kwa kuimarisha ujenzi wa mahoteli ya kisasa visiwani Zanzibar. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi alikutana na kufanya mazungumzo na Makamo wa Rais wa Benki ya Exim Bank ya China, Uongozi wa *Zhongxing Telecommunication Equipment (ZTE),* Uongozi wa *AVIC International Real Estate Limited,* Uongozi wa *Thernal Bullon Endomentrial Ablator - China, Beijing Construction Company*, Kampuni ya Uvuvi China, *China Habour Construction na Beijing Construction Engineering Group.*

iv. Afisi imeratibu ziara 21 za ndani ya nchi (Unguja, Pemba na Tanzania Bara) za Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

v. Vikao ishirini na nane (28) vimefanyika vya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na Mabalozi wageni mashuhuri kwa ajili ya kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na kibiashara baina ya Zanzibar na nchi, taasisi na mashirika yanayotoka. Aidha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alikutana na mabalozi wapya 14 wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi za Kenya, Uganda, Sudan, China, Korea ya Kusini, Ubelgiji, Qatar, Ufaransa, Uswiss, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Brazil, Italia, Uturuki na Oman.

vi. Afisi imeendelea kushughulikia malalamiko na kera na migogoro ya wananchi yanayohusu masuala ya ardhi nyumba, fidia na kesi za maeneo ya uwekezaji. Jumla ya malalamiko 53 yamepokelewa na kuwasilishwa kwa taasisi zinazohusika na masuala hayo yanayolalamikiwa ili kupatiwa ufumbuzi. Afisi inaendelea kufatilia utatuzi wa malalamiko hayo. Miongoni mwa malalamiko hayo 28 yamepatiwa ufumbuzi na Ofisi imeendelea na kufatilia hatua zinazochukuliwa katika kuyapatia ufumbuzi malalamiko yaliyobakia.

vii. Afisi imefanya matengenezo ya kawaida katika nyumba za makaazi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais za Mazizini Unguna na Dodoma matengenezo hayo yalihusisha uzibaji wa nyufa katika nyumba kuu, marekebisho ya vifaa vya umeme, matengenezo ya jiko na upakaji rangi. Aidha matengenezo

makubwa yamefanyika katika makaazi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Dar-es-Salaam.

viii. Afisi imezipatia thamani mpya nyumba za makaazi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais zilizopo Mazizini Unguja na Dar-es-Salaam. Afisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa ahadi za Mhe. Makamo wa Pili wa Rais katika kusaidia shughuli za maendeleo ya wananchi ikiwemo madawati, katika skuli za Fujoni, Mangapwani, Kitope na Mahonda kufatia mashine ya uchapishaji, *photocopy machine* na *computer* katika Skuli ya Sekondari ya Kitope, Mahonda, Kiwambamvua na Fujoni. Ujengaji wa uingizaji wa vifaa katika maabara katika skuli za Fujoni na Kitope. Ujenzi wa banda la skuli za Mahonda na skuli ya maandalizi ya Kiwambamvua. Kuchangia jumuia ya Siti bint Saad, ZANAB, Ushirika wa Wafuga mbuzi wa Mangapwani na wananchi wa Katavi waliopatwa na maafa. Vile vile kuchangia viyoyozi (AC) katika chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) cha hospitali ya Mnazimmoja na fedha taslim shilingi 45 milioni zilizotolewa kwa wananchi mbali mbali za kusaidia huduma za kijamii.

Program ya Uratib wa Shughuli za Serikali (C012)

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kupitia program hii imetekeleza kazi zifuatazo:

i) Afisi kupitia Kamisheni ya kukabiliana na maafa imeratibu na kutoa misaada ya kibinaadamu kwa waathirika wa majanga au maafa yaliyotokea ambapo jumla ya wananchi wananne (4) Unguja na kumi (10) Pemba wamepatiwa misaada hiyo.

ii) Afisi imeendelea na ujenzi wa kituo cha huduma za mawasiliano ya dharura za kimaafa *Emergency Operation Centre* kilichopo Maruhubi.

iii) Ofisi imefanya tathmini ya hali ya maafa na kutoa mafunzo ya kukabiliana na maafa katika shehia 50 (40 Unguja 10 Pemba). Aidha jumla ya vipindi kumi na nane vya redio na television vinavyoelimisha masuala ya kukabiliana na maafa vimerushwzaa hewani kupitia Shirika la Habari la Zanzibar (ZBC) na radio jamii za Mtegani Makunduchi na Tumbatu.

iv) Ofisi imeraribu ushirika wa viongozi wa wananchi wa Zanzibar katika maadhimisho ya sherehe za miaka 55 ya uhuru wa Tanzania Bara zilizofanyika Dar es Salaam tarehe 9 Disemba, 2017. Aidha, ofisi ilifanikisha ushiriki wa

viongozi na watendaji katika maadhimisho ya siku ya mashujaa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliofanyika mjini Dodoma.

v) Ofisi imeratibu na kushimamia Maadhimisho ya Sherehe za miaka ya Sherehe za miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kusimamia shughuli zote zilizopangwa kutekelezwa katika maadhimisho hayo. Miongoni mwa shughuli hizo ni uwekaji wa mawe ya msingi na ufunguzi wa miradi ya maendeleo katika Wilaya zote za Zanzibar urushaji wa fashfashi na kilele cha sherehe katika uwanja wa Aman. Katika sherehe za miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar jumla ya miradi 19 iliwekewe mawe ya msingi na miradi 32 ilifunguliwa.

vi) Ofisi imeratibu Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa Zanzibar Karume Day ambapo viongozi na wananchi walisoma Hitma na Duwa ya kumuombea Rais wa kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Kwanza wa Baraza la Mapinduzi Sheikh Abeid Aman Karume pamoja na waasisi na viongozi wengine wa Zanzibar waliotangulia mbele ya haki.

vii) Ofisi imekusanya Taarifa za Utekelezaji ya miezi18 ya Ilani ya Uchanguzi wa CCM ya mwaka 2015-2020 kutoka Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

viii) Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa kufatilia marejesho ya matumizi ya fedha ya mwaka 2015/2016 pamoja na kufatilia miradi iliyotekelezwa kupitia fedha za mfuko huo. Ofisi pia imetoa mafunzo juu ya sheria na uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa wajumbe wa Kamati zote za Mfuko huo wakiwemo Wakurugenzi wa Halmashauri zote za Zanzibar ambazo pia ni Makatibu wa Kamati hizo. Vile vile, Ofisi inasimamia malipo kwa kipindi cha Julai - Machi cha mwaka 2016/2017 kwa majimbo 46 ya Unguja na Pemba.

ix) Ofisi inaendelea na uimarishaji wa tovuti ya Serikali kwa kutoa Habari za Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi pamoja na kuendelea kuziunganisha Taasisi za Serikali katika Tovuti hiyo.

x) Ofisi imeratibu utowaji wa vibali 61 kwa watafiti kwa ajili ya kufanya tafiti zilizohusu maeneo ya mazingira, ustawi wa jamii, elimu, historia, maji, ardhi, utalii, uvuvi, vyombo vyaz habari pamoja na uchumi. Ofisi imeratibu kikao cha Kamati ya Kisekta ya Utafiti ya Zanzibar ambacho kilijadili kwa upana mwenendo wa shughuli za utafitin na kupitia maombi mapya ya utafiti yaliyowasilishwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

xi) Ofisi imeratibu na kushiriki katika vikundi katika vikao vya masuala ya muungano ikiwemo Kikao cha Mawaziri wa SMZ na SMT na Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMZ na SMT. Aidha, Ofisi imeratibu na kushiriki vikao kumi (10) vya mashirikiano baina ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

xii) Ofisi imeratibu imeshiriki katika vikao 18 vya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi za Kibalozi za nchi za nje au Mashirika ya Kikanda na Kimataifa.

xiii) Ofisi imeratibu vikao Tisa (9) vya kujadili masuala ya muungano ambavyo vilianza na ngazi ya Wataalamu (Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMZ na SMT), Makatibu Wakuu wa SMZ na SMT, Mawaziri wa SMZ na SMT pamoja na kikao kimoja cha Kamati ya Pamoja ya SMZ na SMT kinachoongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

xiv) Ofisi imesimamia Programu ya TASAF III ambapo malipo kwa kaya masikini yamefanyika katika shehia 204 (126 Unguja na Pemba 78) na jumla ya Shilingi 5,052,368,000 zimelipwa kwa wastani wa kaya masikini 32,700. Aidha, jumla ya Shilingi 397,412,400 zimelipwa kwa Kaya 11,682 katika utekelezaji wa Miradi ya Ajira za Muda kwa Walengwa kupitia Programu hiyo.

xv) Katika kusimamia miradi ya Muungano, Ofisi imefanya ziara ya kutembelea miradi ya Muungano iliyopo Zanzibar ili kuona utekelezaji wa miradi hiyo na changamoto zinazojitokeza ili kuchukua hatua zinazostahiki. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III), Mradi wa Kutengeneza Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mradi wa Kuimarisha Huduma za Mifugo (*ASDPL*), na Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Masoko, Kuongeza Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (*MIVARF*).

xvi) Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huko Dar es Salaam kwa kuhudhuria mikutano 45 ya majadiliano na mashirikiano baina ya Wizara na Taasisi za SMZ na SMT na Taasisi nyengine za Kibalozi na Washirika wa Maendeleo huko Dar es Salaam.

xvii) Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za SMZ Dar es Salaam kwa kuhudhuria mikutano 45 ya majadiliano ya mashirikiano baina ya Wizara na Taasisi za SMZ na SMT na Taasisi nyengine za Kibalozi na Washirika wa Maendeleo huko Dar es Salaam.

xviii) Ofisi imeratibu vikao vitatu (3) vya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu na vikao vitatu vya maafisa waratibu wa masuala ya Watu wenye Ulemavu wa wizara kwa lengo la kujadili changamoto na maendeleo ya Watu wenye Ulemavu.

xix) Ofisi imeratibu Mafunzo kwa vikundi 14 vya Watu wenye Ulemavu katika azma ya Serikali ya kuvijengea uwezo vikundi hivyo ili viweze kuzalisha kwa tija kuweka misingi imara ya kujiari wenyewe. Aidha, wajasiriamali wenye ulemavu wameshiriki katika maonesho ya kibiashara ili kuwajengea uwezo wa kujiamini katika kuzalisha bidhaa bora na kuzitafutia masoko ya ndani na nje ya nchi.

xx) Jumuiya tano (5) za Watu wenye Ulemavu zimepatiwa ruzuku ili ziweze kusaidia katika shughuli zao za kiutendaji.

xxi) Ofisi imefuatilia kesi sita (6) za udhalilishaji wa Watu wenye Ulemavu zilizoripotiwa katika maeneo mbali mbali ya Unguja (5) na Pemba (1) ambazo tayari zimeshapatiwa ufumbuzi.

xxii) Ofisi imewapatia Watu wenye Ulemavu wa Unguja na Pemba visaidizi 234 vikiwemo, fimbo nyeupe, mafuta ya kulainisha ngozi na viti vya magurudumu mawili.

xxiii) Ofisi pia imeendelea kukuza uelewa wa jamii juu ya masuala ya watu wenye ulemavu kwa kurusha vipindi 23 (20 radio na 3 TV) na igizo moja “Talk show” na pamoja na kuendesha mikutano na uhamasishaji wa makundi mbali mbali ya kijamii.

3. Programu ya Usimamizi waShughuli za Upigaji Chapa (C013)

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

Ofisi kupitia Wakala wa Serikali wa Uchapaji imeendelea kutoa huduma za uchapaji kwa kazi zote zilizowasilishwa na Wizara/Taasisi za Serikali na watu binafsi. Miongoni mwa kazi hizo ni Hansard za Baraza la Wawakilishi, Miswada ya Sheria, majarida, mabango ya matangazo, vitabu vya risiti, kalenda za ukutani na za mezani na “Cash books” na “Log books”.

4. Programu ya Mipango na Utawala (C014)

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ofisi imesimamia shughuli za uendeshaji wa Ofisi za kila siku kwa kufanya malipo ya huduma za kiofisi na uendeshaji, kuimarisha huduma za usafiri za ofisi kwa kufanya matengenezo ya vipando (gari na vespa). Vilevile, Ofisi imelifanyia matengenezo jengo la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Vuga ikiwa ni pamoja na kulipaka rangi. Aidha, Ofisi ilitoa mafunzo ya matumizi ya vifaa vya uzimaji moto na kuweka vifaa vya huduma ya kwanza *(first aid kit)* kwa ajili ya dharura.

KUWEKA KANDO KANUNI YA MUDA

Mhe.Naibu Spika: Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kuwa kwa mujibu wa hotuba yetu bado inaonekana kwamba hatutoimaliza ningemuomba Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aongeze muda kwa kutumia Kanuni ili tuweze kumaliza hotuba yetu hii kwa leo mchana. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa na Waheshimiwa Wajumbe muda ulio mbele yetu si rafiki na kwa kuwa bado Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anahitaji muda wa ziada ili kumalizia hotuba yake, hivyo naomba tuweke kando Kanuni ya muda ili tumpe nafasi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kumalizia hotuba yake ya bajeti.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa naomba kutahadharisha tu kwamba kutakuwa na ziada ya dakika 25 tu baada ya hapo nafikiri hotuba inaweza ikaingia katika *hansard* kwa ajili ya kuendelea na hotuba ya mchana.

Sasa niwaulize Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja hiyo aliyoitoa Mhe. Waziri wanyooshe mikono, wanaokataa.Wanaokubali wameshinda.,

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Makamu naomba uendelee.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika,

ii. Ofisi imeratibu na kuandaa makisio ya mishahara na maposho ya watumishi pamoja na Mpango wa Rasilimali Watu wa miaka mitano (5) kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2021/2022. Vilevile, Ofisi imefanya malipo ya baada ya saa za kazi, posho la kukaimu kwa wafanyakazi waliostahiki. Ofisi pia imewalipia wafanyakazi ishirini na mbili (22) ada na gharama nyengine za masomo ya muda mrefu.

iii. Ofisi kupitia Kitengo kinachosimamia Programmu za Kukabiliana na Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu Zanzibar zinazofadhiliwa na Mfuko wa Dunia (*ZGFCCM*) imeendesha vikao vitatu vya kawaida vya robo mwaka na vikao 4 vya dharura vya Kamati vilivyojadili utekelezaji wa shughuli za mfuko huo na kuandaa maombi ya fedha ya mwaka 2018 – 2020 kwa miradi ya Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu. *ZGFCCM* pia imepitisha Mpango Kazi na bajeti yake ya miaka mitatu (2017 – 2019).

iv. Ofisi imeandaa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais za kila mwezi pamoja na taarifa za utekelezaji wa kazi za kawaida na miradi ya maendeleo kwa kila kipindi cha robo mwaka 2016/2017 pamoja na kutayarisha bajeti ya mwaka 2017/2018.

v. Ofisi imefanya ziara ya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na idara na taasisi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Katika ziara hiyo Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Maafa, Programu ya TASAF III, Mradi wa Afya ya Uzazi Mradi wa Kupunguza Madhara Yatokanayo na Matumizi ya Dawa za Kulevya na Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ilikaguliwa na kuona hatua zilizofikiwa za utekelezaji wake ikiwemo mafanikio na changamoto zinazoikabili.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Programu 1: Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali (CO21)

Programu 2: Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi (CO22)
Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Baraza la Wawakilishi kupitia programu hizi limetekeleza yafuatayo:-

i. Afisi ya Baraza la Wawakilishi imeratibu kazi za Kamati zote saba za Kudumu ambapo kamati hizo zilizipitia Taasisi mbali mbali za Serikali na kuwasilisha ripoti zao katika Mkutano wa Tano wa Baraza hili uliofanyika mwezi wa Februari, 2017.

ii. Baraza la Wawakilishi lilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Bunge la Afrika ya Mashariki (*East African Legislature Assembly– EALA*) uliofanyika kuanzia tarehe 10/10/2016 hadi tarehe 20/10/2016. Mkutano huo ulipata baraka ya kuhutubiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein.

iii. Afisi ya Baraza la Wawakilishi iliratibu Mikutano minne (4) ya Baraza la Wawakilishi ambapo katika mikutano hiyo jumla ya miswada kumi na tano (15), Hoja za Wajumbe nne (4) pamoja na ombi la wananchi (*Petition*) moja (1) iliwasilishwa. Aidha, jumla ya maswali 274 ya msingi na 676 ya nyongeza yaliulizwa na kujibiwa.

iv. Afisi ya Baraza iliratibu ziara na mikutano ya viongozi wa Baraza katika nchi za Mauritius, Cuba na Iran ambazo Mhe. Spika aliongoza ujumbe wa baadhi ya Wajumbe wa Baraza na watendaji katika ziara na mikutano hiyo. Miongoni mwa mikutano hiyo ni Mkutano wa Kamati Tendaji ya Umoja wa Jumuiya ya Mabunge (*CPA*) Kanda ya Afrika uliofanyika Dar-es-Salaam, Tanzania. Mkutano ambao ulijumuisha na mikutano mengine kama vile Jumuiya ya Umoja wa Makatibu Mezani (*SoCAT*) uliohudhuriwa na Katibu wa Baraza.

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

Programu 1: Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi

Programu 2: Usimamizi wa Kazi za Utawala za Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

Mhe. Naibu Spika, hadi mwezi wa Machi mwaka wa fedha 2016/2017, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilitekeleza Programu hizo kama ifuatavyo:-

i. Katika kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Ofisi kupitia Tume ya Uchaguzi imeshughulikia mashauri 1,522 juu ya masuala ya wapiga kura ambapo miongoni mwao 298 ni maombi yanayohusu shahada zilizopotea, 335 ni masuala juu ya uhamisho wa wapiga kura, 290 ni masuala yanayohusu masahihisho ya taarifa za wapiga kura na mashauri 599 yanayohusu uchukuaji wa shahada za kupigia kura.

ii. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliendesha Uchaguzi Mdogo katika Wadi ya Ndagoni tarehe 18/2/2017 ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi kutokana na kifo cha aliyekuwa Diwani wa Wadi hiyo, Mhe. Juma Ali Kombo. Jumla ya

Shehia tatu zilihusika katika uchaguzi huo ambazo ni Ndagoni, Wesha na Michungwani. Vyama viwili vya CCM na ADC vilishiriki katika uchaguzi huo ambapo mgombea wa CCM alishinda katika uchaguzi huo kwa asilimia 94.7.

iii. Tume ya Uchaguzi imefanya mapitio ya Daftari la Kudumu la Wapiga kura ambapo jumla ya wapiga kura 6,743 kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba waliopoteza sifa ya kupiga kura wameondolewa katika daftari hilo.

iv. Tume ya Uchaguzi imewasilisha Ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa Oktoba 2015 na Uchaguzi wa Marudio wa Machi, 2016 kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Jumla ya nakala elfu moja na mia moja (1,100) za ripoti hiyo zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau wa uchaguzi wakiwemo Taasisi za Serikali na zisizokuwa za serikali na maktaba za Taasisi za Elimu ya Juu za Zanzibar.

v. Tume ya Uchaguzi imeendelea kutoa elimu ya wapiga kura katika ngazi ya shehia ambapo jumla Masheha na Wajumbe wa Baraza la Masheha wa shehia 132 sawa na asilimia 34 za Unguja na Pemba wamepatiwa elimu hiyo.

vi. Ofisi imewapatia mafunzo wafanyakazi watatu (3) katika ngazi ya Shahada ya Kwanza na ya Pili ili kuleta ufanisi katika kazi zao.

TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Programu 1: Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Programu 2: Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Dawa za Kulevya

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar ilitekeleza Programu hizo kama ifuatavyo:-

i. Kutoa mafunzo juu ya udhibiti wa dawa za kulevya kwa wadau katika shehia zenye bandari rasmi na zisizo rasmi juu ya kuweka wazi mbinu mbali mbali zinazotumiwa na wahalifu katika kupitisha dawa za kulevya. Jumla ya shehia 94 zenye bandari rasmi na zisizo rasmi zilipatiwa mafunzo hayo ambayo yalihusisha washiriki 186.

ii. Kufanya mikutano minne (4) ya Kamati ya Kitaalamu ambayo iliweka na kupanga mikakati ya udhibiti wa dawa za kulevya pamoja na uimarishaji wa kinga dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya.

iii. Kuzisaidia Nyumba za Upataji nafuu (*Sober Houses*) ambapo jumla ya nyumba tisa (9) zimepatiwa ruzuku kwa lengo la kuzijengea mazingira bora ya kazi ili ziweze kukabiliana na changamoto zake.

iv. Ofisi kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti Dawa za Kulevya imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za Dawa za Kulevya ambapo jumla ya vipindi 10 vya redio na vitatu (3) vya TV vilirushwa hewani. Kufanya ziara za utoaji taaluma katika skuli 53 ambapo jumla ya wanafunzi 5,321 (Wanawake 2,834 na Wanaume 2,487) walipatiwa taaluma hiyo . Pia ziara kama hizo zimefanyika katika Shehia 34 za Unguja na Pemba.

v. Ofisi kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilifanya mkutano maalum na wazazi wa vijana walioathirika na dawa za kulevya (*Family therapy*) katika Skuli ya Fujoni. Lengo ni kuwakutanisha wanaotumia na wanaoacha kutumia dawa za kulevya, wazazi, walimu na viongozi wa Shehia ili kuwasaidia vijana hao waweze kujiunga na nyumba za marekebisho ya tabia.

TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Programu 1: Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI(C051)

Programu 2: Utawala na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI(C052)

Mhe. Naibu Spika, kazi za Programu hizi zimetekelezwa na Tume ya UKIMWI kama ifuatavyo:-

i. Ofisi kupitia Tume ya UKIMWI imeandaa mpango wa utekelezaji wa Mkakati wa Tatu wa Taifa wa UKIMWI, Mkakati wa Makundi maalum na mpango wake wa utekelezaji (*Action Plan*), Programu ya Mipira ya Kinga (*condom programming*), Muongozo wa UKIMWI kwa Muitiko wa Jamii (*HIV Guidelines for Community Response*) na Mpango wa UKIMWI wa Vijana.

ii. Ofisi imewapa mafunzo ya uelimishaji rika vijana 60 wenye umri baina ya miaka 10-34 juu ya masuala ya UKIMWI na afya ya uzazi ili wawafundishe vijana wenzao katika shehia 12 zilizoko Wilaya za Kaskazini "A", Unguja na Micheweni Pemba. Vijana hao waliweza kuwafikia vijana wenzao 2,374 ambapo Unguja ni 910 na Pemba 1,464 wakiwemo wanawake 1,040 na wanaume1,334.

iii. Ofisi ilitoa mafunzo kwa wadau 213 juu ya ukondeshaji wa masuala ya UKIMWI na afya ya uzazi katika shughuli zao za kila siku. Jumla ya wafanyakazi 52 wa sekta za serikali, 31 wa asasi za kiraia na viongozi wa dini 130 walipata mafunzo hayo.

iv. Ofisi imeendelea kuratibu programu za makundi maalum ambapo jumla ya watu 1,100 walifikiwa kwa kupatiwa huduma mbali mbali za kinga ikiwemo elimu juu ya UKIMWI na maradhi ya kujamiiana, upatikanaji wa huduma za afya, kuhamasishwa kupima VVU na kuzitumia huduma za tiba kwa wanaoishi na VVU.

v. Ofisi ilisambaza vipeperushi 3,000 na kurusha hewani vipindi 84 vinavyohamasisha masuala ya UKIMWI na afya ya uzazi vilivyorushwa katika redio 4 za jamii (Tumbatu, Makunduchi, Micheweni na Mkanyageni) na *ZBC*, *Hits FM* na *Zenji FM*.

vi. Tume ya UKIMWI imefanya ufuatiliaji kwa taasisi za Serikali na zisizo za Serikali kwa ajili ya kupata taarifa za utekelezaji wa shughuli zao kwa kipindi cha mwaka mmoja (Januari hadi Disemba, 2016) ili kupima utekelezaji wa muitiko wa Taifa dhidi ya UKIMWI na kuandaa ripoti ya pamoja itakayoonyesha hatua zinazochukuliwa na wadau hao katika mapambano dhidi ya maradhi ya UKIMWI.

vii. Ofisi ilitoa mafunzo ya Sheria Nam. 18 ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI ya mwaka 2013 kwa washiriki 163 wakiwemo wataalamu wa afya 55, viongozi wa dini 25, wawakilishi wa sekta za serikali 43 na wasaidizi wa sheria 40. Mafunzo hayo yalitolewa kwa kushirikiana na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar. Aidha, Ofisi imewapa mafunzo wafayakazi 25 wa vituo 7 vya huduma za tiba na vituo rafiki juu ya ujumuishaji wa huduma za UKIMWI na afya ya uzazi katika vituo vyao.

viii. Ofisi imefanya mikutano 8 ya kuratibu muitiko wa UKIMWI kwa sekta za Serikali, asasi za kiraia, taasisi za kidini na taasisi zinazofanya kazi na makundi maalum.

UTEKELEZAJI KIFEDHA

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Programu zake 12 na Programu Ndogo 24 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 26,142,549,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2017 imetumia shilingi 16,934,374,410 ambazo ni sawa na asilimia 65. Ofisi pia iliidhimishiwa jumla ya shilingi 9,849,526,000 kwa kazi za maendeleo na hadi kufika Machi, 2017 imetipatiwa shilingi 7,472,505,100 ambazo ni sawa na asilimia 76 *(Angalia Kiambatanisho Nam. 1 na 2).*

Mhe. Naibu Spika, Ofisi vilevile imekusanya shilingi 516,950,772 ambayo ni…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Makamu wa Pili naomba sasa uingie kwenye hitimisho pamoja na kuomba kutoa hoja kwa ajili ya kuomba fedha ambazo zimekasimiwa humu ili mengine yatabakia kwenye *hansard*.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba sasa hotuba yangu iliyoko kuanzia ukurasa wa 19 kwa hii mliyonayo kwenye vitabu vyenu hadi 85 iingizwe kwenye *hansard* kama ilivyo kwenye kitabu cha hotuba.

…asilimia 68 ya Shilingi 806,126,000 ilizopangiwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 *(Angalia Kiambatanisho nam.3).*

BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na taasisi zake kwa mwaka 2017/2018 itaendelea kusimamia na kutekeleza programu kuu kumi na mbili (12) na programu ndogo ishirini na nne (24). Kupitia Programu hizo, Ofisi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Programu ya kwanza: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais (C011)

Mhe. Naibu Spika, lengo la Program hii ni kuimarisha utendaji wa kazi kwa Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais. Matarajio ya muda mrefu ni kuimarika kwa Ofisi hii na kutoa huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi kupitia Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais imepanga kufanya yafuatayo:

a) Kuratibu ziara 40 za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais za ndani ya nchi na ziara mbili (2) za nje ya nchi;

b) Kuimarisha mashirikiano na mahusiano mema ya Kitaifa na Kimataifa kwa kukutana na Mabalozi pamoja na Wageni Mashuhuri;

c) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais zinazolenga kuleta maendeleo katika jamii;

d) Kuyafanyia kazi malalamiko, migogoro na kero za wananchi kwa kushirikiana na taasisi husika;

e) Kufanya matengenezo makubwa katika makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais yalioko Dodoma na kufanya matengenezo ya kawaida katika makaazi ya Dar-es-Salaam na Zanzibar;

f) Kuendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi sita (6) wa Ofisi ya Faragha kwa kiwango cha Stashahada na Cheti pamoja na kuwapatia stahiki za likizo wafanyakazi.

Programu ya Pili: Uratibu wa shughuli za Serikali (C012)
Mhe. Naibu Spika, programu hii lengo lake kubwa ni kuweka mfumo imara na endelevu kwa Uratibu wa Shughuli za Serikali, ambapo matarajio ya muda mrefu ni kutoa huduma bora za Serikali kwa jamii.

Programu hii ina programu ndogo tano ambazo ni: -

i. Kukabiliana na Maafa
ii. Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa
iii. Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano.
iv. Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dar es Salaam
v. Usimamizi wa masuala ya Watu wenye Ulemavu

Programu ndogo C0121 Kukabiliana na Maafa
Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina lengo la kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa kabla na baada ya

kutokea. Huduma ambazo zinazotarajiwa kutolewa ni Uratibu wa shughuli za Kukabiliana na Maafa ikiwemo kutoa mafunzo kwa jamii, kuwahudumia waathirika wa majanga na maafa pamoja na kuandaa na kutoa miongozo inayosimamia utekelezaji wa kazi za maafa.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Programu ndogo (C0121) imepanga kufanya yafuatayo:

a) Kuanzisha Mfumo wa Tahadhari za Mapema pamoja na kuimarisha Mfumo wa Mawasiliano Wakati wa Dharura;
b) Kutayarisha na kurusha vipindi vya Redio 20 na Televisheni 12 vya kujiandaa na kukabiliana na maafa;
c) Kununua vifaa vya huduma za kibinadamu Unguja na Pemba;
d) Kuainisha maeneo yaliyo katika hatari ya kukumbwa na majanga/ maafa baharini na nchi kavu;
e) Kuratibu shughuli za uokozi na utoaji wa huduma za kibinadamu;
f) Kufanya tathmini kwa jamii juu ya uelewa wa masuala mbali mbali ya kukabiliana na maafa;
g) Kuandaa midahalo na makongamano kwa wanafunzi wa Skuli za Sekondari na Vyuo Vikuu kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kukabiliana na maafa;
h) Kufanya ukaguzi wa majengo yanayotoa huduma kwa jamii juu ya uzingatiaji wa kujikinga na kukabiliana na majanga/maafa;
i) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi wawili (2) wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa.

Programu ndogo C0122: Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa ina lengo la kuwa na sherehe zenye hadhi na kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa shughuli za sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na kuwaenzi viongozi wa kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Programu ndogo (C0122) imepanga kufanya yafuatayo:

a) Kuandaa mazingira mazuri ya Ofisi na utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi na kuendelea kulipia gharama za masomo kwa wafanyakazi watatu (3);
b) Kuratibu Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 54 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar;
c) Kuratibu Hitma na Dua ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume pamoja na viongozi wengine waliotangulia mbele ya haki;
d) Kuratibu ushiriki wa viongozi na wananchi wa Zanzibar katika maadhimisho na sherehe za kitaifa zitakazofanyika nje ya Zanzibar;
e) Kuliyafanyia matengenezo eneo lililopo kaburi la Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume lililopo Kisiwandui na eneo lililopo kaburi la Marehemu Dk. Omar Ali Juma lililopo Wawi, Pemba;
f) Kuendelea kuchangia katika mapato ya Serikali kwa ukodishaji wa vifaa vya sherehe.

Programu ndogo (C0123): Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano (C0123) imepanga kufanya yafuatayo:-

a) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya 2015 – 2020;
b) Kuratibu shughuli za Muungano na Miradi ya Muungano ndani ya Zanzibar;
c) Kuratibu vikao vya Mashirikiano kati ya Wizara na Taasisi za SMZ na SMT;
d) Kuratibu shughuli za utafiti nchini;
e) Kuratibu, kusimamia na kuendesha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;
f) Kuratibu shughuli za Serikali katika ngazi za Taifa, Mikoa na Wilaya ikiwemo uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kusaidia kuyatafutia ufumbuzi malalamiko ya wananchi;
g) Kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Zanzibar kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (*TASAF III*);
h) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi watatu (3) wa Idara.

Programu Ndogo C0124: Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dar es Salaam

Mh. Naibu Spika, Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dar es Salaam ina lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano kati ya Taasisi/Wizara za SMZ na SMT, Washirika wa Maendeleo, Ofisi za Kibalozi na asasi nyengine za kimataifa.
Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi kupitia Programu ndogo CO124 imepanga kufanya yafuatayo:-

a) Kuratibu utekelezaji wa shughuli za SMZ zilizopangwa kufanyika Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na kuziwakilisha Taasisi na Wizara za SMZ katika mikutano na vikao na kuratibu na kushiriki ziara za Wizara na Taasisi za SMZ Tanzania Bara;
b) Kuratibu mashirikiano baina ya Wizara/Taasisi za SMZ na SMT, Ofisi za Kibalozi na Taasisi za Kimataifa;
c) Kuweka mazingira mazuri ya kazi za ofisi kwa kuhakikisha upatikanaji wa maslahi ya wafanyakazi, vifaa na huduma muhimu za kiofisi;
d) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wawili (2) ili kuwaongezea utaalamu;
e) Kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na ofisi za kibalozi na mashirika ya Kimataifa ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

Programu Ndogo C0125: Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu lengo lake kuu ni kuhakikisha kuwa haki na fursa kwa Watu wenye Ulemavu zinapatikana bila ya vikwazo. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Programu ndogo hii imepanga kutekeleza yafuatayo:-

a) Kufanya mapitio ya usajili wa Watu wenye Ulemavu katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na Mkoa wa Kaskazini Pemba;
b) Kusimamia upatikanaji haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu;
c) Kuratibu ukondoishwaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu na kuwajengea uwezo Watu wenye Ulemavu pamoja na taasisi zao;
d) Kufanya uhamasishaji wa jamii juu ya masuala ya Watu wenye Ulemavu;
e) Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Programu ya Tatu: Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa (C01

Mhe. Naibu Spika, Programu hii lengo lake ni kukiimarisha Kiwanda cha Upigaji Chapa cha Serikali ili kutoa huduma bora za machapisho na kwa ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kutekeleza yafuatayo:

a) Kutoa huduma za machapisho ya Gazeti Rasmi la Serikali, Miswaada ya Sheria, Sheria na Nyaraka mbali mbali za Serikali;
b) Kutoa machapisho mbalimbali na huduma ya kuuza vifaa vya ofisini na kuandikia kwa taasisi/Wizara za Serikali na sekta binafsi yatakayokidhi mahitaji ya uchapishaji na kukuza mapato ya Wakala;
c) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wanne (4) Wakala Serikali wa Uchapaji pamoja na kuwapatia stahiki zao;
d) Kuimarisha ubora wa mitambo ya uchapaji kwa kuiweka katika mazingira mazuri na kuifanyia matengezo ya mara kwa mara kila itakapohitajika;
e) Kufanya utafiti kwa ajili ya kuimarisha ufanisi wa machapisho na ukuzaji wa soko la uchapaji ndani na nje ya nchi.

Programu ya Nne: Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (C014)

Mhe. Naibu Spika, lengo la Programu hii ni kuimarisha mazingira bora ya wafanyakazi, usimamizi wa mipango na shughuli za Ofisi. Matokeo yanayotarajiwa ni kuimarika mipango na utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wafanyakazi na wadau mbali mbali wa Ofisi hii. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni: -

i. Uongozi na Utawala
ii. Mipango, Sera na Utafiti
iii. Ofisi Kuu Pemba

Programu ndogo (C0141): Uongozi na Utawala

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Matokeo yanayotarajiwa ni matumizi bora ya rasilimali, wafanyakazi wenye ujuzi na uzoefu ili kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu ndogo ya Uongozi na Utawala imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. Kusimamia shughuli za uendeshaji wa Ofisi za kila siku ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi vikiwemo Kompyuta tatu, mashine ya 'photocopy', vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi, umeme, maji, mawasiliano, mafuta, huduma za usafiri pamoja na matengenezo ya vifaa na vipando;
b. Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wanne (4) wa Idara pamoja na kuratibu mafunzo ya wafanyakazi 37 wa Idara za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na kuratibu kupatiwa mafunzo ya awali (*Induction course*) kwa wafanyakazi wapya;
c. Kufanya semina ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma pamoja na mafunzo yanayohusiana na masuala ya UKIMWI na maradhi yasioambukiza;
d. Kufanya matengenezo madogo madogo ya miundoumbinu ya Ofisi ikiwemo umeme pamoja na njia ya watu wenye mahitaji maalumu katika Jengo la Ofisi, Vuga;
e. Kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani na Kitengo cha Mawasiliano na Habari kwa kuvipatia vitendea kazi.

Programu ndogo (C0142): Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ndogo ina lengo la kuandaa na kusimamia Mipango na Bajeti na kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwa na mipango endelevu na yenye kuleta matokeo bora na endelevu.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Programu ndogo hii imepanga kutekeleza kazi zifuatayo:-

a. Kuandaa Bajeti na kutayarisha Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019;
b. Kufanya ziara nne (4) za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Programu/Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Idara/taasisi zilizomo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
c. Kuratibu na kusimamia tafiti zinazofanywa na Idara na Taasisi zilizomo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
d. Kuratibu Sera, Sheria na Miongozo inayotayarishwa kwa ajili ya shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
e. Kuwajengea uwezo wafanyakazi watatu (3) wa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu;

f. Kusimamia ujenzi wa nyumba ya makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais Pemba;
g. Kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria kupitia Mfuko wa Dunia (*Global Fund*).

Programu ndogo (C0143): Ofisi Kuu Pemba

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Program hii ndogo ni kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba. Matokeo yanayotarajiwa ni utendaji na utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi Kuu Pemba itatekeleza lengo la kuratibu shughuli za Idara na Taasisi zilizomo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba kama ifuatavyo:-

a) Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
b) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 3;
c) Kuandaa mipango ya Ofisi na bajeti kwa mwaka wa Fedha 2018/2019;
d) Kuimarisha kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba;
e) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali Pemba
f) Kutangaza huduma za Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar kwa ajili ya kuongeza idadi ya wateja na mapato;
g) Kuratibu shughuli za kukabiliana na maafa na kutoa elimu kwa jamii juu ya kujikinga na kukabiliana na maafa;
h) Kuratibu shughuli za Watu wenye Ulemavu na kutoa elimu kwa jamii juu ya haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pia inaratibu shughuli za Baraza la Wawakilishi, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Tume ya UKIMWI, ambazo zina Programu Kuu na Programu Ndogo kama ifuatavyo:-

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Wawakilishi linatekeleza Program kuu mbili (2) ambazo ni:

Programu ya tano: Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha haki na utawala wa sheria unatelekelezwa Zanzibar, ambapo matarajio yake ya muda mrefu ni kukua kwa demokrasia na uwakilishi wa wananchi. Huduma zinazotolewa ni kujadili, kurekebisha na kupitisha miswada ya Sheria, kusimamia utendaji wa taasisi za Serikali na kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali.

Programu ya sita: Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi
Mhe. Naibu Spika, Programu hii ina jukumu la kuweka mazingira mazuri ya kazi, kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza, ambapo matarajio yake ya muda mrefu ni kuongezeka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Baraza na Ofisi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Baraza la Wawakilishi kupitia Programu hizi limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Kufanya mikutano minne (4) ya Baraza la Wawakilishi;
b) Kuziwezesha Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kufanya kazi zake kwa ufanisi;
c) Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wa Baraza la Wawakilishi;
d) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Wajumbe ili waweze kutekeleza majukumu yao;
e) Kuendeleza mahusiano na vyombo vyengine vya Mabunge vya Kanda ya Afrika na ngazi za Kitaifa;
f) Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya majengo na Kumbi za Mikutano pamoja na kutoa huduma bora kwa Wajumbe katika kutekeleza majukumu yao ya kikatiba.

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Uchaguzi inasimamia Programu kuu mbili zifuatazo:

Programu ya saba: Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi
Mhe. Naibu Spika, Programu hii ina jukumu la kukuza demokrasia na umoja wa kitaifa ambayo matarajio yake ya muda mrefu ni kuwa na uchaguzi huru na wa haki na wenye kufuata misingi ya kisheria.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kupitia programu hii imepanga kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuandikisha Wapiga Kura wapya waliotimiza sifa za kuandikishwa kuwa wapiga kura;
b) Kuendeleza Daftari la Kudumu wa Wapiga Kura;
c) Kuendelea kutoa elimu ya wapiga kura kwa makundi mbalimbali;
d) Kuimarisha majengo na kufanya michoro ya majengo mapya ya Ofisi za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;
e) Kuendelea Kufanya mapitio ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 kwa kuifuta Sheria hiyo na kuanzisha Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi;
f) Kutoa elimu ya Uchaguzi kwa Wajumbe na Watendaji wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Programu ya nane: Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.
Mhe. Naibu Spika, Programu hii ina jukumu la kuimarisha usimamizi wa mwenendo wa shughuli za uchaguzi, ambayo matarajio yake ya muda mrefu ni uendeshaji bora wa kazi za Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Programu hii inasimamia programu ndogo mbili nazo ni:-

i. Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.
ii. Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi Ndogo ya Tume ya Uchaguzi Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Tume ya Uchaguzi kupitia programu hii imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Kununua vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi za Ofisi.
b) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watano (5) katika ngazi na fani mbalimbali za elimu.
c) Kufanya ununuzi wa gari mbili kwa ajili ya shughuli za Ofisi.

TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ina jukumu kuu la kuratibu mapambano dhidi ya biashara, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya; kutoa taaluma kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya pamoja na tiba na ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa hizo. Taasisi hii imepangiwa kusimamia Program Kuu mbili kama ifuatavyo:

Program ya tisa: Udhibiti wa Dawa za Kulevya
Mhe. Naibu Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii ni:-

a. Kuzijengea uwezo nyumba za upataji nafuu (*sober houses*);
b. Kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya katika bandari rasmi na zisizo rasmi;
c. Kuratibu na kuendeleza mapambano juu ya uingizaji, usambazaji na usafirishaji wa Dawa za Kulevya;
d. Kuangamiza Dawa za Kulevya zilizokamatwa;
e. Kuitisha mikutano ya wadau waliomo kwenye mapambano ya Dawa za Kulevya;
f. Kupunguza matatizo ya athari za utegemezi wa Dawa za Kulevya.

Programu ya kumi: Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya.
Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la programu hii ni kuweka mazingira mazuri ya kazi za ofisi. Huduma zinazotarajiwa ni upatikanaji wa huduma na vitendea kazi, kujenga uwezo wa wafanyakazi na usimamizi wa matumizi ya fedha pamoja na kukuza uwajibikaji. Programu ina program ndogo mbili ambazo ni:

i. Utawala wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya,
ii. Uratibu wa Masuala ya Dawa za Kulevya Pemba.

Mhe. Naibu Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii ni:-

a) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kazi;
b) Kujenga uwezo wa wafanyakazi katika mapambano ya dawa za kulevya;
c) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi wa Tume.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Ukimwi ina jukumu la kuratibu masuala ya UKIMWI hapa Zanzibar, ambapo imepangiwa kusimamia Programu Kuu mbili kama ifuatavyo:

Programu ya kumi na moja: Uratibu wa Muitiko wa Taifa wa UKIMWI
Mhe. Naibu Spika, Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni:

i. Uratibu wa muitiko wa Taifa wa UKIMWI.
ii. Mawasiliano na Utetezi wa Masuala ya UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii ni:

a) Kuandaa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano na Utetezi na nyaraka za Mfuko wa UKIMWI;
b) Kuzisaidia asasi za kiraia kuandaa mapendekezo ya mradi;
c) Kuendelea kutoa elimu juu ya Sheria Nam.18 ya Kukinga na Kusimamia masuala ya UKIMWI ya mwaka 2013 kwa wadau mbalimbali;
d) Kutoa mafunzo ya ukondoeshaji wa masuala ya UKIMWI kwa taasisi mbalimbali;
e) Kutoa uelewa wa Mkakati wa Tatu wa Taifa wa UKIMWI na kuwasilisha matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI wa 2016/17 kwa wadau na kuwajengea uwezo wa namna ya kuyatumia matokeo hayo katika programu zao;
f) Kufanya mijadala ya kuibua mila na mitizamo ya jamii ambavyo ni vikwazo kwa vijana kufikia huduma za kuwakinga na maambukizi ya VVU;
g) Kuhamasisha utekelezaji wa programu za UKIMWI katika shemu za kazi Serikalini na sekta binafsi;
h) Kufanya uhamasishaji na utetezi juu ya hatua za kudhibiti mazingira na tabia hatarishi katika mamlaka za mikoa, wilaya na Shehia na kupitia viongozi wa dini;
i) Kufanya mikutano ya kuratibu muitiko wa taifa wa UKIMWI;
j) Kuuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za UKIMWI;
k) Kutekeleza programu ya makundi maalum, vijana na rika baleghe juu ya UKIMWI na afya ya uzazi;

l) Kutoa elimu kwa njia za vielelezo, redio, tv, tovuti na simu juu ya kupiga vita unyanyapaa wa watu wanaoishi na VVU na kuhamasisha upimaji wa VVU na matumizi ya huduma za tiba.

Program ya kumi na mbili: Utawala na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI
Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la programu hii ni kuweka mazingira mazuri ya kazi za ofisi. Programu hii imepangiwa kusimamia programu ndogo mbili ambazo ni: -

i. Uratibu wa Masuala ya UKIMWI Pemba
ii. Utawala na uendeshaji Unguja.

Mhe. Naibu Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni:

a) Kufanya uratibu wa muitiko wa UKIMWI Pemba;
b) Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi ili kuongeza ufanisi na umakini wa kazi;
c) Kuupitia muongozo wa fedha, kufanya ukaguzi wa kifedha, kusimamia utekelezaji na uwajibikaji wa kifedha;
d) Kulipia huduma, kununua vifaa vya ofisi, pamoja na kufanya matengenezo ya majengo na gari;
e) Kutekeleza programu ya afya kwa wafanyakazi na familia zao.

MGAO WA FEDHA KWA PROGRAMU

Mhe. Naibu Spika, mgao wa fedha kwa Programu kumi na mbili (12) za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake ni kama ifuatavyo:

Programu ya Kwanza: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 1,024,217,282 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Pili: Uratibu wa Shughuli za Serikali. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 5,507,508,060 kwa kazi za kawaida na Shilingi 13,863,777,000 kwa kazi za maendeleo ambapo Shilingi 726,000,000 kwa fedha za SMZ na Shilingi 13,137,777,000 ni mchango wa Wahisani.

Programu ya Tatu: Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 2,068,089,200 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Programu ya Nne: Mipango na Utawala. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi 2,068,774,658 kwa kazi za kawaida na Shilingi 500,000,000 kwa kazi za maendeleo kwa fedha za SMZ.

Programu ya Tano: Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi 6,595,520,000 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Sita: Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi 12,066,180,000 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Saba: Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi. Programu hii fedha zake zinatoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Programu ya Nane: Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi 1, 695,500,000 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Tsa: Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi 151,777,000 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Kumi: Utawala wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi 447,123,000 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Kumi na Moja: Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi 235,044,000 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Kumi na Mbili: Utawala na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi 611,756,000 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya makisio kwa Programu zote 12 za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni Shilingi 44,769,177,000 ambapo Shilingi 30,405,400,000 kwa kazi za kawaida na Shilingi 14,363,777,000 kwa kazi za maendeleo *(Angalia Kiambatisho Nam. 4 na 5)*

UKUSANYAJI MAPATO

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 32,521,000 kupitia kodi ya milango ya maduka na vifaa vya Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.

HITIMISHO

Mhe Naibu Spika, baada ya kueleza hayo sasa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohamed Aboud Mohamed na Naibu Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mihayo Juma Nhunga kwa juhudi zao kubwa wanazozichukua katika kuendelea kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru pia watendaji na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zilizo chini ya ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Joseph Abdallah Meza na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ahmad Kassim Haji kwa juhudi zao katika kutekeleza majukumu yaliyo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na shukurani maalumu kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano, ushauri na maelekezo waliyotupa katika kukamilisha bajeti yetu ya mwaka ujao wa fedha 2017/2018. Aidha, napenda kuwashukuru sana Washirika wa Maendeleo (*Development Patners*) na nchi marafiki ambazo zinaendelea kuchangia katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya ofisi yangu na ya nchi kwa jumla katika mwaka wa fedha 2016/2017. Miongoni mwao ni:-

Benki ya Dunia, *Clinton Foundation*, China, *FAO*, Finland, Norway, India, Japan, Marekani, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu Malaria na UKIMWI (*Global Fund*), Oman, *UNAIDS*, *USAID*, *UNDP*, *UNICEF*, *UNFPA*, *WHO*, *WFP na WIPO*. Vile vile naishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri MKuu kwa ushirikiano wao mkubwa na Ofisi yangu. Pia nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali, Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima kwa kuendelea kuisaidia serikali katika kutoa huduma za jamii na kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana wananchi wangu wote wa Jimbo la Mahonda kwa kuendelea kushirikiana nami katika kutekeleza majukumu yangu

kwao nikiwa Mwakilishi wao katika Baraza hili na katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa nikiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Nawashukuru pia wananchi wote ambao wamefuatilia na kusikiliza hotuba yangu hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya 44,769,177,000 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa ajili ya kutekeleza Programu nilizozieleza hapo awali. Mchanganuo halisi wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

i.	Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	Shilingi	22,964,277,000
ii.	Ofisi ya Baraza la Wawakilishi	Shilingi	18,661,700,000
iii.	Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar	Shilingi	1,695,900,000
iv.	Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya	Shilingi	598,900,000
v.	Tume ya UKIMWI Zanzibar	Shilingi	846,800,000
Jumla		**Shilingi**	**44,769,177,000**

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu umekwisha hivyo naakhirisha kikao hadi jioni saa 11:00 jioni.

(Saa 7:19 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa) Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa viumbe vyote na mwenye kukirimu uhai kwa kila kiumbe ambacho kipo chini ya miliki yake. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutukirimu neema na pumzi ya uhai ambayo inatufanya sisi sote tuliomo ndani ya ukumbi huu wa Baraza na wengineo ambao wapo katika Baraza hili kuendelea kuwepo hapa na kufanya kazi za kusimamia na kuishauri serikali katika masuala mbali mbali ambayo ni yenye manufaa makubwa kwa wananchi wa nchi yetu ya Zanzibar.

Tunakuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu, utuongoze katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa uadilifu na tunakuomba Mwenyezi Mungu umpe nguvu, hekima na busara nyingi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Dkt. Ali Mohammed Shein na viongozi wote wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. (Amin).

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa shukurani ikiwa nitaacha kumshukuru kwa dhati Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuwa mstari wa mbele kwa kuwatumikia wananchi, kwani mara zote yanapotokea maafa au jambo lolote la kitaifa kwa haraka huchukua hatua kuwatembelea ikiwa kwenye furaha au msiba ili kuwafariji wananchi wetu, ikizingatiwa kwamba anaepata au jambo lolote liwe la msiba au furaha pia anahitaji kufarijiwa.

Aidha, nitoe shukurani zangu za dhati na pongezi kubwa kwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kwa utendaji wake wa kazi za kila siku, sambamba na Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mihayo Juma N'hunga, na kuwa kama sehemu ya Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa tangu kuidhinishwa kwa bajeti ya wizara hii, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia Mkutano huu wa Sita ikiwa ni Mkutano wa Pili wa Bajeti na tangu kuanza kwa Baraza hili la Tisa, ambapo serikali inakusudia kupitisha bajeti hii ya mwaka wa fedha 2017/2018. Tumefanya nao kazi bega kwa bega kwa vipindi vyote vya kamati kwa mwaka

mzima bila ya kuchoka na pale inapotokea dharura ya kukosekana kwa ajili ya majukumu mengine ya kitaifa, huwa wanaiarifu kamati yangu na kupanga utaratibu mwengine ambao unaiwezesha kamati hii kufanya kazi bila ya kukosa.

Mhe. Naibu Spika, sitakuwa kiongozi mzuri iwapo nitaanza na kumaliza kusoma maoni haya ya Kamati ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais juu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, kwa kuwapongeza na kuwashukuru watendaji wote wa ofisi hii wakiongozwa na katibu mkuu wa wizara hiyo, kwa kuonesha ushirikiano mkubwa kwa kamati yangu katika kipindi chote cha mwaka wa fedha 2016/2017, wakati kamati yangu ikiendelea na majukumu ya kuisimamia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji bora wa bajeti kwa kuzingatia nidhamu ya matumizi ya fedha kwa mujibu wa sheria.

Aidha, nichukue fursa hii pia kuwapa pole wajumbe na wananchi wote ambao kwa namna moja au nyengine kwa mwaka 2016/2017 walipata misiba mbali mbali, ikiwa ni pamoja na vifo na maafa mengine ya kijamii. Niwaombe wawe ni wenye kustahamili na kukubaliana na mabadiliko yote ya kimaisha yanayoendelea kujitokeza siku hadi siku, kwani mambo haya yote ni maandiko ya Mwenyezi Mungu na kwamba mabadiliko yoyote yanayotokea ikiwa ni furaha au msiba ni sehemu ya maisha ya binadamu ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, nianze kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa muhtasari wa jumla kwa jukumu la msingi la wizara hii ambayo ni kuratibu shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na shughuli zote za Muungano kwa upande wa Zanzibar, ikiwa ni pamoja na miradi ya muungano ndani ya Zanzibar. Aidha, majukumu mengine ya msingi ni pamoja na kusimamia sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuratibu masuala ya kukabiliana na maafa, kusimamia na kuratibu shughuli za upigaji chapa serikalini, shuhuli za watu wenye ulemavu, kusimamia masuala ya UKIMWI, kuratibu na kudhibiti dawa za kulevya, shughuli za uchaguzi na Baraza la Wawaklishi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliomba kuidhinishiwa jumla ya Tsh. 44,767,177,000 ambazo zimetegwa kwa ajili ya shuhuli zake za kawaida na za maenedeleo. Kwa ujumla shughuli zote kwa mwaka wa fedha 2017/2018 zimegawanywa katika makundi au *VOTE* tano, ambazo ni *VOTE* ya *CO1*- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais**,** *VOTE* ya *CO2*- Baraza la Wawaklishi, *VOTE* ya *C03*- Tume ya

Uchaguzi, *VOTE* ya *C04*- Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na *VOTE* ya *C05*-Tume ya UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kunukuu bajeti kwa ujumla kwa kila taasisi iliyo chini ya wizara hii, kwa idhini yako naomba maoni ya kamati yangu yajikite kwa kila taasisi kwa mujibu wa programu, shughuli na huduma zilizopangwa kutekelezwa kwa taasisi husika kama ifuatavyo;-

OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu imepitia fungu baada ya fungu kwa ajili ya kupata ufafanunzi na hatimae kuridhia jumla ya fedha zote ambazo zimeombwa zinakusudia kutekeleza jumla ya programu kuu nne kama inavyoonekana katika hotuba ya wizara. Aidha, lengo la programu kuu zote nne ni pamoja na kuimarisha utendaji wa kazi wa ofisi ya faragha, uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa, kuwa na sherehe zenye hadhi pamoja na kudumisha historia na kumbukumbu za Viongozi Wakuu wa kitaifa, kuimarisha utoaji wa huduma kwa taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara, kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa watu wenye ulemavu, kuimarisha kiwanda cha upigaji chapa ili kutoa huduma bora za machapisho ambazo zitatolewa kwa ufanisi zaidi na kuimarisha mazingira bora ya kufanya kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Unguja na Pemba.

Programu ya Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio taswira ya serikali yetu, pia ni kiungo muhimu sana baina ya serikali na wananchi wake kupitia Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais ambayo, moja ya jukumu lake la msingi ni kushuhulikia na kupokea malalamiko na kutataua matatizo mbali mbali yanayowasilishwa kutoka kwa wananchi. Idara hii ni miongoni mwa idara muhimu na kadri siku zinavyokwenda mbele changamoto kuongezeka kwa malalamiko na migogoro inayowasilishwa inazidi kuongezeka. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 idara hii imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa kutatua migogoro ambayo imeripotiwa kwa asilimia 50 tu. Hii inaashiria kwamba, kumekuwepo na malalamiko ya asilimia 50 ambayo bado hayajafanyiwa kazi au utatuzi wake haujakamilika kwa sababu tofauti. Kamati yangu inashauri idara kupitia programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais, kuongeza jitihada ili kuhakikisha malalamiko ya wananchi yanapata utatuzi kwa muda muwafaka bila ya kuwakwaza, kwani matarajio ni kuona kwamba pale panapotokea migogoro serikali inasimamia na kupatikana kwa haraka ufumbuzi wa matatizo hayo.

Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali

Mhe. Naibu Spika. kupitia programu kuu hii na fedha ambazo wizara inaomba kuidhinishiwa, zinatarajiwa kutumika kutekeleza programu ndogo tano kama zinavyoonekana katika hotuba ya wizara, ni programu ndogo ya kukabiliana na maafa, programu ya sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na kuwaenzi viongozi wakuu wa kitaifa, programu ya kushughulikia shughuli za SMZ na SMT, utafiti wa masuala ya Muungano, programu ndogo ya shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar-Dar-es-Salaam, na programu ndogo ya usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, progamu kuu tano ambazo kila moja zina umuhimu wake kwa nafasi yake na mchango wake ndani ya serikali. Moja ya programu ndogo muhimu ni programu ya kukabiliana na maafa. Pongezi nyingi na za kipekee kutoka kwa kamati yangu ni kwa Idara ya Kukabiliana na Maafa kwa juhudi wanazoendelea kuzichukua kuhakikisha wanawafikia kwa kuwapa huduma za msingi wananchi wote pale wanaopatwa na maafa kwa upande wa Unguja na Pemba. Kamati inashauri kwamba, pamoja na fedha inayotengwa na serikali kwa ajili ya Mfuko huu wa Maafa, lakini ipo haja ya kutafuta wahisani wa nje, wafadhili na wafanya biashara wa ndani, kuchangia Mfuko huu na kuwa na *account* yake maalum kwa ajili ya kukabiliana na maafa au janga pale litakapotokea; tukiamini kwamba janga au maafa yanaweza kutokea wakati wowote hata bila ya kutarajia. Pia kamati inaishauri serikali kununua hata boti za uokozi kwa ajili ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ili inapotokezea ajali ya kuzama kwa vyombo vyetu baharini boti hizo ziweze kutoa huduma hizo za uokozi kwa Unguja na Pemba, ili kuokoa maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, imekua ni kawaida kwa maeneo mengi ya visiwani kukumbwa na mafuriko hususan katika kipindi hiki cha mvua za masika ambayo yanafahamika na idara hii. Kamati yangu inashauri kupitia bajeti hii na programu ya kukabiliana na maafa, ichukue jitihada za kukabiliana na maafa kabla hayajatokea ili kuepusha gharama ambazo sio za lazima na zinazoweza kuepukika, husasan kwa majanga yanayoweza kutabirika kama vile ya mvua kali zinazokwenda sambamba na mafuriko kupitia mfumo wa utoaji wa tahadhari za awali na kuweka hadharani ramani inayoonesha maeneo hatarishi ambayo pia umetajwa kwenye bajeti hii. Lakini pia kamati inawataka wananchi waache tabia ya kujenga kwenye maeneo hatarishi, sambamba na kuacha tabia ya kuziba mitaro inayopitisha maji wakati wa mvua, tunaiomba serikali kuchukua hatua kali dhidi ya watu wanaokataa kufuata utaratibu wa ujenzi na

kuamua kujijengea nyumba kiholela bila ya kufuata utaratibu uliopangwa na wataalamu wa mipango miji.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine katika programu hii ambayo kamati yangu inalipa uzito mkubwa kwa nafasi yake na mazingira ya historia ya Zanzibar na hali ya kisiasa inavyoendelea katika jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni suala la kero ama changamoto za Muungano. Uwepo wa suala la changamoto za Muungano ni suala mtambuka, ambalo kila Mzanzibari analifahamu na kuwepo kwake tangu kuasisiwa kwa muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar. Sisi viongozi tunafahamu jinsi ya Serikali zote mbili yaani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinavyojitahidi kutafuta ufumbuzi wa kero hizo kwa lengo la kuendeleza na kuimarisha muungano na udugu wetu wa asili baina ya maeneo haya mawili, yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Bajeti hii imeweka wazi kuwa, kwa mwaka 2016/2017 jumla ya vikao nane (8), vyenye lengo la kujadili masuala ya muungano vilifanyika na ni imani ya kamati yangu kwamba, kwa kuwa kiasi kikubwa cha vikao hivi vimezaa matunda na mafanikio makubwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini changamoto kubwa ambayo kamati yangu imeibaini, ambayo inawafanya wananchi wahisi kwamba serikali zetu mbili zinacheleweshа kuyapatia ufumbuzi au kutotilia maanani changamoto za muungano, ikiwa ni pamoja na suala zima la wafanyabiashara wa Zanzibar kulipia ushuru mara mbili kwa bidhaa zinazoingizwa nje, jambo ambalo ni kilio kikubwa kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Suala jengine ni upatikanaji wa taarifa kila baada ya muda kuhusiana na mambo yanayohusu Muungano wetu.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wamekuwa wana hamu ya kupata taarifa za mambo ya Muungano kutoka kwa viongozi wetu wenye dhamana ya kushuhulikia changamoto ya Muungano, hususan na hatua au mafanikio ya vikao vinavyofanyika kwa lengo la kutatua changamoto hiyo. Hii ni moja ya sababu inayosababisha kila siku kuzuka kwa taarifa zenye kupotosha ukweli juu ya mambo yanayohusu chanagamoto za muungano, pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na viongozi wetu. Aidha, kwa kuwa leo tunakusudia kujadili matumizi ya Wizara ya nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambayo pia ina dhamana ya kusimamia masuala ya Muungano na imezingatiwa katika bajeti hii. Hivyo ni maoni ya kamati yangu kuwa, katika vikao nane (8) ambavyo vinakusudiwa pia kufanyika kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kuwepo na mfumo maalum wa utoaji wa taarifa kuhusu maendeleo yanayofikiwa katika vikao vinavyokusudiwa kujadiliwa na kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo, kwani kufanya hivyo kutapunguza *propaganda* za wapinzani zenye lengo la kuharibu au kutia doa Muungano wetu.

Mhe. Naibu Spika, programu nyengine ndogo iliyo kwenye progamu kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ambayo kamati yangu imeona nayo ni muhimu kupewa mazingatio ya kipekee, ni juu ya Progamu ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dar-es Salaam. Kwa lugha nyepesi tunaweza kusema kuwa Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ iliyopo Dar-es-Salaam. Hii ndio sura ya serikali yetu kwa upande wa Tanzania Bara, idara hii inafanya jukumu kubwa la kuziunganisha serikali zetu mbili yaani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bila kusahau shughuli zote za kiserikali zinazofanyika Tanzania Bara kwamba zinaratibiwa na ofisi hii.

Mhe. Naibu Spika, imekua ni changamoto ya muda mrefu kwa idara hii kutokana na hali mbaya ya jengo ambalo ni ofisi iliyopo Dar-es-Salaam, kulinganisha na hadhi ya idara yenyewe. Kamati yangu imeliona tatizo hilo, kwani suala hili limekuwa likizungumziwa kwa muda mrefu sasa. Hivyo kamati yangu inaitaka serikali kutafuta namna ya kupata fedha kwa lengo la kulijenga jengo hilo au kulifanyia ukarabati mkubwa ili liendane na hadhi ya ofisi yenyewe, pamoja na mazingira yanazozunguka ofisi hiyo ukizingatia kwamba jengo hilo hutumika kwa Kiongozi wetu Mkuu, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anapokuwa na vikao na Mabalozi wa Nje au viongozi wengine wa kitaifa au wa kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na unyeti wa idara hii na maingiliano yake yanayotokea baina ya watendaji wa idara hiyo na idara nyengine za SMZ na SMT pamoja na viongozi wengine wa kidiplomasia, suala la mafunzo yenye lengo la kuwajengea uwezo watendaji wa ofisi hii ni suala la msingi sana; pamoja na kwamba Bajeti hii imeonesha kuligusia suala la mafunzo japo ni kwa uchache mno. Kamati yangu inashauri mafunzo hayo yazingatie mahitaji ya ofisi hiyo kwa mujibu wa shughuli zake na maingiliano ya shughuli zinazofanyika kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, programu nyengine ambayo kamati yangu inaipa uzito katika bajeti hii ni programu ya kuimarisha ujumuishaji wa watu wenye ulemavu. Suala la msingi katika Idara ya Watu wenye Ulemavu ni dhidi ya udhalilishaji wa kundi hilo la watu wenye mahitaji maalum, suala ambalo siku hadi siku limekua likiongezeka. Bejeti hii inaonesha kwamba, kwa mwaka 2016/2017, hakuna hata lalamiko moja miongoni mwa malalamiko yaliyoripotiwa ambayo yamepata ufumbuzi kamili. Huu ni msiba mkubwa, kutokana na ukweli kwamba, suala la udhalilishaji wa watu wenye mahitaji maalum linaongezeka siku hadi siku. Kamati inashauri serikali kuyafuatilia

kwa karibu sana malalamiko hayo na hatua kali za kisheria zichukuliwe mara moja dhidi ya wale wote watakaobainika kwamba wamejihusisha na tatizo hili la udhalilishaji wa watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, suala hili ni suala mtambuka, kwa lugha linagusa jamii moja ama nyengine na ni kilio cha muda mrefu. Aidha, tatizo hili linachangiwa pia na kutokuwepo kwa kifaa cha upimaji cha *DNA*, ambacho kwa mtazamo wa haraka ndio muarubaini wa udhalilishaji hususan kwa watu wasioweza kujieleza ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu na watoto wadogo. Kamati yangu inafahamu kuwa suala hilo lipo nje ya uwezo wa idara hii, lakini ni imani ya kamati yangu kuwa, serikali inalifahamu na inahitaji suala hilo ilifanyie kazi haraka iwezekanavyo, ili kupunguza tatizo hili la udhalilishaji wa watu wenye ulemavu. Lakini pia kamati yangu inapenda kujua ni lini hasa serikali italeta kipimo hicho cha *DNA* ambacho sio tu kitatua tatizo la watu wenye ulemavu bali mashine hiyo itasaidia katika shughuli mbali mbali za uchunguzi.

Mhe. Naibu Spika, harakati za kuleta usawa wa ujumuishwaji kwa watu wenye ulemavu ni jambo la msingi sana, na mafanikio haya hayatokuja wenyewe, bila ya watu wenye mahitaji maalum kupata jukwaa maalum kupitia Wawakilishi wao, kujadili mambo yanayowahusu na kujiwekea mikakati, juu ya namna gani wanaweza kutatua changamoto zao. Jukwaa pekee kwa sasa ambalo tayari limeanza kufanya kazi katika baadhi ya nchi jirani ni Baraza la Watu wenye ulemavu.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Baraza la watu wenye ulemavu hapa kwetu Zanzibar, halikupata kukaa hata kikao kimoja kati ya vikao vinne (4), vilivyokusudiwa kufanyikwa kwa mwaka husika. Kwa uelewa wa kamati yangu, miongoni mwa sababu zilizopelekea kutofanyika kwa vikao hivyo ni pamoja na ufinyu na ucheleweshwaji wa bajeti kwa idara ya watu wenye ulemavu. Kamati inaiomba serikali kuwapatia fedha zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha, kwa muda muafaka ili kuondoa changamoto za kiutendaji zinazoikabili idara hiyo.

Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Idara ya Watu Wenye Ulemavu kupitia programu ya usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu, imeongezewa bajeti. Kamati yangu inapongeza Wizara kwa kuwaongezea Bajeti, ingawa bado Kamati yangu inaamini bajeti hiyo ni ndogo kwa mujibu wa mahitaji ya Idara hiyo, na uhalisia wa shughuli zake za kila siku.

Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa

Mhe. Naibu Spika, Miongoni mwa mafanikio makubwa ya uwekazaji yaliyofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ni pamoja na uimarishaji wa Kiwanda cha Upigaji Chapa cha Serikali. Kamati yangu inapongeza serikali kwa kuonesha dhamira ya dhati ya kukiboresha kiwanda hicho kwa kiongozea bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Hata hivyo, kamati yangu inashauri na kusisitiza zaidi kuwa ongezeko hilo la bajeti liende sambamba na ukamilishaji wa Bohari Kuu wa kiwanda hicho kinakoelekea, kutahitajika sehemu kubwa kwa ajili ya kuhifadhia machapisho na nyenzo nyengine. Kamati yangu inaipongeza idara ya upigaji chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa kubaini kuwa uzalishaji mkubwa unaokusudiwa kufanyika kwa kutoa huduma za uchapaji, hauwezi kufikiwa bila ya kuwepo jitihada za makusudi za ushajihishaji, suala ambalo nalo pia limezingatiwa katika bajeti hii, kwa kukusudia kufanya matangazo manane (8) tofauti yenye lengo la kushajihisha umma juu ya huduma zinazotolewa na idara hiyo. Kamati yangu inasisitiza zaidi kuwa, kwa kuwa wanaohitaji huduma za uchapishaji ni kutoka matabaka tofauti, basi na matanagzo hayo ya uchapishaji yafanyike sio tu kupitia Televisheni, bali na vyombo vyengine vya habari, ikiwa ni pamoja na magazeti, redio na mitandao ya kijamii kwa lengo la kuwafikia walio wengi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia inazishauri wizara, zote za serikali, kukitumia vyema kiwanda hicho, kwa kupeleka kazi zao hapo na kulipa ada, stahiki na kwa wakati muafaka, ili kukiwezesha kiwanda hicho kukabiliana na ushindani wa kibiashara na viwanda vyengine vya uchapishaji vya Tanzania Bara na vya hapa Zanzibar. Pia Kamati inazitaka zile taasisi zinazodaiwa, zilipe madeni haraka ili kiwanda hicho kiweze kufanya kazi zake ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Tume ya Madawa ya Kulevya

Mhe. Naibu Spika, Suala la madawa ya kulevya ni suala la kitaifa, na vita vyake vinahitaji uzalendao wa hali ya juu kabisa Mhe. Naibu Spika. Bajeti hii kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, imetenga fedha kwa lengo la utekelezaji wa shughuli zote za Tume, kupitia programu kuu mbili ambazo ni pamoja na Programu ya Udhibiti wa dawa za kulevya na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Dawa za Kulevya.

Mhe. Naibu Spika, Bajeti ya Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti wa dawa za Kulevya imeongezeka kwa mwaka 2017/2018. Kamati yangu imekua ikifanya kazi kwa ukaribu na ushirikiano mkubwa na tume hii, hivyo inafahamu changamoto zake ambazo pia zinaambatana na ufinyu wa bajeti. Hivyo basi, kwa ongezeko hili la bajeti, ni imani ya kamati yangu kuwa, Tume hiyo itaweza kutekeleza majukumu yake ya msingi, kwa ufanisi zaidi kulinganisha na mwaka wa fedha unaokwisha.

Mhe. Naibu Spika, Geografia ya Visiwa vyetu vya Zanzibar, kulinganisha na uwezo wa kifedha na nyenzo za kufanyia kazi za Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa dawa za kulevya, inafanya programu ndogo ya kudhibiti na Usambazaji wa Dawa za kulevya izidi kuwa ngumu kwa kile tunachoamini kuwa, sehemu kubwa ya Zanzibar iliyopakana nayo ni bahari na kuwa kila sehemu ya bahari kuna Bandari. Ni ukweli usiofichika kupitia bandari zisizo rasmi, dawa za kulevya zinaweza zikaingizwa na udhibiti wa bandari hizo bado ni mdogo katika utekelezaji wa bajeti hii, ambayo programu ndogo ya kudhibiti Uingizaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya imeongezewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kamati yangu inaamini, chini ya usimamizi mzuri wa Mkurugenzi wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa dawa za Kulevya, programu hii itatekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kuwa vita dhidi ya madawa ya kulevya ni vita ya kitaifa, na inamgusa kila mwananchi, kamati yangu inashauri pia, suala la kuihamasisha jamii juu ya athari ya dawa za kulevya, suala ambalo nalo limetajwa kama moja wapo ya eneo ambalo litafanyiwa kazi na Tume. Kamati inaitaka serikali kulipa kipaumbele cha upekee jambo hilo, kwa lengo la kuwafikia wananchi walio wengi kupitia shehia zao. Sambamba na jitihada binafsi zinazochukuliwa na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa niaba ya kamati yangu napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Mhe. Ayoub Mohammed Mahmoud kwa kuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya dawa za Kulevya. Kamati yangu inaamini kwamba, mapambano hayo ya vita, dhidi ya madawa ya kulevya, tutashinda tu iwapo tutashirikiana kwa pamoja na kuondoa muhali, kwani muhali ni rushwa mbaya sana, na tunatarajia kwamba tutakapofanya hivyo taifa litapiga hatua kubwa sana kwenye mapambano dhidi ya madawa ya kulevya, iwapo miongozo hii tuliotoa tutaitekeleza kwa pamoja.

Mapato

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii imeeleza na kuchambua kwa uwazi kabisa juu ya shughuli zilizopangwa kufanyika, lakini sitakuwa nimetenda haki bila ya

kugusia suala la mapato. Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ni moja wapo ya wizara zenye kukusanya mapato kupitia Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa**.** Kwa kuwa Serikali yetu bado ina uhitaji mkubwa wa kuongeza vyanzo vyake vya mapato na hatimae kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa bajeti. Kamati yangu inashauri**,** Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kutumia fursa zilizopo hapa Zanzibar kupitia huduma zake inazozitoa.

Mhe. Naibu Spika, kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa imetajwa kupata bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa inavyohitaji kwa ajili ya utoaji wa huduma zake kwa aslimia 100% kama inavyotarajiwa pia kwa bajeti ya mwaka 2017/2018. Kamati yangu inashauri idara kuona ukamilifu huu wa bajeti inayoipata, kuwa kama ni fursa ambayo wanaweza kuitumia kwa kujitangaza zaidi, sio tu kwa Taasisi za Serikali, bali hata kwa watu binafsi wenye uhitaji wa huduma zao, na kufanya hivyo kutaiongezea idara mapato na kupata ufanisi zaidi ambao utaimarisha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa ujumla.

Hitmisho

Mhe. Naibu Spika, Kwa kumalizia maoni haya ya kamati yangu kwa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika bila ya kumsahau Katibu wa Baraza la Wawakilishi**,** kwa kuwa nami pamoja na kamati yangu bege kwa bega, kutuongoza na kutushauri, ushauri wenu kwa lengo la kutuongezea ufanisi katika kazi zetu.

Aidha niwashukuru pia watendaji wote wa Afisi ya Baraza, kwa kazi ngumu wanayoifanya kwa kutoa huduma za msingi kwa Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na kuonesha busara na uvumilivu wa hali ya juu kwa lengo la kuhakikisha kwamba kazi za Baraza zinatekelezeka kwa ufanisi na kwa wakati unaostahiki.

Shukurani zangu za pekee ziwaendelee Wajumbe wa Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa kuonesha ushirikiano na uvumilivu, katika kazi zetu za kuisimamia serikali ndani ya kipindi chote cha mwaka wa fedha 2016/2017. Na ni matumaini yangu kuwa, katika kipindi hichi chote Wajumbe wamejifunza mengi na kutengeneza zaidi katika mwaka wa fedha unaofuata.

Mhe. Naibu Spika, Kwa ruhusa naomba sasa niwatambue Wajumbe wote wa kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Omar Seif Abeid	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamo Mwenyekiti.
3.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mjumbe
4.	Mhe. Ame Haji Ali	Mjumbe
5.	Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Mjumbe
6.	Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	Mjumbe
7.	Mhe. Mussa Ali Mussa	Mjumbe

Bila kusahu makatibu wetu wawili ambao ni:-

1.	Ndg. Karima Abdul Wahab	Katibu
2.	Ndg. Kassim Tafana Kassim	Katibu

Mhe. Naibu Spika, Kwa umakini, uchapa kazi na uzalendo wa Wajumbe wa kamati hii, bajeti hii imepitiwa na kuridhiwa, na hatimae kutolewa maoni kwa maeneo ambayo kamati imekubaliana na kuyaoana ya msingi zaidi na yanafaa.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuwasilisha maoni ya kamati yangu kwa ruhusa yako pia naomba na mimi nichangie machache katika hotuba hii ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naendelea tena kumshukuru Mwenyezi Mungu na wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi baada ya kuwasilisha maoni ya kamati, kuwasilisha maoni yangu mimi mwenyewe binafsi yaliyomo katika hotuba tunayoichangia ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kujikita katika hili janga au matatizo ambayo taifa letu sasa hivi yamekutwa ya mvua. Mimi natoa pongezi sana kwa serikali Mhe. Naibu Spika, kwa kukabiliana na kipindi hiki. Kwa sababu leo Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) amezungumza jambo la msingi na pia napenda kuunga na Mwenyekiti ya Ustawi wa Jamii Mhe. Mwinyihaji Makame pale alipotoa maoni yake juu ya athari zinazoweza kujitokeza juu ya mvua zinazoendelea.

Mhe. Naibu Spika, hili halijafikia janga lakini ni athari. Ni athari kama tulivyosema kwenye kamati kwamba tunaweza tukaziepuka athari hizi kwa

sababu Mhe. Naibu Spika, mvua hizi za masika baada ya kumalizika kinaweza kikaibuka kipindu pindu na kipindu pindu kwa wakati mwingi au mara nyingu huwa kinasababishwa na kinyesi kinachosababishwa na njia tafauti, ikiwa moja ni hayo maji. Leo tumeshuhudia kwamba mitaro mingi katika miji yetu ya Unguja na Pemba ima imezibwa au imefukiwa kwa makusudi ni jambo la kusikitisha sana.

Mitaro kama tunavyofahamu Mhe. Naibu Spika, ilijengwa kwa lengo mahususi na ni gharama na serikali inapata gharama kubwa kujenga mitaro hiyo. Lakini si hilo tu kwamba wananchi wamepangiwa utaratibu wa Mipango Miji kuna Idara inayoshughulikia Upimaji na ramani inayotoa maelekezo ya namna gani watu wanaweza kujenga maeneo gani watu wanastahiki kujenga na maeneo gani watu hawastahiki kujenga. Lakini kwa bahati mbaya kabisa Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wananchi hawajali, hawahisi kwamba hili ni tatizo wanalifanyia kwa makusudi. Mfano natoa katika jimbo langu. Mimi mwanzo nilikuwa sijaguswa na mafuriko katika Jimbo langu la Konde lakini ni juzi tu pametokea baadhi ya watu wameiziba mitaro inayopitishia maji jambo ambalo limeleta athari kubwa na baadhi ya nyumba nyingi sasa zimeshaanguka.

Kwa hivyo, naiomba serikali si kwamba kwa jimbo langu tu lakini hata Mhe. Mwinyihaji Makame alilizungumza kwamba kuna mtu ni mfadhili anataka kujenga msikiti lakini uangaliwe ule msikiti je, kweli ule msikiti nini hatima yake, nini faida yake na hasara yake. Tunataka kufanya ibada lakini je madhara yake ni kiasi gani. Mhe. Naibu Spika, na mimi natoa wito tena kwamba suala la ujenzi holela lisipewe nafasi katika nchi yetu kwani tukiliruhusu tunaruhusu matatizo ya makusudi ambayo tunaweza kuyaepuka.

Pia Mhe. Naibu Spika, napenda kuzungumzia kwamba kuhusiana na vijana ambao watapata mafunzo ya utaalamu na tathmini ya mafuta na gesi kwa ushirikiano wa Shirika la OFD la Norway. Mimi ningependa kujua ni vijana wangapi ambao wametapa mafunzo hayo na ni nchi gani wanazopata mafunzo hayo na kwamba serikali ina mpango wa kusomesha vijana wangapi kwa mwaka huu wa fedha kuhusiana na huu mpango wa mafuta na gesi ni vijana wangapi wa Kizanzibari ambao walikusudiwa kusomeshwa na serikali yetu kinyume na huo ufadhili tulioupata sisi serikali tumejipanga kusomesha wanafunzi wangapi vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho nilikuwa napendekeza au natoa wito kwa serikali tumezungumziwa kupewa mafunzo ya kujikinga na maafa kwa kila Shehia ndio nilikuwa naiangalia hapa. Lakini nimeona kwamba kuna Shehia ambazo zimepewa mafunzo 40, 10 Pemba na 30 Unguja.

Mimi nilikuwa naiomba serikali kwamba mafunzo ya kujikinga na majanga ni kitu muhimu sana. Kwa hivyo, yanapotolewa hayo mafunzo yazingatie ni Shehia ngapi wazigawe kwa kila upande na pia isizingatie kwamba ni watu wa aina gani itegemee *gender*.

Kwa sababu kama tulivyozungumza kwamba maafa yanaweza kutokea wakati wowote na zaidi mafunzo haya nilipendekeza yapelekwe kwa wanawake kwa sababu akina mama ndio wanaokaa majumbani, pale yanapotokea maafa au jambo jengine akina mama wawe wepesi wa kuweza kukabiliana na jambo kama hili.

Baada ya haya Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba ya kamati yangu na mimi mwenyewe binafsi ahsante sana nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Sasa mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, atafuata Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf, baada ya hapo atafuata Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kupata nafasi hii ya kuichangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi, ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, nakupongeza kwa kunipa nafasi hii na awali ya yote niseme tu kwamba nampongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya, juu ya kuhakikisha kwamba serikali yetu inakwenda katika mwelekeo unaotakiwa na unaofaa.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika wizara hii nina mambo mawili, matatu lakini yote ni muhimu, lakini nitoyasema na mengine yote nimeyakubali kama yanafaa, tunaamini muda wetu ni mchache hutoyapata yote.

Mhe. Naibu Spika, suala la mwanzo nitazungumzia suala la hali ya uchumi wa Zanzibar. Naipongeza serikali yetu kwa kusimamia vyema hali ya uchumi wa nchi yetu na mapato yanayopatikana tunayashuhudia, lakini kwa juhudi kubwa

za Mhe. Rais na wasaidizi wake kwa kupitia Wizara ya Fedha na taasisi zake, hilo tunalipokea na tunalipongeza kwa dhati kabisa na juhudi hiyo ndio inayotupa uwezo wa kufanya shughuli zetu na kuendelea na ujenzi wetu katika sekta mbali mbali katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza pia Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu hii ni wizara ambayo inakusanya mambo yote au wizara zote, kwa sababu Mhe. Makamu wa Pili ni mtendaji mkuu wa serikali. Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Waziri wa Fedha na watendaji wake kwa juhudi zake na semina mbali mbali anazokwenda nazo ili kuwaelimisha walipa kodi walipe kodi kwa wakati na walipe kodi inayostahiki. Lakini pia wakusanya kodi wakusanye kodi kutokana na majukumu waliyopewa kwa uwezo uliokuwepo kuhakikisha kwamba pato linaingia katika mfuko mkuu wa serikali kuweza kupata mahitaji muhimu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia hivi sasa katika nchi yetu kuna matatizo makubwa yaliyojitokeza, athari za mvua tunazoendelea nazo. Hapa fedha za serikali nyingi zitatumika na fedha hizo ndio zile zinazokusanywa. Kwa hivyo, mimi niiombe serikali tuwe makini katika kukusanya na akiba yetu tunayoipata itatuondolewa adha katika maeneo yetu.

Mhe. Naibu Spika, suala la pili nitazungumzia tena athari za mvua za masika, pamoja na Mhe. Dimwa kutoa hoja binafsi ambayo ni nzuri au taarifa maalum kutokana na hali hii iliyojitokeza katika nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, tukiri kwamba bado serikali naiomba kwa dhati kabisa tuangalie mfumo mzima wa ujenzi katika maeneo yetu, hali ya ujenzi katika maeneo yetu hauko vizuri. Lakini hapo hapo kuna baadhi ya wananchi hawatalaumika italaumika serikali, kwa sababu vibali vya ujenzi vinatolewa na serikali, hivyo tuwaangalie hawa wanaotoa vibali na maeneo yetu ya mazingira yetu katika muundo wa hali ya mji kwa jumla inavyokwenda, au miundo miji sijui inasemekana vipi mimi siwaelewi. Mipango miji ndio wanaoendesha kupanga ujenzi, lakini mipango miji hao hao unakuta unaingia katika madimbwi ambayo sio yao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitasema tu hili wala siogopi, nikipata kura nipate nikiwa sikupata basi. Mhe. Naibu Spika, mimi katika Jimbo langu la Kijitoupele, kuna sehemu ambayo liko daraja la Kijitoupele Meli tano. Hivi sasa naiomba serikali kwa kuwa Mhe. Mkuu wa Mkoa anafanyakazi nzuri katika maeneo ambayo hayastahiki kujenga, na mimi kwangu nampa ruhusa kwa wale waliojenga katika eneo la maji, wamo katikati ya maji katika eneo la Kijitoupele waende wakaliangalie. Yaani nasema sehemu ya Meli tano Mashine ya Maji, upande ule wa Jimbo la Kijitoupele, waangalie watu wamo

ndani ya maji hivi sasa wanaelea na wanaendelea kujenga serikali ipo. Kwa hivyo, wakulaumiwa sio mwakilishi, maana likitokea janga mwakilishi na mbunge kufika ni hati yetu. Lakini je, aliyetoa vibali yuko wapi, naiomba serikali suala hili liangaliwe ili tuondokane na tatizo hili linalotukabili katika nchi yetu. Ujenzi holela ndio unaosababisha maji kutuama katika maeneo.

Mhe. Naibu Spika, naiomba tena serikali, uwezekano wa kuweka mitaro ya maji katika madaraja yetu ya ndani upo, lakini ukosefu wa vyenzo ndio unaosababisha maji hayo kuenea katika maeneo na kuleta hatarishi kwa wananchi wetu. Nazungumza tena, nampongeza Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, pamoja na Mhe. Mbunge aliyepita Mhe. Sereweji walipokuwa mwakilishi na mbunge wa jimbo la Kwerekwe wakati huo, kwa kufanya juhudi kutoka ile njia ya Nyumba mbili, ambapo ndio mkururo kama unakwenda Kwerekwe au wapi unaweza kuchukua nusu saa au zaidi. Lakini kwa uwezo wao walijitahidi daraja lipo, lakini magari ya tani mbali mbali yanapita ni hatari kwa upande mwengine.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba pale pana njia ya ndani ambapo lipo daraja ambalo mbunge Mhe. Shamsi Vuai Nahodha na mwakilishi Mhe. Shihata kwa kupitia na diwani wetu limejengwa zuri tu, lakini ule mtaro wake unatisha. Ndio maana ukenda huko mbele ambako kunaitwa Meli Nne bondeni kabisa, watu wanaelea mpaka sasa hivi. Kwa hivyo, naiomba serikali, nilitoa wito kwa Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Malum katika bajeti iliyopita tufanye ziara twende akaone, hali ni mbaya, inatisha na yule mjumbe wa asubuhi aliyesema hapa kwamba kuna barabara fulani zinajengwa mjini. Sikatai, ukenda Mitiulaya imejengwa, Misufini imejengwa ndio maendeleo. Lakini bahati mbaya serikali haitizami wapi kuna shida, shida ziko katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi A na B. Mimi nachukulia zaidi katika Jimbo langu la Kijitoupele ukianza Nyumbambili mpaka Nyumbamoja huko, au mpaka Jitimai mpya huko, huko hakukaliki mheshimiwa matatizo matupu.

Kwa hivyo, niiombe serikali hebu tuwe na utaratibu maalum wa kufuatilia haya matatizo tusingoje wakati wa maafa. Mhe. Naibu Spika, hakuna kitu kibaya kusema mimi nangojea matibabu tu hutaki kujipima afya yako, hilo ni kosa. Kwanza utizame afya yako ujijuwe uko vipi halafu nenda katika matibabu. Kwa hivyo, naiomba serikali kwa dhati kabisa matatizo yamo.

Mhe. Naibu Spika, hili daraja langu la Kwashunda nalipigia kelele sana, Meli Nne Uzi pamoja na Kwarara huko na Tomondo Uzi huko ni kwahala hatarishi. Naiomba serikali bajeti yetu hii tunayoendelea nayo, lakini tuwe na fungu

maalum la kufuatilia au kamati ya maafa ifanye kazi zake kabla ya kungoja mvua.

Mhe. Naibu Spika, jengine baada ya kutokea hili tu pole tumeshatoa, tulikwenda kutembea tu, lakini ni pole za mdomo tu. Nisemr tu kwamba ningeomba serikali kwa dhati kabisa ikatoa kauli haya yaliyotokea, kwa sababu mtu ukimpa mkono wa pole pia au akisikia salamu zako atashukuru na atasema *Alhamdulillah* nimepongezwa. Tusikae kimya linapotokea tatizo taarifa rasmi itoke ya serikali inawaambia nini wananchi wetu na angalau kuwapa ule mkono wa pole. *(Makofi)*

Jengine Mhe. Naibu Spika, ninalotaka kuzungumza niseme tu kwamba katika serikali yetu kuna mpango mzuri uliowekwa juu ya watu wenye ulemavu. Mhe. Naibu Spika, wizara hii ndio inayohusika naipongeza kwa kuwaendeleza watu wenye ulemavu, lakini ningetoa rai au ningetoa mwelekeo tubadilike Mhe. Naibu Spika, watu wenye ulemavu tunao wengi katika majimbo yetu, lakini naamini wengine hawajulikani wala hawafikiwi. Kama kuna kitengo maalum cha idara hii ya watu wenye ulemavu, basi kiingie katika majimbo tuwatafute wakilishi, wabunge na madiwani, pamoja na masheha wetu orodha kamili zijulikane. Kwa sababu inapotoka riziki yoyote na wao wana haki ya kupata. Lakini naipongeza serikali kwa kutoa fursa nzuri kwenye ajira na kwengineko bila ya kubagua.

Mhe. Naibu Spika, mimi Wizara yangu ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, Wizara ya Habari, Utalii na Michezo. Naipongeza Wizara ya Habari, Utalii na Michezo kwa kukuta kwamba katika sehemu ya sanaa, kuna wafanyakazi wanafika 10 watu wenye ulemavu wasioona. Kwa hivyo, naipongeza wizara, naipongeza idara ya sanaa, nawataka na wengine wajitokeze kuwasaidia wenzetu hawa kwa kuwa uwezo wa kusoma na fani zao zinaelekea na zina uwezo wa kufanyakazi ambapo na wao watapata riziki yao.

Mhe. Naibu Spika, hali ambayo inazungumzwa sana katika nchi yetu ni dawa za kulevya. Mhe. Naibu Spika, nampongeza tena Mhe. Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, lakini naipongeza na jamii kwa jumla katika mikoa mbali mbali. Mkoa wa Mjini Magharibi ndio mkoa ambao ulianza na zoezi hili lisiishie hapa, naiomba serikali mikoa yote ya serikali mitano na wilaya zetu kumi na moja, zifanye kazi hizo kwa mashirikiano. Ukitoka mjini unalikuta Kaskazini, ukitoka Kaskazini unalikuta Kusini Pemba, ukitoka Kusini Pemba unalikuta Kaskazini Pemba, mwisho Kusini Unguja, ili mradi hili suala tupigane nalo liondoke katika nchi yetu. Vijana wetu wanaathirika, vijana wetu wamekuwa hawajielewi, lakini adabu fupi waliyoipata kutoka kwa Mkuu wetu wa Mkoa

wa Mjini Magharibi. Mimi nampongeza Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi na niko pamoja na yeye na niko tayari kuwafichua wale watu wanaotumia madawa katika eneo langu bila ya kuogopa.

Lakini kubwa niseme tu Mhe. Naibu Spika, zoezi hili limeleta manufaa kwa baadhi sio sana, lakini limepunguza kasi. Kwa hivyo, kuna watu wanatumia madawa ya kulevya walikuwa wanatoka, hii nasema tu mfano, wanatoka sehemu ya Mkele kwa Mhe. Hamza, huko pamoja na soko la Mapinduzi pale Mikunguni ndio jirani ninatoka huko huko. Leo ukitoka asubuhi, mimi kama naingia nyumbani nalikuta kundi hili, Mheshimiwa hatujanywa chai, kumbe wamekimbia rungu za kule wanakimbilia huku kwenye amani. Kwa hivyo naomba bado msako huu uendelee katika maeneo yote ili tuondokane na tatizo hili janga la watoto wetu ambao wanapotea na tunawategemea kesho.

Mhe. Naibu Spika, jengine la mwisho baada ya kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu, Wakurugenzi wote na watendaji wote kwa jumla, mimi niseme tu kwamba bado Mheshimiwa ana kazi nzito, kwa sababu yeye ni mkuu wa Shughuli za Serikali tumsaidie kwa hali na mali. Mimi naomba tu linapotokea tatizo lolote, likiwa la maafa, la madawa ya kulevya, watu wenye ulemavu na jenginelo, virusi vya ukimwi ambao watu wetu maskini ya mungu bado wengine wanaathirika na Serikali imejidhatiti kuwasaidia basi tuwaelekeze watu wetu katika maeneo yetu tuwafikikishie matatizo yao katika wizara hii ambayo imekusanya mambo hayo yote kwa ajili ya kuendeleza katika maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache mimi mwenyewe binafsi na kwa hotuba yangu hii asilimia 99 wananchi wangu wananiunga mkono katika Jimbo la Kijitoupele na yote niliyosema waliojenga katika eneo la bonde la daraja la Kijitoupele kuelekea katika Jimbo langu la Kijitoupele wafatiliwe ambao hawana idhini wabomolewe.

Nasema naiunga mkono hutuba hii kwa asilimia mia moja, sina tatizo Mhe. Naibu Spika. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uzima. Lakini la pili nataka kujua dakika ngapi leo thalathini au 25.

Kwanza mimi nitaomba kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato ya mwaka 2017/2018 ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar. Nitaanza na suala la maafa, nitalichangia kidogo tu kwa sababu nishalizungumza pale kwenye

mchango wa Mhe. Mohammed Said Dimwa, suala la maafa naomba sana Idara ya Maafa itapofanya ziara zake basi ije ipite Jimbo langu la Chaani ikaangalie hasa zile sehemu zinazoathiri watu kila mwaka kwenye masuala ya Kipindupindu pamoja na vijiji vitatu vinne vimeathirika na hizi mvua ningeomba sana watapofanya ziara zao basi na Jimbo la Chaani waende eneo la Kikobweni, Lungalunga Chaani, pamoja na Chaani Masingini na Chaani Kubwa maeneo yale wakazunguke waangalie vipi wataweza kuwasaidia wananchi wangu wa Jimbo la Chaani.
Mhe. Naibu Spika, naendelea kwengine kwenye suala la watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu kwa kweli hawapewi *support* sana na wanasahauliwa sana. Ningeomba sana Wizara hii au Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wakawapa sana kipaumbele watu wenye ulemavu kwa ujumla kwenye kitu, wawape *first priority* kuliko hata waheshimiwa. Mfano mdogo tutapofika sehemu basi kama kuna Mheshimiwa na mtu mwenye ulemavu apitishwe mwanzo mtu mwenye ulemavu halafu ndio apitishwe Mheshimiwa. Ikiwa kama kwenye Ofisi, kama kwenye matibabu, kama kwenye gari daladala, sehemu zozote mwanzo apewe *first priority* mtu mwenye ulemavu.

Naomba sana kama wanavyojaaliwa nchi nyengine vitu vingi wanapewa bure, magari wanapanda bure, mahospitali bure, skuli bure na hata kama skuli *private* ambazo za watu basi wapewe nusu bei ili waweze kusoma hata skuli za *private* wakijisikia. Naomba sana serikali ikishirikiana na Waziri wa Elimu wafanye hivi vitu wawape *first priority* hawa watu wenye ulemavu wa aina zote, wapewe mwanzo heshima kuliko waheshimiwa wenyewe. Sisi waheshimiwa tuwe namba 2 watu wenye ulemavu wawe namba moja katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna vifaa vingi watu wenye ulemavu Zanzibar wanavihitaji hawana, kuna miguu ya bandia hawawezi kumiliki, kuna mikono ya bandia hawawezi kumiliki, kuna miwani hawawezi kumiliki, kuna vya kusikia maskioni hawezi kumiliki, pamoja na vitu vingi sana ambavyo wanahitaji hawawezi. Lakini naomba sana Wizara pamoja na Idara husika waweze kuwanunulia hivi vifaa wawaite siku moja mkutano mkubwa ufanyike wa Zanzibar nzima halafu waende na Pemba wakazungumze waangalie nini tatizo lao waweze kuwasaidia kuna watu wanahitaji miguu, wanahitaji mikono mguu mmoja si chini ya laki tisa. Lakini serikali kama itaomba msaada au itafatilia wenyewe kupata nje kwa mujibu wa *order* basi ule mguu uta-*cost* kwenye laki mbili laki mbili na nusu waweze kuwasaidia. Lakini leo mtu anaweza kutembea lakini kwa kuwa mguu tu anao wa bandia hawezi kutembea.

Ninaiomba sana Serikali iwaangalie hawa watu wenye ulemavu wawape *first priority* kwa sababu hali yao ngumu, mabarabarani wanadharauliwa, sehemu ambazo hakuna heshima. Mimi ninachoomba zaidi kwamba kuweko na *fine* kubwa sana kwa mtu yoyote atakayemdharau mtu mwenye ulemavu *fine* kubwa sana na ashtakiwe.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda kwenye suala la Muungano SMZ na SMT. Kuna mambo yanajitokeza kwa kweli yanasikitisha Wizara hii Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ipo inashughulika na masuala ya Muungano, lakini kunatokezea vitu sisi wenyewe Zanzibar tunajiuliza mfano mdogo kauli ya suala la umeme. Kuna suala la *Diplomatic Passport* nimelizungumza, kuna na masuala mengine yanafanyika ninafikiri hata hiyo Idara zenyewe au Serikali yenyewe kuna baadhi ya mambo haijui inashtukizia tu tunafanya nini.

Mimi ninachoomba Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais isiogope, kazi yake kama masuala ya Muungano. Leo *Diplomatic Passport* imetoka amri huko kwamba Wawakilishi, wake zao watoto wao wote wasipewe. Lakini ukiangalia sababu aliyefanya hivyo mtu mwengine aliyepita nyuma. Sasa mimi niulize hawa Wawakilishi walioingia safari hii ni majambazi au wizi hata wasipewe, kwa sababu waliofanya hivyo ni viongozi waliopita huko nyuma na kama wamefanya makosa basi wakachukuliwe hatu. Isiwe amefanya mtu mmoja ndani ya Baraza la Wawakilishi au wamefanya watu watatu ndani ya Bunge la Jamhuri la Muungano ikafanya wote waoze wasiweze kupewa *Diplomatic Passport.* Haiwezekani Mheshimiwa anasafiri akiwa mwanamke akiwa mwanamme yeye mke anasafiri *VIP Diplomatic Counter* anapita mume wake anapitishwa huko pata sote.

Mimi ningeomba sana hili nije nijibiwe. Kama hawawezi kupewa wake zetu na watoto wetu paspoti za *diplomatic* basi hata sisi Wawakilishi tunyan'ganywe tutumie *Ordinary Passport* tuko tayari. Lakini kwa sisi Wawakilishi kwamba labda kaharibu mtu mmoja huko nyuma halafu intoka amri tu kwamba wasipewe, hicho kitu hakiwezekani, *expecially* nyinyi mawaziri. Nyinyi ni watu wakubwa haiwezekani kabisa asipewe mke wenu au mtoto wenu *Diplomatic Passport*. Haiwezekani kabisa kwamba mtu anakaa tu huko anatoa barua hata awe nani madhali sisi Zanzibar tuna Serikali yetu na Jamhuri ya Muungano wana Serikali yao tunatakiwa tulizungumze Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ifanye kazi kwenye suala hili.

Haiwezekani kuna masuala mengine inakuwa kama udhalilishaji. Kama wamefanya watu masuala ya ubadhirifu wakamatwe washtakiwe lakini sisi tuliokuwemo humu tumo safi tupewe *passport*. lakini nitakwenda kwenye kauli

nyengine. Mimi nitaomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akija aje kunijibu atafanya juhudi gani ili *Diplomatic passport* tuzipate kuanzia yeye mwenyewe Mawaziri mpaka Wawakilishi na wale waliofanya yale makosa wachukuliwa hatua isiwe sababu ya kwamba sisi tusipewe kwa sababu ya mtu aliyefanya makosa.

Lakini tukija kwenye suala jengine hilo hilo la Muungano imetoka kauli Mhe. Rais huko nje kwenye ziara umeme uzimwe Zanzibar, hili suala hatuwezi kufika mimi nishajitolea muhanga kama mtu atanifukuza, atanitoa mimi aliyenileta hapa ni Mwenyezi Mungu na wananchi wa Jimbo la Chaani, haiwezekani kabisa tuna Rais, tuna Serikali halafu tunadhalilishwa. Leo Rais yuko huku watu wote taabani wapo waliozimia wenye fikra, wenye biashara tafrani wote umeme Zanzibar unazimwa, halafu anakuja kuinuka Waziri wa Tanzania Bara anasema ati Wazanzibari msiwe na wasiwasi umeme hatukuzimieni tena. asitufanyie masihara bwana sisi tuna akili zetu tunaomba sana masuala kama haya yazungumzwe mwanzo Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano ndio itoke kauli, hichi kitu hatuwezi kwenda hivi mimi nasema kabisa kitakachokuwa na kiwe mimi sijaja hapa kumpapatikia mtu nimekuja hapa kufanya kazi kwa mujibu wa wananchi wa Jimbo la Chaani na Zanzibar nzima. Sasa tukienda kama hivyo Rais wetu anapata vitu haambiwi anaadhirishwa.

Maana yake mimi alivyojibu Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein nampongeza kajibu sawa sawa tutatumia vibatari na mimi niko tayari kutumia kibatari. Lakini kwa mujibu wa kwamba ikalipwe bilioni kumi hii haipendezi kwamba tushaadhirishwa halafu tumelipa bilioni kumi ndio umeme tumebakishiwa hivyo hatwendi. Naomba sana Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati wafanye kazi ya ziada hili suala haiwezekani nchi kama hii ikutwe na deni kama hilo wakati Serikali tunatulipishwa umeme, kodi *infrastructure tax* katika masuala ya kununua umeme halafu unakuta tuna deni kubwa kama hilo hicho kitu *impossible.*

Mhe Naibu Spika, Wizara hii inanunua magari ya kifahari kwenye Shirika la umeme magari yanayopakia nguzo gari la milioni 70 thamanini linapakia nguzo tu za umeme kwenye shirika la umeme. Gari inayokwenda kuchukua fedha anayotumia Mhe. Mohammed Aboud ndio inakwenda kuchukuliwa pesa tu hapo Shirika la Umeme, hatwendi Wizara ina deni kwenye shirika la umeme *failure*, viongozi wa Shirika la umeme wanapeana umeme mkubwa ya nini wapewe umeme? wapewe umeme watendaji wa chini katika Shirika la umeme, wao ndio wanakwenda kupanda nguzo siku za jua na mvua usiku na mchana

ndio wanaohangaika wale ndio wapewe umeme bure sio viongozi wa juu, wanaharibu Wizara ya Ardhi kwenye shirika la umeme wamefeli.

Kama hakutofanyika ubadilishaji wowote hivyo hatutafika matokeo yake ndio hayo lakini kwa upande mwengine tunasoma tunatakiwa tufikirie mbele, tunatakiwa tulete umeme wetu wenyewe tutengeze umeme wenyewe kuna umeme wa jua Zanzibar unafaa. Kuna umeme wa upepo Zanzibar unafaa, kuna umeme wa mawimbi makali Zanzibar unafaa lakini mpaka tunataka tuzimiwe ndio muone. Sasa hivi ndio mmeshasoma na nafikiri mmefahamu leo imekwenda kulipwa bilioni kumi tumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kafanya busara zake lakini mara ya pili utazimwa tu. Na ukizimwa humu ndani tutakuja kufanya vikao bila ya AC kwa vibatari humu ndani tutakuja kufanya hivyo hivyo tutakavyokwenda.

Lakini suala jengine la *TASAF* mimi nataka kuja kujua hajanijibu Mhe. Waziri hizi fedha zilizoletwa za *TASAF* zimefaidisha vipi katika wananchi wa Jimbo langu la Chaani mpaka sasa hivi. Kama zimetumika kwengine na huku kwenye Jimbo langu nije nijue zimetumika vipi. Lakini ukija kwenye hotuba hii hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuna sehemu page 15 Wizara yake karibu vitu vyote kafanyiwa Afisi ya Makamu wa Rais jimboni kwake hakuna hata jimbo jengine lililofanyiwa maendeleo katika nchi hii. Karibu asilimia 90 ya humu ndani kafanyiwa Mhe. Balozi tu kwenye jimbo lake. Hivyo hatwendi, sote tuna majimbo vitu vikifanywa vifanywe kwa niaba ya wananchi wote, ukurasa wa 15 unasema kabisa vitu vilivyofanywa karibu vyote vya jimbo lake vijiji tu tofauti.

Sasa jamani Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mnaona haya mnamuogopa au vipi hata mnamfanyia peke yake, au kama hizi fedha kapewa kwa jina lake tuseme tunataka tufanye hapa kihaki *lillahi* kila jimbo lifanyiwe tunaomba sana, hapa hatukuja kumpendelea mtu. Mimi kila mmoja hapa wangu lakini kwenye kazi sina wangu nazungumza kabisa hapa hii inasikitisha vitu vya maendeleo vyote vimefanyika kwenye jimbo moja isipokuwa ICU tu na hiyo ICU sijui kama haipo huko huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye suala la Polisi, Polisi kwa kweli viongozi wa juu wa Zanzibar tuna Polisi wazuri sana watendaji wazuri sana wasikivu, kuanzia Kamishna, Naibu Kamishna na baadhi ya makamanda wako vizuri. Lakini Polisi *Traffic* kazi yao kusumbua watu hasa njia ya Kaskazini na Kusini, Kaskazini wanakaa na ile tochi ile ya *Speed limit* ile kwenye barabara hakuna bango la *speed limit* lililowekwa lakini wanakamata watu nasikia akishakuwa

na njaa mkubwa mmoja wa Polisi huko Kaskazini huitoa ile camera na huwapa vijana anawaambia kafanyeni kazi muniletee fedha zangu.

Naomba sana sheria ifuate mkondo wake, nchi haijaweka mabango ya *Speed limit* halafu mnamkamata mtu ambae ni mgeni katoka huko hajui hata bango hajaliona halafu mnakuja kumkamata kwamba kwamba kavuka *speed* ule ni udhalilishaji na Polisi natoa wito sana kwa Wizara hii inayohusika na Muungano, mapolisi wa Zanzibar wengi sana sio wote baadhi lakini wengi sana kazi yao kusumbua watu, kukamata wageni bila ya makosa kwa kuwa hawajui sheria na kusumbua baadhi ya Wawakilishi njiani, wanabana tu sehemu *post*, *post* wanazitengeneza wao wanajificha kwenye miti, wanajificha kwenye kona wao wenyewe wanasababisha hatari. Isitoshe zaidi kwamba Polisi hawa saa nyengine wana maneno ya kifedhuli.

Mimi nasema kabisa ndani ya Baraza akija akiniletea Polisi mambo ya kijinga jinga mimi simuachi sijali *uniform* sijali nini, kwa sababu hatutoweza kudhalilishana tunataka tufuate sheria polisi yeye ndio anavunja sheria halafu anakusingizia wewe lazima tufahamu polisi wapewe *discipline*. Polisi viongozi wakubwa tunao, tunahitaji mapolisi ambao wastaarabu ambao wanafanya kazi. Polisi wa Kaskazini na Kusini wametengeneza *Post* wanamkera mgeni anatoka zake *Airport* Zanzibar anakwenda Nungwi atasimamishwa mara kumi na nne sehemu tofauti na hapo atasimamishwa atatoleshwa pesa, ataenda mbele anatoleshwa pesa. Kuna wale boda boda wanaotumia mahonda wale wanamzunguka mtu mbele na mabunduki utafikiri mtu kafanya suala la vita, kumbe wana wasiwasi nae tu hawatumii ustaarabu tunakuomba sana Wizara yako itizame watu wafanye masuala ya ustaarabu. Polisi tunataka sisi wastaarabu kama walivyo viongozi wao wa juu hatutaki mapolisi ambao wazembe wazembe wanafanya mambo wanavyotaka wao.

Lakini nitakwenda kwenye suala jengine la madawa ya kulevya, Mhe. Naibu Spika, madawa ya kulevya Zanzibar hayatokwisha mpaka tutakufa kama hatujaweka sheria ya kifo kwa mtu ambaye analeta unga ndani ya nchi hii au aliyekamatwa na unga. Tusome nchi nyingi sana kwamba zenye kuweka adhabu ya kifo adhabu ya kunyongwa unga umepungua lakini Zanzibar tunawabembeleza, kama Waheshimiwa Wawakilishi hatujaleta sheria ya kuipitisha hapa ya kunyongwa mtu anayeleta madawa ya kulevya au aliyesambaza basi hatutofika kokote tutatumia fedha tutahangaika hakitokuwa kitu, tutoe mfano tunyonge mtu ikiwa kama kuna Mwakilishi humu ndani tumnyonge kama kuna mtu nje tunanyonga huo ndio mfano utakuwa wa mwanzo. Hatuwezi kwenda hivi hivi nchi nyingi zilizofanikiwa adhabu ya kunyonga na naomba sana Wizara yake ije itwambie wakati wa majumuisho

watu wangapi walioleta unga wameshakamatwa ndani ya Zanzibar hadi sasa hivi, na unga uliokamatwa una wingi gani.

Lakini ninachoomba vile vile wale waliokamatwa watumiaji wa madawa ya kulevya waachiliwe wakatibiwe na Serikali sio wawafunge, mtu aliyevuta madawa ya kulevya aachiliwe wampeleke hospitali wakamtibu Serikali afanye maisha yake wasimuweke ndani. Kule ndani katika watu elfu watu 998 ndio wavutaji watu wawili tu, tena ukiuliza utaambiwa kakamatwa na bangi ule unga haumo naomba sana waliokamatwa muwaachie mkawatibu wasiwepo wanazidisha idadi wanataka kufanya maisha.

Mhe. Naibu Spika, hii Wizara kwa kweli mimi nataka saa moja lakini nakwenda mbio mbio kwa sababu najua mara naambiwa dakika hazitoshi, ninachoomba jambo langu jengine Mhe. Naibu Spika, kuhusu Baraza la Wawakilishi mimi nawapongeza wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, nawapongeza wafanyakazi wote kuanzia viongozi Mhe. Spika, Naibu Spika, Mwenyekiti, Katibu wetu jembe na wengine wote kwa kufanya kazi vizuri kwa kutusaidia na naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi hapa tumekuja kufanya kazi, kuna siku tulileta suala la umeme hapa kumepandishwa bei sisi tukasema usipande bei kutokana na mazingira ya wananchi kuna wawakilishi hapa wametugeuka. Sasa sijui wao Waziri vivuli au kwamba hawana uchungu na wananchi au vipi leo suala la ku-*support* wananchi wao ndio wanakuponda wewe mwakilishi mwenzao.

Mimi kwa kweli kuanzia siku ile nimewatoa thamani kwa sababu kazi yao hawaijui na tunachotaka hapa tumekuja kuwatetea wananchi, Shirika la umeme mimi nashangaa mpaka tunafika kuadhirishwa dunia nzima, shirika linaingiza fedha shirika ambalo lina *cash in hand* linapokea pesa *cash* ndio linatoa umeme. Ukitaka nguzo mwananchi unaambiwa lipia nguzo umeme mpaka chini ya nyumba yako mapesa tele nguzo moja laki na thamanini unatoleshwa halafu leo unakuja kuambiwa mabilioni tele yanadaiwa yanadaiwa vipi. Wizara hii ifutwe kama haifai, Shirika la mambo ya umeme iondoshwe iwekwe mpya ndivyo tutakwenda.

Mhe. Naibu Spika, mimi naingia kwenye masuala ya kodi, nchi hii hatutokwenda hata siku moja na hatutokuja juu hata siku moja kama tutaendelea kupandisha kodi kila siku, nchi hii ukiangalia kila miaka hawafikirii kushusha bei wanafikiria kupandisha bei hivi wachumi gani tunawatumia katika masuala ya uchumi wa nchi. Kuna vitu vingi sana tunaweza tukashusha bei na watu ndio watakapokuja zaidi kuwekeza na ndio nchi itakwenda. Lakini nchi hii sijawahi kusikia hata siku moja tumshukuru

Mwenyezi Mungu tumepata Rais Dkt. Ali Mohammed Shein angalau kapandisha hiyo mishahara, lakini mishahara ukiangalia itakuja kufeli kwa sababu mshahara unalipwa laki na nusu kodi ilikuwa iko chini, lakini unakuja pewa laki tatu watu wanapandisha kodi hatuendi kodi kote zimepanda *in-general* nje wazimu mtupu watu wanahangaika. Wafanyabiashara wanalia watu masikini wa chini ndio wameangamia hawana kitu. Tufikirie sana mimi nitakuja kulizungumza hili kwenye Wizara ya Fedha kwa sababu nina *list* ya kuzungumza kipande hichi kirefu tusifike huko.

Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais hivi vitu wahakikishe kuna Wizara hapa kama Wizara ya Ujenzi , Mawasiliano na Usafirishaji, mvua imenyesha sasa hivi unaiona hasa barabara inchi moja lami, inchi moja hii ya kidole kiasi ichimbuke wanadanganya hawasemi ukweli, barabara zinajengwa chini ya viwango barabara mbovu, watu wanakula fedha tu bilioni moja na milioni mia tatu kwa kuweka watu wanaotaka wao. Barabara haiwezekani wanasema tu barabara itachukua tani kumi na tano wakati zilikuwa tani nane, hatuwezi kwenda miundombinu mibovu mvua tupu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli sitaki kuzungumza sana kwa sababu hapa mimi nafahamu utakuja kuambiwa aa hivi vile, lakini nasema tena mimi hapa nimeshazungumza tutakutana mbele, mimi ninachoomba mambo niliyozungumza nije nijibiwe na yote nafikiri yamefahamika na nchi hii iheshimike ina Rais, Makamu wa Pili wa Rais, ina Mawaziri na Wawakilishi majembe kuliko Wabunge. Haiwezekani tufike wakati tusimame masuala ya Muungano tukikuulizeni mutujibu leo Naibu Waziri wa Mawasiliano kachemka, kwenye masuala ya *co-pilot* na mengine anasema aa yako Muungano mimi siwezi kwanza yaachwe wanaamua wenyewe, wanaamua wenyewe kwani sisi tuko kama nani, tuko njugu hapa sisi ni watu. *(Makofi).*

Lazima Wizara ijue Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ijue ishughulikie inabidi leo watu wetu wako tayari kufa huku kwa ajili mapaka yatoke maamuzi kwenye Muungano kwa sababu ya *co-pilot*, lazima ndege zile ziwe na *co-pilot* na *pilot* mwenyewe ili iweze kwenda. Hapa mtakuja kusema huyu bwana si mwenzetu lakini mimi mtakavyofikiria itakuwa ndio hivyo hivyo na mimi najijua Mwakilishi wa Jimbo la Chaani na muda wangu ukisha Mwenyezi Mungu akitaka atanirudisha hajataka najua kuna kheri yangu.

Lakini ninachoomba kwamba Wizara hii ikafanye kazi kwenye masuala ya Muungano Zanzibar isidhalilishwe mimi ndio maneno yangu ya mwisho na naishia hapa Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir Mhe. Abdalla Maulid Diwani ajitayarishe, Mhe. Tatu Mohammed Ussi na baadae atafuata Mhe. Saada Ramadhan Mwenda karibu Mheshimiwa Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, awali ya yote nimshukuru sana muwasilishaji Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri kwa mbwembwe na madaha na ufahamu.

Lakini naomba niende moja kwa moja nisipoteze muda kwa sababu muda wenyewe ni mdogo nakwenda katika ukurasa wa saba suala zima la mtambuka, ikumbukwe kwamba suala la mtambuka linakamata dhana nzima ya mazingira na katika bajeti iliyopita Wizara hii nilishika shilingi katika kadhia nzima ya Mazingira katika eneo la Jang'ombe ya Mshelishelini, ilikuwa siku ya Jumaatatu tarehe 15/5/2016 saa 3.15 hapa usiku, Mheshimiwa Mohammed Aboud akaniomba sana kwa kupembejea na kwa kunisifu kwamba umekuwa mwakilishi mahiri Jang'ombe wamekuchagua hivi na hivi naomba tuachie hili suala tutalifanyia kazi, lakini cha kustaajabisha bajeti inamalizika sasa hivi sijaona kitu.

Nathubutu kutamka tena kwamba sitokuwa tayari tena kupitisha bajeti hii mimi binafsi yangu Abdalla Maulid Diwani muwakilishi wa wananchi kama suala langu zima juu ya kadhia ya mazingira katika Jimbo la Jang'ombe eneo la Mshelishelini sijapata majibu ya kuridhisha. Niko tayari kuzuia shilingi katika fungu hili mpaka Mhe. Mohammed Aboud tena pengine aje anisifu zaidi anipe mbwembwe kubwa zaidi katika suala hili. Sasa hivi tuko katika kadhia nzima ya mvua tunaona mazingira ya pale jinsi yalivyo, lakini tulivyosema ndio tumemaliza ndio yamekwenda basi sawa sawa na machozi ya samaki huyaoni kwenye maji lakini ndio keshasema keshaondoka.

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika suala jengine la madawa ya kulevya, madawa ya kulevya ni ukurasa wa 11 naipongeza sana Serikali katika hili kwa dhana kabisa ya kupiga vita au kuratibu uingiaji na usambazaji wa madawa ya kulevya katika visiwa vya Zanzibar, mpaka kufikia hatua kuweza kwa radhi kabisa kutenga kiasi cha 1.4 bilioni katika ujenzi wa nyumba za kurekebisha tabia kule Kidimni. Lakini cha kustaajabisha na cha kushangaza mpaka katika bajeti hii ambayo tunataka kuipitisha hapa 2017/2018 imeletwa tena inaombewa tena nyumba hiyo hiyo inaombewa shilingi milioni 695. Sasa kule mwanzo ilikuwa 1.4 bilioni nafikiri nyumba sijui ghorofa kumi au ghorofa nane sifahamu ni pesa nyingi lakini ujenzi wenyewe wa nyumba ni wa kawaida tu

haiendani sambamba na matumizi haya 1.4 na leo hii unatuletea ripoti kwamba tukuidhinishie tena milioni 695 nitaomba sana katika fungu hili nije nieleweshwe hasa mpaka nifahamu matumizi ya 1.4 ilikuwaje na mpaka sasa hivi hazijatosha ili tuidhinishe pesa nyengine katika matumizi haya. Najua wana dhana nzuri ya kuzuia uingizaji usambazaji wa madawa ya kulevya lakini je hii thamani yetu ya pesa tunayoitoa ni kweli inatumika kwa lengo au kuna wajanja tu waliokuwa hizi pesa wanafanyia shughuli zao.

Nitaomba sana Mhe. Waziri na sitopenda nionekane mkorofi katika hili lakini nitakuwa mkorofi katika suala hili, kwa sababu nathubutu kusema kwamba japo sitofahamika vizuri mimi Mhe. Abdalla Maulid Diwani si muumini wa busara, hekima na ubinaadamu kwa sababu haya ndio yanayotufikisha hapa, busara hekima kwa binaadamu tunatumia pesa tunaambiwa aa bwana busara binaadamu, binaadamu nimepitikiwa si kweli lazima tuheshimu katiba, kanuni na Sheria ndio vitu vyetu vya kufanyia kazi na vitu vya kupatia maendeleo katika nchi hii. Lakini kila wakati tukiendekeza ubinaadamu hekima busara hatuwezi kufika pesa zetu zinaliwa ovyo watu wanajifaidisha tu wenyewe mwisho wa siku tunakuja kuomba fedha tena hapa, watu wanapiga zogo pesa hamna lakini wachache wanafaidika na pesa zile.

Mhe. Naibu Spika, naendelea katika fungu la C 11.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nimepata malalamiko kwamba wanaosikiliza yaani Mawaziri wanapata shida kusikia kutokana na minong'ono iliyokuwemo ndani humu mingi mno, kwa hivyo nakuombeni sana wale ambao wananong'ona nong'ona wapunguze ili Waheshimiwa wapate kusikia vizuri na kuweza kuleta majibu sahihi. Naomba sana kama watu wanataka kuzungumza bora ata afadhali watoke nje kuliko kuwemo humu kwa sababu wanakera watu wengine. Mhe. Abdalla Maulid Diwani endelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika C11 ibara ya nane, mwenzangu aliyepita alizungumza lakini hapa nina katiba ya Chama cha Mapinduzi ibara ya 18 miko ya uongozi naomba kunukuu. Mwiko wa Kiongozi:

"Kutumia madaraka aliyopewa ama kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume na lengo lililokusudiwa katika madaraka hayo".

Leo tumeletewa kitabu cha bajeti hichi ambapo Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais waliyotekeleza na kwa mbwembwe kabisa walithubutu kuandika kwamba

malengo ya utekelezaji kazi za kawaida za miradi maendeleo katika kipindi cha miezi tisa Julai mpaka Machi, lakini ukienda katika kifungu cha nane ukiangalia miradi yote iliyotekelezwa imetekelezwa katika jimbo la Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Sasa sijui kama kayafanya haya *as* Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda au kafanya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nadhani kafanya Makamu wa Pili ndio maana ikawemo humu. Sasa juu ya mapenzi na jimbo lake juu na nafasi kubwa aliyokuwa nayo, nathubutu kusema kwamba katumia vibaya, katumia vibaya madaraka yake. Kwa sababu pengine ka-*lobby* kawambia Makatibu wake, kawambia Wakurugenzi wake wamemuidhinishia haya kenda kufanya, kila unachokisoma hapa ahadi za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kusaidia shughuli, kusaidia shughuli za maendeleo kwa wananchi zikiwemo madawati Skuli ya Fujoni, Mangapwani, Kitope, kompyuta nyingi tu, sasa sisi majimbo mengine tusiokuwa na watu kama hawa itakuwaje tuoneni huruma, tunatoa pesa nyingi sana hizo hizo ambazo tunazozipata tunajinyima sisi wenyewe kwa ajili ya kuwapelekea maendeleo wananchi kwenye Majimbo yetu.

Majimbo yetu tumefanya lakini tumefanya as Mwakilishi wa Jimbo Mhe. Abdalla Maulid Diwani, tumenunua magari, tumejenga matawi, tumetoa huduma za afya, hatuna nafasi kama ni Waziri, Naibu Waziri namna gani? Sasa inakuwaje Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kutuletea kitabu ambacho yote kimebeba faida mambo ambayo amekuja kujisifu kafanya katika jimbo lake kwa kweli hajatutendea haki katika hicho. Na mimi katika hichi kidogo nitakuwa mtukutu nitaomba sana na nitazuia shilingi katika hili vile vile ili nijue mustakbali ya haya ilikuwaje imepitishwa vipi na nitazuia shilingi kujua kadhia hii.

Yale ndio maana bahati nzuri Katiba yetu ya Chama imetwambia ni mwiko kwa kiongozi kutumia madaraka yake Katiba ya Chama cha Mapinduzi sio maneno ya Abdalla Maulidi Diwani, ni Katiba ya Chama cha Mapinduzi na maelezo ndio yapo hapa nitaomba sana nipate ufafanuzi wa kina juu ya kadhia hii ambayo imeletwa katika kitabu hichi.

Nikenda katika 11(c) kifungu ambacho kinazungumzia C 013 Uchapaji.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa hapa Bajeti iliyopita 2016/2017 alikuja Mheshimiwa akaleta ahadi nyingi sana na tumeisoma naomba kunukuu kidogo Programme Usimamizi wa Uchapaji. Mhe. lengo kuu kuimarisha Kiwanda cha Upigaji Chapa ili kutoa huduma bora machapisho ya ufanisi katika mwaka wa fedha 2016/2017 Programme hizi hapa. Alikuwa na Programme karibuni

nne, lakini cha kushangaza leo hii anakuja kutuletea ufanisi wa kazi, zake ki-*paragraph* kimoja hichi na mambo yaliyokuwemo humu nitaomba kuyanukuu:

“Alizungumza kutoa huduma bora ya uchapishaji, Nyaraka na Sheria za Serikali”. Aje atufafanulie kafikia vipi na kafanya vipi hakuna.

(d) "Kutangaza kushajihisha uwelewa wa utowaji wa huduma za uwakala wa kiwanda hakuna."

Ina maana kaja hapa katwambia tu ofisi kupitia wakala wa uchapishaji imeendelea kutoa huduma uchapaji kazi zilizowasilishwa Wizara, Taasisi kwa kweli haiko sawa, tulitaka angalau haya mambo aliyoyaomba alikuwa ayaoneshe hasa kwa kina kama mwaka jana nilikuja hapa niliomba mlinipa haya, niliomba haya, mlinipa hapa na nikafanya lakini kutwambia leo kwamba kafanya hivi vitu ambavyo ki-*paragraph* kimoja nafikiri sijui nitumie lugha gani ambayo iliyokuwa nzuri haitoudhi lakini ndo tutakwenda hivyo hivyo tutafika.

Kwa kweli hii inastaajabisha lakini si hilo tu hapa hapa Mheshimiwa alikuja akatanabahi pale kasema kwamba kuanzia sasa haitoruhusiwa taasisi yoyote ya Serikali kuchapisha kazi zozote nje ya Ofisi ya Mchapaji Mkuu wa Serikali, cha kushangaza mpaka dakika hii bado watu wanajifanyia mambo yao nje hawachapishi pale na katika hilo mimi nina gazeti hili hapa la tarehe 22 Machi, 2015 Mkurugenzi wa Uchapaji naomba kunukuu Mhe. “Taasisi za Serikali zatakiwa kutumia Wakala wa Uchapishaji” hapa kasema sana Mheshimiwa Mkurugenzi wa Wakala kuziomba kagundua kama kuna Taasisi bado hazijakubali agizo la Serikali kufanya kazi katika Mchapaji Mkuu wa Serikali.

Kulikoni wanakimbia nini, kuna sababu gani, Mheshimiwa unakuja pale unatulabu kwamba una mitambo mizuri, kuna wafanyaji wanye uwezo mbwebwe nyingi sana lakini bado taasisi ambazo mnazozisimamia nyinyi wenyewe bado hazifanyi uchapaji katika taasisi yetu kulikoni. Hata hili gazeti letu tulilolisoma hapa linachapishwa Tanzania Bara. Gazeti lenyewe hili nililolisoma linachapishwa Tanzania Bara. Sasa kulikoni katika hilo lakini ukisoma chini huku anasema ana mpaka wataalamu lakini wachache, alisema anao wataalamu wenye uwezo wa kutumia mitambo iliyopo kwa asilimia 41 huku wakipanga kuajiri wataalamu 22 lakini bado kuna kazi mpaka leo Taasisi za SMZ zinachapisha nje ya Zanzibar au nje ya Taasisi ya Uchapaji ya Serikali katika viwanda vya Waheshimiwa pengine sijui wa namna gani wana *percent* zao hivyo hatuwezi kwenda.

Tunapokuja hapa tunaposimamia ile ahadi lazima tusimamie kweli, isiwe hapa tunasema hivi tukifika nje aa bwana pale nimesema tuleteeni mfanyakazi hatuwezi kufika hivyo na hivyo viwanda vyengine sisi humu humu ndani pengine tunavyo vyetu vinachapisha kazi hizo hizo za serikali. Ukisema mbele unakataza lakini nyuma yake unachukuwa unachapisha tutafika wapi? Kwa kweli tunapata wakati mgumu kuisimamia kwa sababu katika Hotuba hii amezungumza mpaka hii leo wengine ukiwauliza utafanya utafiti wanakwambia kwamba kuchapisha Zanzibar ni gharama kuliko Dar es Salaam sababu moja kulikoni!

Uchapishe kule, ufunge, usafirishe ulete Zanzibar sokoni gharama ndogo kuliko gharama kuchapisha Saateni pale, kwa kweli sifahamu kuna gharama gani ambazo zinaingia mpaka watu washindwe kufanya kazi hiyo katika taasisi yetu. Nitakuomba sana Mheshimiwa Waziri, katika suala hili uje utufahamishe vizuri ili tufahamu zana nzima ya kuboresha Kiwanda chetu hichi cha Uchapaji ili kuona ule mzuguko wa fedha wa Zanzibar unabakia katika sehemu yetu hiyo humu humu ndani.

Niendelee katika Kifungu cha 023 Uratibu wa Shughuli za SMT na SMZ na malalamiko ya wananchi ukurasa wa 38 naomba kuunukuu

“Kuratibu wa shughuli za Serikali kupitia ngazi ya Taifa, Mikoa, Wilaya ikiwemo Uratibu wa ufuatiliaji, utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu, Kitaifa na kusaidia kuyatatulia ufumbuzi malalamiko ya wananchi”.

Serikali kwa dhana kwa nia safi kabisa imeunda kitengo kizuri sana lakini, nathubutu kutamka kwamba hakina meno. Hakina kinachoratibu pengine kinawekwa tu pale ilifika *time* nathubutu kusema mimi ni mjumbe wa Kamati ya *PAC,* tunakwenda kufanya kazi zetu Ofisi nzima ya Uratibu ile gari yeye mwenyewe kama Ofisi ya Mratibu hawana.

Wataratibu nini tunachelewa tunamsubiri mfanyakazi kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, anasema kwamba mimi sina gari ya bwana ya kujia huku nimeazima gari kwa mtu halafu tunasema tunaratibu nitamuomba sana Mheshimiwa Waziri kama kitengo kwenye idara yako kiangalie ukipe usafiri ili kinapohitajika kiweze kufika. Malalamiko yako mengi pengine gari, pengine kwa mapenzi, kwa urafiki Mhe. Naibu Waziri hayupo ndio anatoa gari yake.

Inatiwa SMZ anachukua wafanyakazi aje kufanya nao kazi hawatendei haki, kama kitengo tumekiunda lazima tukiwezeshe. Si hayo tu kuna waratibu muhimu sana na ndio maana pale nikasema mimi si muumini wa busara,

hekima sijui na ubinaadamu leo hii Ofisi hii ya Uratibu imefika *time* kuna baadhi ya Viongozi humu ndani ya SMZ wanafanya mambo hata Ofisi ya Mratibu haina taarifa. Ilitokea kadhia ya uvunjwaji wa nyumba Kianga.

Ofisi ya Uratibu haina taarifa ikiwa yeye ni Mratibu wa Shughuli za Serikali sasa sijui ndio ugatuzi tayari, kwamba watu wamegatua wakafanya haya mambo au kwamba watu kwa nguvu zao tu, nitaomba sana katika hicho. Kuna nyumba zimefunjwa kule sijui kama ndio kwenye eka, ukiangalia kwenye eka nyumba za asimilia watu 60 humu zote ziko kwenye eka. Kwa sababu kuanzia Kwerekwe mpaka Fuoni heka tupu zile ee na watu wamejenga hakuna kilichofanyika.

Lakini si hilo tu, kuna watu wamejenga katika njia kuu za maji, ndio wanasababisha mafuriko haya hatua gani mnachukua mnakwenda kuvunjia watu wamejenga ndani ya eka, tunawaacha watu ambao wanaoharibu jamii kubwa ya watu kuwapa adhabu ya usafiri, kuwapa adhabu pengine chungu nzima, panajaa maji Kwerekwe kwa sababu pengine mtu tu kajenga kwenye njia ya maji kubomoa hatuwezi. Sasa nasema hekima, busara tuwachie hao itakuwa hivi hatuwezi kufika lazima tuangalie Sheria inasemaje ardhi ni mali ya serikali, Serikali ndio hii.

Sasa kwa kulitatua lile suala pale tuone ata tukitatuwa hilo tuvunje hapa, tuvunjeni ili matatizo watu waondokane na matatizo yale, yale maji sasa hivi zamani miaka mitano nyuma, kumi palikuwa hapajai maji pale kama vile, maji yanapita yanakaa kidogo yanapita kwa sababu njia za maji zipo. Zinapita zake pale chini kule makaburi ya wakristo samahani kusema hivyo, mpaka yanakwenda zake ziwa maboga, lakini leo hii mtu kajenga nyumba kwenye mtaro, kaziba mtaro kajenga nyumba maji yale uendaji wake umekuwa mdogo. Sasa inasababisha kadhia pale chungu nzima, ukitaka kutoka Fuoni uje mjini unatumia masaa matatu. Utoke kwako saa moja kamili ufike hapa Barazani saa tatu na leo imefanyika hivyo, kwa kisa tunaogopa kuchukua maamuzi magumu. Na Ofisi ya Uratibu hipo sasa sijui inaratibu nini? Nitaomba sana katika hilo hayo wanayoratibu ni yepi nije niambiwe vizuri ili na mimi niridhike katika hicho.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Diwani umebakiza dakika mbili.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante nitamalizia, vile vile juzi tu hapa nilikuwa mfuatiliaji mzuri mimi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Juzi ilikuja kadhia yetu kuna mbunge mmoja, aliuliza juu ya kadhia Gesi na Mafuta kwa bahati nzuri Mhe. Mwakiembe alisimama akajibu majibu

sisi wenyewe tunaambiwa na watu mnaona nyie mnakaa mnatudanganya mnasema mnatunga Sheria mnamuona mwanamme yule yaani inaonekana kama kule ndio wanaume sisi huku wanawake kwa vile walivyoamua.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa kauli hiyo siyo nzuri, huwezi kusema kama kule wanaume sisi wanawake naomba sana uombe radhi Baraza hiyo kauli sio nzuri hasa kwa kuwa mimi nataka nikwambie maana ya kauli hiyo. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa kipenzi Naibu Spika, nachukua fursa hii kuomba radhi Baraza kwa lugha niliosema lakini itakuwa *massage send and delivery*. Sasa katika hicho, basi tuambiwe tuwekwe sawa katika suala hilo, kulikoni Mhe. Mwakiembe, alivyosema Zanzibar haina mamlaka na hana sababu ya kuyatoa mafuta yale katika Maungano kazungumza Waziri aliyekuwa Waziri wa Sheria na Katiba ambae sasa hivi ni Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo Tanzania Bara na mwisho akamalizia Kalamanganda Kabudi alijibu hilo hilo kwa sababu suala lile liliulizwa na Mbunge wa Upinzani.

Je, nini tunajibu, hichi ndio chombo kikuu cha Wazanzibari kusikia sauti zao, nitaomba sana Mheshimiwa atakapokuja kujibu hili lazima alipigie kelele na tujuwe kama alivyosema mwenzangu hapa kama Muungano tunaogopa upande mwengine kusema ukweli, lakini sisi itabidi tuseme. Kwa sababu ukweli utabakia hivyo hivyo, hauwezi kufutika.

Baada ya hayo siungi mkono hoja nasubiri majibu yangu ipasavyo kutoka kwa Mhe. Waziri baada ya hapo kunipa majibu ya kuridhisha na itabidi niunge mkono. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Abdalla Maulid Diwani, ingawa kwa kweli Mhe. tujirekebishe kwenye kauli zetu, wakati tunasema hivi kwanza tufanye utafiti kwa mambo ambayo tunaanza kuyalaumu hapa. Lakini nashukuru kwamba Waziri atayajibu, lakini kauli ya kudhalilisha mtu mwengine hasa tumo ndani Baraza la Wawakilishi na kuna wanawake ndani ya baraza hili, kauli uliyoitumia kwa kweli si haki huwezi kusema kwamba wanawake maana yake sisi ni dhaifu, ndio kauli ambayo umeitumia. Mhe. kumbuka umepigiwa kura na wanawake wengi sana katika jimbo lako. Tunaendelea. *(Makofi)*

Utaratibu

Mhe: Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 63 nilikuwa naomba kitu kimoja Naibu Spika, kutokana na mazingira ya Baraza letu wakati wajumbe kutoka upande ule wanapochangia

na masuala ya *echo* huwa hatusikii kabisa upande huu, kwa hivyo tunaomba sana wajumbe wanapochingia upande ule kule watumie kidogo sauti, kidogo kidogo au haraka sana hatusikii kabisa. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Tunaendelea Waheshimiwa na jengine ambalo nimekumbuka kuhusiana na kugonga meza, mafundi wetu wa mitambo wanasema sababu moja inayofanya hizi *microphone* zisifanye kazi kwa sababu tunagonga meza sana na tunaziharibu. Kwa hivyo naomba sana vile vile, hilo muwe nalo makini kwamba msigonge meza sana, kwa sababu hichi hichi ambayo inatusaidia katika kusikia tuna na kuzungumza vile vile tunakiharibu kwa hivyo ningeomba Waheshimiwa tukigonga tugonge tunajua mengine yanatufika ndani ya nyoyo zetu lakini tugonge taratibu. Tunaendelea. *(Makofi)*

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kuweza kusimama hapa katika jioni hii ili na mimi niungane na wenzangu kuchangia, Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja mchango wangu utakwenda ukurasa wa 28, 29 Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti Madawa ya Kulevya. Kwanza nishukuru Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa juhudi zake wanazochukua katika kupambana na hali hii ya madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, kwanza nipongeze tena jinsi wanavyofanya jitihada ya kuelimisha jamii juu ya athari ya madawa ya kulevya. Katika ukurasa wa 29 Kifungu cha 4 wameeleza hapa jinsi walivyotoa elimu kwenye vyombo vya Redio, vyombo ya TV lakini na hata katika shehia katika maskuli lakini pia Mhe. Naibu Spika, na mimi nashauri kwa vile sasa hivi tuna mabaraza katika shehia yetu mabaraza ya vijana ilikuwa naomba Tume hii nayo iwaelimishe yale mabaraza ya vijana ili na wao waweze kuelimisha vijana wenziwao kwa sababu, Mhe. Naibu Spika, hili janga la madawa ya kulevya ni janga ambalo linaathiri vijana wetu ambao ndio tegemeo la taifa la kesho.

Mhe. Naibu Spika, vijana wetu hivi wanaingia sasa katika madawa ya kulevya na kusababisha kuingia katika vitendo viovu kama vile, wizi, ubakaji, udhalilishaji wa watoto wetu hivyo nilikuwa nashauri, kwamba wapewe elimu tena zaidi ili kuondokana na janga hili. Lakini Mhe. Naibu Spika, pia nataka Ofisi hii iwashughulikie zaidi wale ambao wanaleta haya madawa. Kwa sababu tumeona jidihada zinachukuliwa hapa lakini hatuoni ni watu wangapi wamechukuliwa hatua kuhusu masuala haya ya uletaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. nikitoka hapo naenda ukurasa wa 46 unaohusiana na Baraza la Wawakilishi, kwanza niipongeze Afisi yetu ya Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote kwa juhudi zake wanazozifanya lakini pia niwapongeze Wawakilishi wote kwa jinsi wanavyotumikia wananchi waliotutuma. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba pia Afisi ya Baraza la Wawakilishi iko Unguja na iko Pemba. Naomba na ile Afisi yetu ya Pemba ya Baraza la Wawakilishi lile jengo lifanyiwe matengenezo ili baadhi ya vikao navyo vifanyike Pemba.*(Makofi)*

Kwani wananchi walio Pemba na wao wana hamu ya kuona Baraza nawao ninafanyika Pemba kwa hivyo hapa naishauri Serikali ilifanyiwe matengenezo ili baadhi ya vikao tufanyie kule Pemba.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi niende kwenye suala zima la maafa ya mvua. Suala hili wengi wameshalizungumza lakini na mie kwa sababu maafa haya yametokea ndani ya wilaya yangu zaidi. Wilaya ya Mkoani kama alivyosema ilivyosomwa ripoti pale na Mhe. Makamu wa Pili kwa hivyo ni wape pole wale wote waliofikwa na maafa haya kwani hii ni kudra ya Mwenyewe Mwenyezi Mungu si ya mtu. Kwa hivyo niwaase tu wazanzibari wenzangu kuwacha kujenga zile sehemu ambazo zina mabonde zina milima zina maji. Kwa sababu tunajenga bila ya kuangalia hapa athari ya mvua ikitokea itakuwaje. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, niwapongeze watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuanzia yeye mwenyewe, mawaziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Afisi, kwa kutuletea hotuba hii, kwani bila ya wao tusingeweza leo kukaa hapa tukaijadili hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Tatu Mohamed Ussi, mchangiaji anayefuatia ni Mhe. Saada Ramadhan Mwenda, baadae atafuatia Mhe. Simai Mohammed Said. Karibu Mhe. Saada Ramadhan Mwenda.

Mhe. Saada Ramadhan Mwenda: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, aliyeweza kunipa uwezo wa kusimama hapa nikapata kuongea niliyokuwa nayo ndani ya moyo wangu.

Pia jengine niwape pole tu wananchi wa Zanzibar mpaka Tanzania Bara waliopata na maafa, Mwenyezi Mungu ndiye aliyetupa mtihani huu lakini Inshaallah Mwenyezi Mungu ndiye atakayetuondolea mtihani huu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza naanza kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kazi kubwa waliyotufanyia sisi wananchi wa Chumbuni Karakana ,kutuwekea ule mtaro, nasema tunawashukuru sana pamoja na wananchi wote wa Karakana hususan wanawake, tunawashukuru Serikali kutuwekea mtaro ule kwa sababu tunashukuru sasa hivi tupo vizuri. Kwa hivyo kubwa nilikuwa nikiomba tu Mheshimiwa kama kuna jitihada nyengine naomba kupitia serikali basi wafanyiwe na wanawake wa Sebleni kwani ndio wanawake walionipigia kura. Lile tatizo bado ni kubwa nalo lipate kuonekana, kwa hivyo naomba sana serikali pale ipatupie jicho pale Sebleni na yale maji yapate kuondoka kama yalivyoondoka pale Karakana.

Mhe. Naibu Spika, jengine nilitaka kuzungumzia mambo ya mazingira ukurasa wa 7. Lakini nisiwe mkosefu wa fadhila pia niwashukuru Manispaa ya Mjini kwa kuhakikisha Mstahiki Meya kusimamia Baraza lake na kuweza kupitisha ili tukawekewa ule mradi wa mtaro ukaja kule kwetu Chumbuni, bila ya yeye nadhani usingefika.

Mhe. Naibu Spika, kumezungumziwa habri ya mazingira. Ni kweli mazingira tunataka kuyafatilia na tunayatengeneza na tunajitahidi kuwashajihisha wananchi wetu ili wapande miti. Lakini na tunajitahidi kuwaambia wananchi wetu wasichimbe mchanga ovyo na wasiharibu vitega uchumi tunavyowekewa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni kwa bahati nzuri mimi kule Wilaya yangu ya Mjini au Mkoa wangu wa Mjini kuna vijana wengi sana kwa vile tunavyojua serikali yetu haina uwezo wa kuwachukua wananchi wote wakafanya kazi lakini imetoa agizo wananchi wale wajielimishe na wajiendeleze kufanya biashara ili kujipatia mahitaji wao wenyewe na familia zao. Kwa bahati nzuri hivi karibuni, kule karakana kuna wananchi wengi wanachonga, hivi karibuni waliitwa na Idara ya Misitu. Wakaenda, walipofika wakaambiwa tunakwambieni kuanzia sasa hivi watu wasilete mkaa, miti ya simbauranga, wasilete magogo. Sasa nikawa najiuliza hapa ndio tunaambiwa tulinde mazingira hivi bila ya kuleta bidhaa hizi kutoka kule Bara sisi kweli tunazo nyenzo kama hizi za kuweza kufanya kazi hapa kwetu ili tukapata kustirika na familia zetu na watoto wetu. Lakini ni vipi tutaweza kujenga mazingira hayo bila ya kupata vitu vinavyotoka mbali.

Mhe. Naibu Spika, suala hili limewasikitisha sana wananchi wa kule. Sijui Mkurugenzi alikusudia yeye mwenyewe kashirikiana na serikali au kaamua tu yeye mwenyewe kuwambia maneno kama hayo. Hivyo Mheshimiwa

unapowaambia watu wasichukue miti au mkaa kutoka Bara, hivi kweli sisi tunao mkaa hapa Zanzibar wa kupikia bila ya kupata mkaa kutoka Bara. Lakini juu ya hivyo hao wananchi mliowambia kwamba wajitegemee watajitegemeaje wakati vitega uchumi vyao mnawakataza mnamwambia mtu asichukue chochote hivi unategemea hao wananchi watajiendeleza. Halafu tunasema hakuna kazi. Sasa kazi zenyewe watazipata wapi na wakati wameshajiajiri wenyewe. Nilikuwa naomba sana hili suala nije niambiwe. Suala hili ni yeye Mkurugenzi kalikusudia kusema tu kwa starehe zake au hili limezungumzwa kwamba yeye ndio awambie wafanyabiashara ili wadhalilike na familia zao pale walipo, aje anambie Mheshimiwa Waziri.

Mhe. Naibu Spika, jengine nilikuwa nazungumzia hili la udhalilishaji. La udhalilishaji hili tutaendelea kulisema kwa sababu bado hili suala linaendelea. Ingawaje serikali imejitahidi pia Mahakama inajitahidi kwa uwezo mkubwa. Tunasema tunawashukuru kama sisi wanawake, lakini tunasema bado waendelee. Kesi ikipatikana isiwekwe, wahukumiwe na wafungwe kama miaka saba, miaka mingapi na kama kunauwezekano wazidishiwe hasa isiwe saba tu. Maana wanawadhalilisha na wanawabaka vibaya watoto wetu. Nilikuwa naomba kubwa ingawa wanajitahidi serikali lakini iongeze bidii ili tuhakikishe haya matatizo yanakwisha. Inawezekana kama tutaamua kwa pamoja matatizo yatakwisha.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mengi isipokuwa naunga mkono hoja hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Saada Mwenda, sasa anayefuata ni Mhe. Simai Mohammed akimaliza atafuata Mhe. Suleiman Sarahan. Mhe. Simai Mohamed Said karibu.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kwa niaba ya wananchi wangu au wananchi ambao mimi nikiwa kama mtetezi wao na msemaji wao wa Jimbo la Tunguu kwa kufika hapa, najua wananipenda na mimi kama wananisikiliza niwambie pia nawapenda sana, Wazungu wanasema *I love you, I love you too.*

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii pia kuwapa pole ndugu zetu wa Tanzania kule Arusha baada ya msiba mkubwa uliowakuta Watanzania wenzetu, watoto wetu, malaika na kwa kweli sote tumepata majonzi makubwa. Lakini nichukue nafasi hii kupitia Afisi yako Mhe. Naibu Spika, upeleke

salamu zangu za pole kwa Mhe. Spika kwa msiba uliomkuta leo juu ya mlezi wake, yaani mama yake, *Innalillahi Wainna Ilayhi Rajiuun*.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kutoa mchango wangu katika Afisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndiye msimamizi mkuu wa serikali, penye mabaya, penye mazuri yote yatamkuta yeye. Pale pia kwa bahati mbaya au nzuri masuala ya maafa yapo kwake yeye. Nataka nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Tunguu ambao nawawakilisha hapa katika hili Baraza la Kutunga Sheria kuipongeza kwa dhati kabisa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mawaziri wote pamoja na Manaibu Mawaziri kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka laki moja na nusu mpaka laki tatu.

Hili ni jambo la kujipongeza kabisa kwa nchi yetu ya Zanzibar. Lakini nichukue nafasi hii pia kuwapongeza zaidi kwa Rais wetu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuanzisha kwa makusudi bidii ya kuweza kuwalipa au kuwasaidia wazee wetu Shs. 20,000/- kwa kila mwezi, kitendo ambacho hakijawahi kutokezea kusini mwa Jangwa la Afrika. Sisi kama Zanzibar tumekuwa tunatoa njia kama miaka ya nyuma iliyopita, nasema pongezi sana serikali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa nitapenda niende katika maeneo tofauti ambayo nitapenda niyachangie. Suala la kwanza nataka nizungumzie suala zima la uimarishaji wa uhusiano wa nchi zetu ambazo zipo majirani na nchi za kutoka Mabara mengine. Kwa upeo wangu katika miaka ya nyuma na kwenye ujana wangu na utotoni mwangu, nakubali bado mimi ni kijana lakini nilipokuwa kijana mdogo zaidi nilikuwa naona wageni au viongozi wa Kitaifa wakija Zanzibar katika miaka ya nyuma. Lakini hivi karibuni imekuwa hili jambo hatulioni na mara nyingi wanaishia katika upande wa pili wa muungano. Tunaweza tukaangalia hata alipokuja Waziri Mkuu wa India, hapa viongozi waliondoka kwenda kuonana nae Dar-es-Salaam.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni tulipata ziara ya mfalme wa Moroco ambaye alikuwa sio kwa mapumziko yake mwenyewe na alifikia Zanzibar na alipapenda sana hapa. Alitembea Zanzibar katika maeneo tofauti lakini haikuwa ziara ya kiserikali. Sasa ninachokiomba Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kupitia maeneo ambayo yanayosimamia maeneo ya Muungano basi watumie nafasi yao. kwamba na sisi pia Wazanzibari tunahamu kuona Viongozi wa Kitaifa kutoka nchi tofauti wanapokuja Tanzania basi na wao wafike hapa Zanzibar kwa sababu Wazanzibari na wao wana hamu nao.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunavyozungumza tunatarajia wakati wowote Rais wa Afrika ya Kusini Mhe. Jakob Zuma atakuwepo katika ziara ya siku tatu hapa Tanzania, lakini hapa sisi Zanzibar hatutomuona. Napenda sana hili lina umuhimu wake kwa Wazanzibari na mahusiano yetu kutokana na huko miaka ya nyuma basi liendelezwe.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka nizungumzie Idara ya Sherehe ambayo inasimamiwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Nataka nishauri kitu kimoja kwenye sherehe panahitajika mambo mengi sana. Lakini kama itawezekana kwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais waongeze nguvu kuanzisha kampuni ya kupata mashamiani ya kisasa, meza, viti ili hata mikutano ya kimataifa pale inapotaka kufanyika Zanzibar kuwe kunawezekana kufanyika. Lakini pia wananchi wanapohitaji kutumia hivi vifaa waweze kukodishwa na waweze kufanya matumizi.

Mhe. Naibu Spika, mashamiani ambayo yanatumika katika sherehe za serikali ukiangalia katika mazingira ambayo tuliyokuwa nayo hata katika kipindi hichi kwa kweli hayastahiki na mazingira tunayokwenda nayo hivi sasa. Kuna uwezekano mkubwa kabisa siku hizi tukapata mashamiani ya kisasa yenye ubora zaidi ambayo serikali na Afisi hii pamoja na Wizara nyengine wataweza kutumia. Naomba sana wafanye mpango maalum watafute fedha ambapo watazipata watuletee hapa, ili tuweze kujipanga na sisi kuidhinisha kwa niaba ya wananchi ili mambo haya yote waweze kufaidika wao pamoja na wananchi.

Mhe. Naibu Spika, katika sherehe hizi za Muungano mara nyingi ukiangalia katika vikundi vinavyofanyika Dar-es-Salaam au mara hii ilikuwa Dodoma. Vikundi vya sanaa vinavyotumika mara nyingi ni vile vile, utawaona watu wale wale wanaokwenda na aina ya ile sanaa au ile burudani inayopatikana pale ni ile ile katika vikundi ambavyo vinatoka Zanzibar. Nilikuwa namuomba Mhe. Makamu wa Rais kwa kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili kwamba hata mimi jimboni kwangu nina vikundi vya sarakasi. Naomba sana na mimi vikundi vyangu vya sarakasi ni vizuri na ni vikundi ambavyo wamejituma sana ili katika kuleta jambo tofauti, basi waangalie uwezekano wa kuvialika hivi vikundi vya sarakasi ili na wao pia waoneshe ubora na umahiri wao kama Wazanzibari na Watanzania.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo niliwahi kuona mara moja katika Sherehe za Muungano Dar-es-Salaam, msanii maarufu kutoka Tanzania Bara Lady JD aliimba wimbo wa Taifa. Mimi naamini tunao wasanii kutoka Zanzibar kama Baby J, waalikwe, waende wakaimbe wimbo wa Taifa na wao pia waonekane. Kwa sababu ukiangalia katika ile burudani pale ni nafasi pia ya kujitangaza,

kwani TV zote zinakuwepo pale. Lakini katika *promotion* nzima na hawa wasanii pia itakuwa tutakuwa tunawasaidia katika kupitia hizi sherehe. Tumeona katika Sherehe zetu za Mapinduzi Zanzibar jinsi walivyokuja pale na wananchi walivyofurahi. Serikali ilifanya sherehe za aina yake pale Maisara, wasanii walifurahi, vijana walikuwa ni wengi na burudani ilikuwa nzuri kabisa. Kwa hivyo niombe sana na hili naomba maombi yangu yawachukuwe na naamini katika sherehe za mwaka ujao basi na vijana wangu katika jimbo langu watapata kuwaona.

Mhe. Naibu Spika, lakini hapa nataka niliseme jambo moja ambalo ni la muhimu kabisa. Ningeomba sana Mhe. Waziri alikamate vizuri kwa sababu itakuwa ni mara ya tatu nalizungumza katika Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili inasimamia masuala ya Muungano kuna mambo mengi ambayo ni ya Muungano kuna mengine si ya Muungano lakini pia tunafanya kazi kwa ukaribu na ndugu zetu kutoka Tanzania Bara. Lakini kuna mambo muhimu ambayo kama mfano Utalii sio eneo la Muungano lakini linatugusa pande zote mbili za Muungano. Kuna miezi ambayo hapa Zanzibar sisi tunakuwa tayari pengine wagenikama kipindi hiki wanakuwa wanapungua kutokana na mvua, lakini pia kuna miezi kama ya Septemba, Oktoba na Novemba, wageni wanakuwepo. Lakini majirani zetu ukienda Kigali, Nairobi, Kampala kuna raia ambao wapo kutoka nchi za nje wanafanya kazi pale kama wao ni wakaazi wa pale kwa muda ambao wameajiriwa pengine katika taasisi za Kimataifa lakini pia katika taasisi za Kidiplomasia, wana *residence* yao ya kuishi katika nchi hizi za jirani kwa muda usiopungua miaka mitatu mpaka mitano.

Mimi naomba sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar iangalie uwezekana kama wataweza katika ile miezi ambayo ya kimya watafute njia na utaratibu huku ikitambua kwamba masuala ya usafiri wa anga, masuala ya Uhamiaji ni mambo ya Muungano ikiwa mtu anataka kusafiri kutoka Nairobi kuja Zanzibar moja kwa moja katika ile miezi ya kimya basi aje bila ya kulipa *VISA fees* atapigiwa *Visa* yake lakini hatotozwa fedha katika ile *Visa* atakayolipa. Hapo tutampa nafasi Waziri wa Utalii aende zake Kenya, Uganda, pamoja na Rwanda kupiga debe ili kuwavutia hawa raia waweze kuja hapa.

Endapo wenzetu wa Tanzania Bara wao wataona kwamba haina faida sisi tuanze upande wetu kwa sababu mwisho ya siku hizi fedha zinabakia Zanzibar. Naamini vitanda vyetu baada ya kulala vitupu tutaongeza mtaji zaidi, watatumia fedha katika maeneo ya usafiri, maeneo ya kula chakula, maeneo ya malazi, lakini pia kuwakamua hawa wageni katika masuala mazima ya

matembezi hapa katika visiwa vyetu. Ikiwezekana pia na naomba sana Mhe. Waziri uliangalie kwa umakini kabisa. Hapa sisi tuna ndege ya *Ethiopia Air line zi*nakuja, twende zetu sisi mpaka Addis-Ababa, baada ya Washington Marekeni katika nchi duniani yenye watu wengi wanaofanya kazi hasa katika masuala ya deplomasia na taasisi za kimataifa basi ni Addis-Ababa na ni masaa mawili au matatu mpaka Zanzibar. Pia tuna ndege zinazokuja moja kwa moja, sisi tuende kule tumpatie Waziri wa Fedha nyenzo ili aende akapige debe ili aondoe *visa* kwa wale wageni wote wanaoishi pale kwa nchi ambazo sisi tuna mahusiano ili wazidi kumiminika hapa na wao pia watarudi kule watakuja na familia zao. Hatimae yake Zanzibar tutapata fedha zaidi tutakuwa tunatumia nafasi yetu vizuri, tutajenga mahusiano mazuri na tutazidi kupendana sisi wenyewe pamoja na nchi ambazo wageni watakuwa wanakuja hapa kama watalii lakini kwa matembezi.

Mhe. Naibu Spika, hili linawezekana sana kwa sababu hata nchi tofauti za Arabuni na maeneo mengine ya Ulaya ndio njia za kumtongoza au za kumfanya mgeni aweze kuja. Lakini mamlaka haya natambua kabisa yapo chini ya Afisi ya Muungano lakini sisi kama Zanzibar tuna nafasi yetu katika hili. Naamini Mhe. Waziri kama utaweza kulifanyia kazi na Waziri wa Utalii atatoka hapa atakwenda kupiga debe basi sisi Zanzibar tutafaidika na Mahoteli yetu yatazidi kujaa, tutasema sasa hatuna tena *low season* mwezi wa May na mwezi wa Juni tunasema tutaiita *green season* na mwenzi wa Oktoba, Novemba na Septemba tutaiita ni miezi ya burudani ya kwenda kuzamia na tutafuta jina jengine la kuwaita.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwa upande mwengine nataka nishauri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika usimamizi mzima masuala ya utumishi juu ya watendaji ndani ya serikali hasa watendaji wa wakati na kwenda chini. Kuwepo na *uniform* ambazo wafanyakazi wa serikali watazivaa. Unaweza kuingia ndani ya taasisi ya serikali wakati mwengine usimjue mtendaji ni nani, ukafika pahala ukahisi na yeye ni mtu ambaye anahitaji huduma kutoka serikalini. Ukienda kwa mfano katika Afisi ya Rais sasa hivi wafanyakazi wao wote ndani ya Ikulu wanavaa beji. Inawezekana pia na watumishi wengine wa umma ukatafutwa utaratibu maalum kutoka madereva wa Mawaziri mavazi yao ya kaunda wakatengenezewa, wakawa ni rasmi *official* angalau wanapotoka wanapokuwa kwenye makaazi yao wanakuwa wapo vizuri. Mavazi yana heshima yake. Hata sisi tunapokuja humu ndani tumejiwekea utaratibu juu ya mavazi yetu na sura kamili.

Lakini leo ukimuona mtumishi wa umma amevaa makubadhi, amevaa shati, lakini shati alilolivaa au suruwali haliendani na kazi yake ambayo

anayoisimamia. Kwa kweli haipendezi hasa pale tunapopokea wageni kutoka kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara au tunapokutana katika Semina za Kimataifa. Naomba sana hili waliangalie na utaratibu mzuri upangike.

Lakini pia nikienda kwenye suala la Wakala wa Serikali na suala zima la uchapaji. Kwa kweli taasisi hii ni muhimu na ningeshauri wazidi kujiimarisha nyenzo na kutafuta utaalamu zaidi ili kuweza kujitangaza kwa upande wa Tanzania Bara pia na Makampuni mengine waweza kuitumia na pale wanapokwama wasione tabu kutafuta makampuni binafsi ya Zanzibar ili waweze kuunganisha nguvu kufanya kazi kwa pamoja. Huku kwenye *private sector* haya mambo yapo yanafanyika kawaida lakini unapounganisha nguvu kwa maslahi ya nchi au kwa maslahi pia ya kibiashara inawezekana.

Mhe. Naibu Spika, nimeona katika hotuba ya Mhe. Makamo wa Pili amezungumzia suala la tafiti na zimetajwa tafiti 61 mimi ningependa nifahamu hizi tafiti ambazo pengine ni wanafunzi wanaokuja kufanya hizi tafiti, lakini hatma ya hizi tafiti jee zinaishia katika wizara zetu, zinaishia katika maktaba na kumbukumbu na Ofisi ya Makamu wa Pili au zinatumika au wanaondoka nazo na sisi nakala zake tunakuwa hatuzipati. Kama kweli tunakuwa tunazipata hizi tafiti jee zimetumika katika sehemu gani na katika nafasi gani kwa upande wa Zanzibar tumeweza kufaidika kwa sababu inawezekana kuona hizi tafiti ndogo lakini kwa ujumla ina umuhimu wake katika kuisaidia Zanzibar na Tanzania kwa sababu ndani watu hawa hutumia muda, nafasi, fedha na raslimali nyingi ili na sisi kuweza kufaidika kwa tafiti kama hizi, suala jengine nataka nirudi kwenye suala kidogo kwenye muungano.

Mhe. Naibu Spika, nataka nishauri kitu kimoja mwaka jana nakumbuka wakati wa bajeti hapa niliongea sana mpaka nafikiria koo ilinikauka kwa hivyo, mwaka huu sitotumia nguvu kubwa sana kwa sababu naamini katika suala hili nilifahamika vizuri, nikashauri vizuri lakini bado matokeo si ya kuridhisha kabisa na hasa katika suala ambalo la usafiri wa magari kwa Wazanzibari kwenda kwa matembezi au kwa shughuli zao binafsi kwenda Tanzania Bara.

Nilisema mwaka jana ndugu zetu kutoka Kenya, ndugu zetu kutoka Malawi wanaingia Tanzania kwa fedha dola 50 mpaka 70 mpaka 100 kwa muda wanaoutaka miezi mitatu mpaka sita. Lakini iweje leo Mzanzibari akitaka kundoka na gari yake kwenda bara si kwenda kuuza hii suala la kuuza ni sababu ambayo inatumika kwa wale ambao ni wafanyabiashara, wafanya biashara wanaosimamia juu ya masuala ya magari pengine ni 100 au 200. Lakini nazungumza katika suala zima la watu ambao ni raia kama sisi hatufanyi biashara tunataka kuchukua familia zetu kwenda kwenye mbuga wakati wa

mapumziko kwenda kutembelea ndugu zetu kuingiza gari ndani ya *Azam Sea Link* haiwezekani mpaka ufanye utaratibu ambao ni mrefu, lakini Mzanzibari ni Mtanzania narudia tena Mzanzibari ni Mtanzania na mimi ni haki yangu ni haki yetu sote sisi ya kikatiba kuweza kwenda maeneo yote sasa leo mimi siwezi kuondoka hapa na gari yangu ni kwa nini najiuliza hili suala mwaka wa nne wa tano. Nimelizungumza kwenye Baraza la Biashara nikiwa mjumbe kabla sijaingia ndani ya Baraza la Wawakilishi, nimezungumza mwaka jana, nitaongea mwaka huu najiuliza nafsi yangu leo hapa jee nitaendelea kulizunguza hili mwaka ujao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba unionee huruma kwa hili unisaidie wakati waziri anapokuja hapa ili tupate sote majibu ambayo tutarudi kwa wananchi watuelewe hili utaona ni suala dogo. Lakini linawagusa wananchi wetu wengi sana na pana mambo mengi sana hapa, lakini pia nishauri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wafanye ziara aya kwenda Dar es Salaam wakae tu pale Bandarini waangalie jinsi wafanyabiashara wanavyopita kutoka Bara, kutoka Zanzibar na jinsi pale utaratibu mzima ulokuwepo.

Mimi nilikuwa mjumbe kusimamia Ofisi kusimamia Ofisi ya Makamu wa Pili na Ofisi ya Rais kwa sasa nimo katika kamati ya Bajeti pia nilipokwenda nilimshauri Mratibu Tanzania Bara nikamwambia hebu tafadhali jaribu kwenda kuangalia nini kinachoendelea kwa nini wananchi wanalalamika, wananchi wanatakiwa waisifu Serikali yao lakini katika hili wanakuwa wanapatza manjozi wanakuwa hawana raha ni wananchi ambao wengine ni wapiga kura wetu, wengine hawana chama, wengine ndio wale. Sasa mimi nanachokiomba sana katika haya madogo madogo wakati mwengine tunayachia mpaka yanakuwa tena makubwa, ndio baadaye utakuta jambo tunaita Kero za Muungano kero huishia kwa sababu tunaachia jambo mpaka linakuwa kubwa, hasa haya yote tunaomba sana yatatuliwe mara moja ili na sisi tuweze kutembea kifua mbele kwamba haya sasa mambo yamekuwa.

Lakini pia ukiangalia Mhe. Naibu Spika, tangu tumeingia kwenye hili Baraza la Wawakilishi kuna maeneo ambayo ni ya muungano na kuna maeneo si ya muungano, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi inawekana sana tunataka sana tuzungumze na Mawaziri wa Jamhuri hapa, kwa upeo wangu nakumbuka hapa ni Waziri mmoja tu kutoka Jamhuri ya Muungano amefika kutuona sisi au kuja kutusikiliza na akatoka nje tukamuona kabisa ni Mhe. Waziri Januari Makamba. Lakini sijawahi kumuona Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri wa Ulinzi na kuna maeneo ambayo tunaka kuongea nayo kuna masuala ya ajira ndani ya Muungano, ajira ndani ya vyombo vyetu vya ulinzi tunataka tuyasikilize lakini hatuyafahamu.

Kwenye ripoti ukisikia humu Serikali wamekaa vikao wametoa taarifa sawa lakini humu ndani sisi hatujawahi kufanyiwa semina tukahoji tukaeleza haya ndio tumekubaliana, haya ndio matatizo yalokuwepo. Kwa hivyo inawezekana sisi tunaongea mambo hapa tayari yashatatuliwa yanazungumzwa lakini sisi hatuyaelewi kwa undani na sisi kama wawakilishi wa wananchi tutaendelea kuyasema, kwa sababu hatujui undani wake wamefika wapi. Sisi tunataka kwanza pia tupate nafasi hawa Wabunge na Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano waje kutuona sisi pia wasiishie Serena, wasiishie *Park Hayatt* wasende shamba kulala kwenye hoteli na kuondoka wakasema wanaijua Zanzibar. Waje hapa wakae na sisi tukae nao watuone, mbona mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanakwenda Tanzania Bara wanashiriki katika mambo mengi wao hatuwaoni wala hatuwajui na kama tutakwenda hivi tutamaliza sisi mpaka miaka yetu mitano humu ndani hatujawaona. Kwa hivyo, naomba sana mawaziri ambao wanasimamia maeneo ya muungano waje kukaa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili tupate fursa ya kuzungumza nao kujadili, kutafakari na kupeana mawazo lakini pia kuwapa maeneo ambayo tunataka kuzungumza.

Wakati mwengine ninasononeka sana wabunge kutoka Jamhuri ya Muungano wanavyoizungumza Zanzibar, mbunge akisimama upande wa Zanzibar kuzungumza suala la Zanzibar wakati mwengine anazomewa anambiwa kaongee huko haya hayahusu hapa. Sasa mbunge ikiwa anatoka Zanzibar anakwenda kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano ambayo tumewatuma sisi kwenda kuongea kwa niaba yetu anaambiwa pale sipo pake sasa akaongelee wapi. Kuna maeneo tunatambua hawezi kuyazungumza kwa sababu wako wawakilishi wa majimbo yao lakini kuna maeneo ambayo ni ya Kitanzania maeneo ambayo ni ya muungano ni haki yao kuyazungumza kuna masuala ya usafiri wa anga, kuna masuala ya TCRA kuna mambo mengi kabisa. Sasa mimi naomba katika hili naweza nikasema mpaka nikadata waje tukae nao tuzungumze nao ili tumalizane sisi kwenye vikao vyetu halafu tukitoka nje tunajuana sote, lakini leo unasema hili hapa yule kule anapinga kile wache wakae na sisi tuje tusuguane kwa pamoja.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, mimi nikushukuru kwa nafasi hiyo lakini pia nimalizie kwa kuleta maombi kwa Mhe. Waziri kwamba siku zijazo za mbele nitamualika Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Jimboni kwangu afanye ziara ikiwa atapata muda au atapendezewa pia aje kuangalia maeneo ya Tunguu ambapo kunakatwa viwanja watu wanazidi kuongezeka, makaazi ambayo yanakuja kule na pia ikiwezekana atembelee tangi la maji la Unguja Ukuu ambalo linavuja kama mfereji wa mvua ende zake Dunga nikamuoneshe tangi la maji kwa sababu yeye ni msimamizi wa Serikali Kiongozi wetu humu ndani, Kiongozi

wa Serikali kwa hivyo naamini anapokuja kuyaangalia haya yote huku ndani kwa hivyo anapata kuelewa zaidi wakati pale ninapozungumza ili aone changamto ambazo zinanikabili kwa wananchi wangu pamoja na hizi barabara za ndani ambazo ziko chini ya Halmashauri, ili utaratibu mpya ufanyike mwaka huu kwa sababu nyumba hizi hivi viwanja vimekatwa na Serikali, barabara za ndani hakuna, maji hakuna, watu wanachimba visima, wengine hawapati maji ni mtihani kwangu mimi.

Lakini pia mzigo wote tunarejeshewa kwa mbunge na muwakilishi pamoja na halmshauri na fedha hazipo za kutosha kwa hii kazi. Nitamuomba sana Makamu wa Pili aje kufanya ziara jimboni kwangu kwa muda atakapopata ili tuweze kufanya kazi kwa kushirikiana kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, bado nafasi ulonipa nichukuwe nafasi hii kukushukuru sana kwa niaba ya wananchi wangu na nikushukuru wewe kwa nafasi hii ulonipa.Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru mchangiaji anayefuata ni Mhe. Suleiman Sarahan baadae tutampatia nafasi Mhe. Mussa Foum.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuchangia Hotuba na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein katika kutekeleza majukumu yake na kuwaletea maendeleo Wazanzibar wote kwa ujumla na Tanzania kwa ujumla.

La pili pia nimshukuru Makamu wa Pili wa Rais katika jitihada zake za kufanikisha mambo yote yanamkabili katika wizara zake zote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze na suala la maafa na mimi katika watu ambao wamepata msiba na mimi nimepata msiba katika maafa haya ya mtoto mmoja ambaye alifariki tarehe 30 Aprili, 2017 akiwa mtoto kama miaka minane aliangukiwa na ukuta wa chuo ambao wenzake walipona kwa bahati yeye akafariki anaitwa Rahika Ramadhan Mohamed ambaye yuko Chanjaani pale Chakechake. Ningeomba katika Kamati hii ya Maafa pia au Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wakati atakapokwenda Pemba katika kutoa salamu za rambirambi basi afike ili kwenda kutoa mkono wa pole kwa wafiwa hawa maana yake kwa

kweli mtoto akifa anasikitisha sana. Kwa hivyo ningeomba na yeye akipata nafasi apite pale ili kutoa mkono wa pole kama maafa mengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumze kwamba takriban katika maafa hasa Zanzibar ni kila inapofika mwezi wa Machi mpaka mwezi wa Mei kipindi hiki ndio kinachotupa maafa makubwa. Sasa sijui kabla ya kuanza na matukio yoyote tunajipangaje katika miezi hii ambayo ishakuwa kama ni kawaida. Mheshimiwa tukikosa mvua tunakuwa na maafa mengine ya njaa lakini kwa utaratibu tulonao hivi sasa tunaomba mungu hiyo mvua asiilete wakati si jambo jema ile ni neema, lakini kutokana na mataatizo yanayotupata sasa inakuwa mvua zile hatuzitaki wakati ni neema kubwa sana. Lakini tukae tutafakari na tuangalie ni tatizo gani ambalo kwa sasa hivi imekuwa sio kuwa ni maafa tu imekuwa ni kawaida kwa matatizo yanayotukabili ningeomba wizara hii au Ofisi hii ya Makamuo wa Pili wa Rais au kamati hii inayoshughulikia na mambo ya maafa baada ya kumaliza maafa ikafanya tathmini ni wapi kila siku maafa yanatufika na kwasababu gani.

Kama ni nyumba ambazo ziko kwenye mito basi tusichoke kuchukua hatua ya dharura ili kuziondoa nyumba zile ambazo zinaleta maafa ya kila siku bora gharama ya mara moja tukawaondoa watu wale tukawasaidia kwa kila hali waondoke kuliko maafa ya kila siku *otherwise* ingekuwa kama madhara tu yanotokea kwa mantiki nyengine hiyo tunaita madhara kwa watu ambao kila siku tunakwenda tukiwavua. Kwa sababu maalum ya mvua Mheshimiwa hili tungelichukua kama dharura tukawaondoa watu hawa kwa sababu majanga haya yanatupa tabu sana na ningeomba zaidi Mheshimiwa kama itakiwa ni kawaida ambalo jambo hili limeanza kuwa kubwa sana tukaondoka na Kamati tukaifanya Idara Maalum ya Maafa.

Maana yake sasa sio Kamati, kamati ni kitu cha muda lakini sasa tungeifanya Idara maalum ikiwa inashughulika na maafa na Idara hii ikapewa uwezo na ikajipanga kweli kweli, ikawa inafanya mambo yake ya kimaafa kwamba wakati wote iko tayari kuokoa maisha. Sasa wakati wote maafa yanapotufika tunaita vikosi, tunaita zimamoto wakati bado kuna autaratibu maalum wa hali hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumze suala la maafa ni suala kubwa sana, juzi tu Chake Chake na maeneo mengine tulipata mvua na Pemba nzima karibu ya siku kumi mfululizo ambayo haijawahi kutokea kwa ninavyosikia, pahala palipokuwa hapaingii maji paliingia lakini nataka niseme pale Chake Chake eneo la Timbirinzi lilifurika karibu madaraja yote pamoja na ile Hoteli

ya Hifadhi juzi ilikuwa iwe mwisho wake kwa sababu iliingia maji ndani ambayo nyumba ile ina *underground* lakini maji yote yaliishia ndani.

Kwa kweli Serikali pamoja na vikosi vyake vilifanya kazi ya ziada lakini zimamoto mimi nasema kwamba ni mfano wake walilala pale walitumia gari zao na *pipe* kupunguza maji wao wakachukua juhudi kadiri maji yanavyoingia ndio kadiri wanavyosukuma nje, mpaka nyumba ile ikanusurika. Kwa kweli ile nyumba ilikuwa *Inna Lillah Waina Ilayhi Rajiuun* tumeona hali halisi ilivyokuwa ilikuwa mbaya sana. Mimi ningeomba sana Ofisi inayoshughulika na nyumba ile ya ZSSF kama ni Mkurugenzi au mtu gani basi pamoja na mambo yote yalofanyika aende Pemba akamuone Mkuu wa Mkoa na Vikosi vyake walivyofanya kazi wakashirikiana kuikoa nyumba ile, basi awape ahsante ya kwamba ahsanteni sana kwa juhudi mlizozichukua. Maana yake wao pamoja na kwamba kazi yao lakini walifanya juhudi za lazima za kulala pale pale mpaka kuiokoa nyumba ile.

Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya na Vikosi vyote vilifanya kazi hiyo na Mawasiliano wote, kwa hivyo ni mashirikiano mazuri kwa kweli walijitahidi kuokoa maeneo hayo na siyo nyumba hiyo tu, waliokoa maeneo yalikokuwa yameshazingirwa na maji, barabara zilizokuwa zikatike, mazingira yote yalikuwa makubwa kwa kweli walijitahidi vya kutosha. Kwa hivyo, Mheshimiwa nataka niseme kwamba nawapa pongezi mimi lakini ningeomba na Mkurugenzi wa ZSSF achukuwe dhamira makusudi kwenda kuitizama nyumba ile ilivyookolewa na madhumuni yake hilo lilikuwa la kwanza.

Lakini Mhe. Naibu Spika, miye nataka niseme jambo la pili ni kwamba mimi nataka niwape pole sana watu waliopata maafa, lakini nataka nitoe mfano mzuri wenzetu wanaokaa katika Kisiwa cha Pemba mimi nataka tuige mfano ambao ulifanyika. Mheshimiwa nyumba nyingi sana zilivyunjika, watu wengi sana waliathirika lakini kama si juhudi zao za udugu na umoja basi wangekufa watu wengi sana.

Lakini watu wale mvua zilivyokuwa zikienda majirani walikuwa wakienda kubeba watoto katika nyumba ambazo zilikuwa tayari za kuanguka au kuangukiwa wakachukuwa jitihada za kuwaingiza katika majumba yao na mpaka hii leo watu wale wamo kwenye majumba ya majirani, wapo kwenye majumba ya udugu, hapakufunguliwa kambi na watu wale wanaishi katika hali ya usalama na amani.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningekuomba kwamba kutokana na juhudi za watu wale walizochukuwa nataka nisema na watu walioko Zanzibar udugu ule

waufanye ukarimu sana kwamba na wao wasinyanyuwe mikono tu baada ya kuingiwa na maji lakini ndugu zao, rafiki zao waende kuwasaidia katika wakati ule mgumu sio kusubiri Serikali itanifanya nini. Lakini Serikali ni sisi tukijipanga pamoja tunaweza tukaokoa maisha kwanza ndio rena tukatizama hatua gani zitachukuliwa. Kwa hivyo Mheshimiwa mimi nataka niseme kwamba juhudi zile zilizochukuliwa na watu wa Pemba umoja wao na ukarimu wao ule waendelee nao na ule ndio utatusaidia katika kuokoa maisha yetu. *(Makofi)*

Lakini pia nataka niseme Mheshimiwa mtu akishakuchukuliwa katika nyumba ya mtu ni sawasawa na kumwambia mtu kwamba mgeni siku ya kwanza mpe mchele na panza, mgeni siku pili lakini mpaka ikifika siku ya kumi umtoe kwa mateke na magumi. Watu wale Mheshimiwa naomba waliovunjikiwa na kiambaza kimoja, waliokuwa wamekatikiwa na mazingira tofauti hiki kikosi cha maafa kifanye jitihada za dharura kuurudisha ukuta ule, kurudisha matatizo yale watu warudi majumbani mwao haraka iwezekanavyo kwa wale watu ambao nyumba zao tayari zimekaa katika hali nzuri.

Wengine wameangukiwa na madongo kuliko kumuweka mtu kwenye nyumba katika mazingira ya kila siku kama ni muhanga basi bora tufanye jitihada za dharura kuwarudisha katika majumba yao ili kila mmoja apunguze matatizo hasa na mengine ya maradhi ya kuambukizana. Kwa hivyo nilikuwa nasema hilo Mheshimiwa kwamba kuliko kila siku kutoa misaada basi turudishe haraka zile familia katika nyumba ambazo zinaweza zikarudishika kwa haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, pia niseme katika kisiwa chetu kina maafa na sisi ni watu wa maji na kila kitu, mimi naomba sana Vikosi vya Zimamoto viongezewe uwezo wa *pump* za kutoa maji, juzi walijitahidi *pump* ni ndogo halafu hazina uwezo mkubwa, wanajitahidi na magari. Kwa sababu na wao ndio waokozi wakubwa wasaidiwe vifaa vya nguvu hasa vinavyoweza kutoa maji ambayo ndio maafa makubwa yanayotukabili. Kwa hivyo, ningeomba sana hiyo kamati ya uokozi ikaangalia vifaa vilivyopo katika zimamoto vipi waongezewe nguvu kama ni kamati moja ya maafa, mimi ningesema hivyo ili wapate kusaidiwa.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka niseme sasa hivi lazima tukubaliane maeneo hatarishi yaliyokuwa tayari yanaonekana ni hatarishi basi tusiyafumbue macho, kwani yanatutia kwenye tabu, yanatutia katika mdomo siku zote. Leo tumeokoa wahanga wangapi, lakini tatizo ni nyumba tu na maeneo ambayo hatarishi. Kwa hivyo, lazima tukubaliane kwamba tufumbiane macho zile nyumba zilizokuwa hazifai ziondoke tusubiri maafa mengine. Kwa hivyo ningeshauri

neno tukilisema kama hili ni baya basi ijuulikane kama ni baya na tuweze kuliondoa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, jengine nataka nije kwenye hali ya ulinzi kama vile *Airport* ya Pemba. Viwanja vyote ni viwanja vinavyolindwa na viwanja ambavyo kila mmoja katika usalama wetu upo. Mhe. Naibu Spika, katika kiwanja cha Pemba au katika Zanzibar tunapigania sana madawa ya kulevya na mambo mengine. Lakini katika *Airport* ya Pemba sijawahi kumuona mbwa anayenusa madawa ya kulevya wala askari maalum wenye *technical* za madawa yale, na inawezekana watu wakapita katika mitandao ya maji wakaingia Pemba, halafu wakaruka pale pale Pemba wakatoka katika mazingira mengine. Kwa hivyo, ningeomba kama tunadhibiti basi tusidharau *Airport* ndogo wala *Airport* kubwa, kama Pemba nayo imo katika Kisiwa cha Zanzibar na madawa ya kulevya yanapita mbwa awepo pale ikiwa mtu atajuulikana kama ana wasi wasi, mbwa afunguliwe kwenda kutafuta madawa, sio tunapitishana kusachiana mikono na kupapasana, lakini na mbwa lazima awepo pale. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme serikali, najua kutokana na hali ilivyo serikali imejikita sana kuwapa wananchi wake elimu. Katika asilimia 99% tuliomo humu au 100% au 99.9% mheshimiwa kama mtu hajasoma madrasa chuoni, basi elimu yake haijatimia na utu wake haujatimia kwa desturi na mila ya Zanzibar. Lakini ninakumbuka mimi miaka ya nyuma kabla skuli hazijaaza mpango wa elimu ya kur-ani basi lilifunguliwa darasa lilikuwa linaitwa *KC (Kur-an Class)* kwa mnasaba wa watoto aliyekuwa hakupelekwa chuoni aanze na pale. Ninaloliona sasa hivi pamoja na mazingira tuliyonayo bado madrasa hazijatiliwa maanani kwamba ni elimu, ni darasa moja tu lakini kila siku watoto wale wanasoma chini, wanalala na mbwa wakiamka na mbwa.

Kwa hivyo, serikali ingekagua hizi madrasa nazo zingetia katika mkumbo wake zikawa zinakaguliwa, maana yake ni asilimia 99% watoto wote wanaanza na pale. Matokeo yake ndio kama hivyo nyumba zinaanguka, viambaza vibovu, watoto wanasoma hawana pahali pazuri. Kwa hivyo, ningeiomba serikali katika kuangalia tathmini ya elimu, basi na madrasa ikaangaliwa kwamba kuna haja ya wizara au idara maalum ikaangalia madrasa ambazo tunasoma. Mimi ningeomba sana mheshimiwa hili suala la wanafunzi wa madrasa liangaliwe na hili linasababisha pamoja na mambo yote upande huu hauna madawa, lakini upande huu una udhalilishaji.

Mhe. Naibu Spika, walimu wetu wengi wanaleta maafa, walimu wengine wanasoma kur-an mpaka wanakuwa vichaa, akishakuwa kichaa anachukua wanafunzi anawaharibu. Sasa wangekuwa wanakaguliwa na hawa walimu,

hawa nao ni walimu, watizamwe kwamba wewe hufai na wewe unafaa. Lakini ni kichaa kajifunga kilemba anaambiwa ustadh anakwenda tunaye lakini mama na baba hajui anasema madrasa. Kwa hivyo, ningeomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali au serikali ikawatilia maanani hawa wakaguliwe kama walimu hawa wako sawa. Kwa sababu hiki kitu hakuna hata mmoja asiyepita madrasa. Kama tunajua tunapita pale madrasa basi lazima pale pahakikishwe pako salama watoto wengi wanaharibiwa pale, mazingira yanakuwa sio. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na hilo niliseme kwa ajili ya kulitilia mkazo kwamba serikali itaona kuna umuhimu basi suala hilo ilishughulikie.

Mhe. Naibu Spika, pia nije katika mazingira ya miti. Mheshimiwa mazingira ya kupanda miti na kufanya kila kitu sawa, lakini katika jumla moja ya maafa serikali inataka iangalie kwamba miti yote iliyoko maeneo ya barabarani, iliyoko maeneo ya majumbani ambayo haifai na haiwezi tena kustahamili italeta maafa tusisubiri usiku mti ukawa juu ya paa. Serikali ingefanya makusudi kama barabarani kuna mivinje kama *Airport* ya kule Pemba yote imeshapaganyuka imekaa hivi inasubiri mtu tu imuangukie na gari. Mheshimiwa barabara ile anapita Mhe. Rais, barabara ile anapita Makamu wa Rais, barabara ile wanapita viongozi, wanapita wananchi wote, wanapita wanafunzi mivinje haiwezi kustahamili tena inapasuka ikikatika ovyo. Lakini ukiritimba tulionao kila mmoja anazuia nguzo yake, mazingira wanakwambia usiukate, sijui mwengine anakwambia sina *chainsaw***,** mwengine ukimwambia hivi. Matokeo yake tukisababisha maafa ndio tunaangalia leo tumekata. Kwa hivyo, ningeshauri miti ikakaguliwa iliyokuwa haifai hakuna ulazima wa mazingira ndio ushafika siku yake kama binadamu, binadamu ana mazingira siku ya inafika anakufa basi ndio mazingira yake. Utaulazimishaje mti ukae mpaka siku ya mwisho haupo. Kwa hivyo, lazima miti mengine iondoshwe ili kupunguza maafa haya. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka niseme hilo ili yasitokee na maafa mengine.

Mhe. Naibu Spika, kama Kisiwa cha Pemba asilimia 70% ya ardhi yake ni mabonde na milima. Mheshimiwa watu wa mazingira wanapita wakisema sana tunahifadhi mazingira, milima yote iliyopo Pemba, iliyoko Mjini ndio ukasikia imeanguka kwa sababu haijengewi mazingira mazuri. Kuna utaalamu wa kui-*block* ile milima kama pale Mkoani Ikulu, Ikulu ingekuwa haipo tena kama haukudhibitiwa ule mlima basi Ikulu haipo. Sasa na milima mengine ipo Chake-Chake pale Michakaini kuna minara ya *TTCL* hivyo ijengewe uwezo ili ile milima iweze kuishi muda mrefu sana *otherwise* miundombinu itakufa.

Mhe. Naibu Spika, pale Mtambile juzi nusra mnara wa *ZANTEL* uanguke ungeuwa vitu vingapi na sijui kama sasa hivi unajengeka, haujengeki

umeteremka wote umebakisha vyuma vinaning'inia. Kwa hivyo, milima kama ina nafasi yake basi ijengewe watu wa mazingira waweze kukaguliwa wafanye kitu kama hicho.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka nizungumze na haya mabwawa ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia. Mheshimiwa mabwawa ambayo sasa hivi nchi yetu haina udhibiti wala uwezo wa kuzuia maji. Hatuna maji yakipukutika basi hayana mabonde wala mashimo ya kudhibiti. Nchi za wenzetu hata ukitizama Bara wanaweza kuchimba wakaweza kuya-*store* maji kwa wanyama kwa kila kitu. Mheshimiwa haya ni matatizo mabwawa yetu kama Mwanakwerekwe na maeneo mengine tatizo hili ndio linalotusababishia matatizo, lakini bwawa kama la Mwanakwerekwe lilikuwa na kina kirefu sana chakuweza ku-*store* maji, leo limejaa taka mpaka limebakisha labda mita 5 ambayo ina uwezo wa kuweka maji…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashkuru sana.

Kwa hivyo, mheshimiwa ningeomba yale mabwawa wakati wa jua kali yakaweza kufanyiwa utafiti wa kuzuia maji kuliko kuyasemea kila siku kwamba mabwawa yale yanaua au yanahatarisha. Lakini mheshimiwa nataka nizungumze suala la maafa tena narudi, mheshimiwa Skuli ya Madungu na Skuli ya Michakaini nazo zina hali mbaya za vyoo, hawana maji. Kwa hivyo, ninachotaka kukwambia ni kwamba hakuna choo kinachoweza kutumika Michakaini, hivyo tunaweza tukahatarisha maafa wakati wowote. Kwa hivyo, dharura ichukuliwe ili kuokoa nafasi ile ya vyoo katika Skuli ya Madungu na Skuli ya Michakaini ikiwezekana skuli ifungwe kwani hali ni mbaya kupita kiasi, tena ni mbaya nikisema ni mbaya, mbaya, mbaya sana. Kwa hivyo, ningeomba ikakaguliwe skuli kwa hali ilivyo kabla ya kufika miripuko hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nawashukuru wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi waliochangia, lakini niishukuru Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kunipa nafasi hii ili tuchangie mambo mengi, zaidi ya hayo naunga mkono hoja asilimia mia. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kupata fursa hii ya kuchangia wakati huu wa usiku.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze na mimi kwa shukurani, kwanza naipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yeye mwenyewe binafsi pamoja na Waziri

wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Naibu Waziri kwa jitihada zao kubwa za kumsaidia kazi Mhe. Makamu wa Pili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na mimi sasa niende katika athari za mvua za Masika. Mhe. Naibu Spika, hili suala lazima sisi wengine tulizungumze kwa sababu limetugusa. Mhe. Naibu Spika, na mimi katika jimbo langu athari za mvua za Masika zimejitokeza kwa hatua kubwa sana, katika mvua iliyonyesha tarehe 29 mpaka 30 hii imetuathiri sana. Tarehe 1/05/2017 mimi nilikwenda Pemba niliona athari zilizojitokeza, kwanza nimekwenda katika barabara yetu ya Mgagadu/Kiwani imejitokeza athari kubwa kwa uharibifu wa barabara ile. Barabara ile imeharibika haipungui mita 120 sehemu ambayo imeharibika. Pia nakumbuka Waziri wa Mawasiliano na yeye ameshakwenda pamoja na Naibu wake wameshaiona ile athari iliyojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, wakati huo huo katika Shehia ya Mwambe watu walioathirika kwa kipindi hicho cha mwanzo walikuwa ni watu 63, lakini nyumba 15 zimeanguka yaani hazikaliki. Kwa hivyo, naipongeza serikali yetu ya Zanzibar kwa jitihada zao kwanza Mhe. Mkuu wa Mkoa na Mhe. Mkuu wa Wilaya wameenda na kuangalia sehemu na watu walioathirika. Watu walioathirika na nyumba zilizokuwa hazikaliki wamechukuliwa na familia zao wamehifadhiwa. Kwa hivyo, nawashukuru watu wote walioathirika kwamba wako katika hali ya utulivu na nawaomba waendelee kutulia na serikali inafanya jitihada ili kutazama mtazamo wa kuwasaidia ili warudi katika makaazi yao ya asili.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naiomba ofisi hii ichukue jitihada maalum kwa sababu hizi mvua zinaendelea kunyesha na kila zinaponyesha zinaathiri. Kwa wakati ule tulikuwa na watu…

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa mazungumzo yamezidi sasa hivi, naomba tafadhali tumsikilize mwenzetu mchango wake na yeye ni muhimu. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa wakati ule tulikuwa na watu walioathirika lakini baadae mvua zilipoongezeka na wao waliongezeka kuathirika. Sasa naiomba Ofisi ya Makamu wa Pili ifanye jitihada na wale ambao kuwa wameongezeka na wao wasije kusahauliwa, kwa sababu tunaweza tukaja tukawasaidia wa mwanzo tukawasahau wale walioathirika baadae. Kwa hivyo, naiomba hapa

ifanye utafiti mzuri ili watu wote waliopata athari ikitokea msaada na wao wasije wakasahauliwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa na mimi vile vile niende sehemu nyengine katika *TASAF III*. Kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake kubwa za kuwasaidia wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, *TASAF III* imejikita sana katika kusaidia Kaya masikini, na watu wamefaidika lakini hakuna zuri lisilo ila. Hapa katika kutafuta wale Kaya masikini kiukweli kuna watu masikini zaidi waliachwa wakachukuliwa watu ambao kuwa wana afadhali kidogo. Sasa kwa mara nyengine naiomba ofisi litakapotokea hili kwa zile shehia nyengine basi wajitahidi wale wanaostahiki kupata mwanzo basi wapate mwanzo, na wale watakaokuwa kidogo haijambo basi waachwe ili kupunguza hayo manung'uniko. Kwa sababu manung'uniko na wakati mwengine yako dhahiri. Mheshimiwa utamuona mtu yuko hali mbaya zaidi lakini kaachwa, kachukuliwa mtu ambaye kuwa ana haijambo kidogo. Sasa kwa mara nyengine tunaiomba ofisi ifanye jitihada ya kutafuta na mashirikiano makubwa ili kupunguza hayo maelezo niliyoyasema.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo vile vile niende katika udhibiti wa madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamelizungumza sana suala hili, na mimi vile vile naomba nilizungumze. Kwanza na mimi niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini pia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada kubwa ya kutaka kulidhibiti suala hili la madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hili suala limekuwa ni tatizo, nathubutu kusema sote tuliomo humu hakuna mtu ambaye halijamgusa kutokana na familia yake. Kwa hivyo, naiomba serikali ichukue jitihada kubwa zaidi ili suala hili tuone linamalizika kabisa kabia.

Kwa hivyo, mimi niseme kwamba masuala haya ya kudhibiti madawa ya kulevya kwa uoni wangu mimi ninavyohisi limekuwa ni suala kubwa zaidi kuliko suala la ukimwi. Kwa sababu inawezekana katika familia yako ikawa huna mtu aliyeathirika na masuala ya UKIMWI, lakini masuala ya madawa ya kulevya yupo. Sasa katika kiwango ambacho kimepangiwa yaani Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya imepangiwa milioni 598,900,000/- lakini Tume ya UKIMWI imepangiwa milioni 846,800,000/-. Mimi kwa mawazo yangu naomba kwamba hii pesa iliyopangiwa UKIMWI basi ipangiwe udhibiti wa madawa ya kulevya, na ya madawa ya kulevya iliyopangiwa ije kwenye UKIMWI ili hili suala la udhibiti wa madawa ya kulevya basi lishughulikiwe ipasavyo. Kwa sababu serikali imejikita kwamba inataka kulishughulikia hili suala na suala hili limekuwa zito na zito zaidi, kwa sababu hakuna kijiji hata kimoja hata huko mashamba kilichokuwa hakijafikwa na kadhia hii. Kwa

hivyo, mimi naomba hilo suala namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili hili suala tuliongezee hiyo bajeti kidogo ikue ili na shughuli zifanyike vizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo vile vile niende katika kuratibu masuala ya Muungano. Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze serikali kwa jitihada zake kubwa za kufanya vikao vingi na kutaka haya masuala yaaani hizi kero za Muungano ziondoke ili haya manung'uniko basi yapunguke.

Mhe. Naibu Spika, lakini ninavyokumbuka kwamba nchi yetu ilifanya mchakato wa kupata Katiba Mpya na kiukweli hatua kubwa ilifikiwa na haya yanayozungumzwa kwenye Bunge, kwenye Baraza leo tusingeliyazungumza ingelikuwa lile jambo limefika mwisho. Sasa nadhani tunaomba hili suala lishughulikiwe lifike mwisho ili haya manung'uniko yanayojitokeza basi leo isingelizungumzwa habari ya uchimbaji wa mafuta kwa sababu ingelikuwa ile Katiba inayopendekezwa ilimalizika haya masuala yangekuwa hayazungumzwi tena.

Kwa hivyo, naiomba Ofisi ya Makamu wa Pili alau atakapokuja kufanya majumuisho watuelezee lile suala je liko tena au pale lilipofika ni basi tena tuje tuanze alifu kwa ujiti. Kwa sababu ngoma ikilala inavia. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakapokuja kufanya majumuisho basi atueleze ili tujue na wananchi wajue kwamba je lile jambo lipo au halipo tena na sisi tunataka tujue kwa sababu haya mabishano ya kila siku kasoro, kasoro hizi zinatupeleka pahali pabaya katika Muungano wetu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nizungumzie habari ya Mfuko wa Maendeleo ya Majimbo. Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze serikali kwa jitihada yake kubwa kwa kuwa na mfuko huu na kiukweli unatusaidia kwenye majimbo yetu kwa sababu kama sisi wawakilishi peke yetu kama tunachokipata hakiwezi kikahimili vishindo. Kwa hivyo, tunaiomba serikali ikiwa mambo kidogo yametengenea basi na huu mfuko kidogo uongezwe ili na sisi tuna mambo mengi huko majimboni, na sisi kidogo tupate kujitanua ili tuyatekeleze hayo mambo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo niliyoyazungumza mimi naomba nifikie hapo na nasema mimi naiunga mkono hotuba hii mia juu ya mia isipokuwa yale mambo ambayo kuwa tuliyazungumza kidogo kwamba tuje tupate maelezo tunaomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe maelezo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani naunga mkono hotuba hii. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda uliobakia hautatosha kwa mjumbe mwengine yeyote kuchangia kwa hivyo mpaka kufikia hapa itakuwa kwa siku ya leo nitaakhirisha kikao hadi kesho asubuhi saa 3:00 tukijaaliwa.

(Saa 1:36 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 11/05/2017 saa 3:00 asubuhi)